# KANUNI ZA KUTAFSIRI BIBLIA

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Shepherds Global Classroom ipo ili kuandaa mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuinua viongozi kwa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuzidisha programu za mafunzo asilia kwa kuweka mtaala wenye kozi 20 katika mikono ya wakufunzi katika kila nchi duniani.

Kozi hii inapatikana bure kwa kuipakua katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

Mwandishi mkuu: Dr. Randall D. McElwain

Hakimiliki © 2024 Shepherds Global Classroom

Imetafsiriwa kutoka katika Toleo la Tatu la Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Tafsiri hii ni hakimiliki ya mmiliki halali na wanashirikisha chini ya leseni mbalimbali.

Ispokuwa imetajwa vinginevyo, maandiko yote yanatoka katika Swahili Union Version (SUV): Hakimiliki – 1952, 1997: kwa Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

**Angalizo la vibali:**

Nyenzo hizi zinaweza kuchapishwa na kusambazwa bure katika chapisho au mfumo wa kidigitali kwa mwongozo ufuatao: (1) Yaliyomo katika kozi hayatakiwi kubadilishwa kwa namna yeyote; (2) Nakala hazipaswi kuuzwa kwa faida; (3) Taasisi za Elimu ziko huru kutumia au kutoa nakala ya kozi hii, hata kama watabadilisha kiwango cha ada; na (4) Hairuhusiwi kutafsiri kozi hii pasipo kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

# Yaliyomo

Muhtasari wa Kozi ........ 5
(1) Utangulizi wa Kutafsiri Maandiko ........ 7
(2) Uchunguzi: Kuutazama Mstari ........ 17
(3) Uchunguzi: Kuangalia Sehemu Kubwa ........ 31
(4) Tafsiri: Utangulizi ........ 49
(5) Tafsiri: Muktadha ........ 57
(6) Tafsiri: Aina za Fasihi ........ 67
(7) Tafsiri: Kujifunza Neno ........ 93
(8) Tafsiri: Kanuni za Jumla ........ 103
(9) Matumizi ........ 113
(10) Kufanyia kazi Kujifunza Kifungu ........ 123
Nyenzo za Kujifunzia Biblia ........ 133
Vyanzo Vinavyopendekezwa ........ 137
Rekodi ya Mazoezi ........ 139

# Muhtasari wa Kozi

Kozi hii inatoa utangulizi wa kanuni za msingi za kutafsiri Biblia. Masomo mengi katika kozi hii yana msingi katika Kitabu maarufu, *Living by the Book*, cha Howard na William Hendricks. Endapo unaweza kukipata kitabu hiki, utaweza kupata mazoezi ili kufanyia kazi kanuni zinazofundishwa katika kozi, vile vile utapata majadiliano zaidi katika kila kanuni. Hata hivyo, kitabu hakihitajiki kwa ajili ya kozi. Nyenzo zote zinazohitajika zimejumuishwa katika masomo haya.

Mwanafunzi anatakiwa kusoma kila Somo kabla ya kuja darasani. Unapaswa kupanga kuwa na dakika 90-120 kwa kila kipindi, Pamoja na muda wa mazoezi nje ya darasa. Kwa sababu kozi hii ina msingi katika mazoezi ya vitendo, unaweza kupenda kugawanya somo katika vipindi zaidi ya kimoja. Hii inaweza kuwapa wanafunzi muda zaidi wa kufanya shughuli.

Masomo yanajumuisha **shughuli** kadhaa kwa ajili ya kutendea kazi kanuni zinazofundishwa katika somo. Ni muhimu kwamba mwanafunzi achukue muda kufanya shughuli hizi kwa umakini. Shughuli hizi zinatembea katika Maandiko mengi tofauti tofauti. Usikimbilie kumaliza somo. Kwa sababu shughuli nyingi kati ya hizi zitakuwa mpya kwa mwanafunzi, chukua muda darasani ili kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anaelewa namna ya kukamilisha shughuli hizi. Lengo la msingi si kupata jawabu fulani; lengo la msingi ni kukuza stadi katika kujifunza na kutafsiri Biblia.

Mwishoni mwa kozi hii, mwanafunzi atakuwa amesoma vifungu kadhaa vya Maandiko. Kila mwanafunzi atunze **nakili zake alizoziandika wakati wa kozi katika daftari lake** kwa ajili ya matumizi ya baadae. Kazi zilizofanyika katika kozi hii zitakuwa msaada kwa ajili ya kuandaa ujumbe na somo la Biblia.

**Maswali ya majadiliano** na **shughuli za darasani** zimeoneshwa kwa dondoo mshale ►. Kwa habari ya maswali ya majadiliano, wanafunzi wajadili majibu. Jaribu kuhakikisha kwamba wanafunzi wote darasani wanahusika katika majadiliano. Kama itabidi, waite wanafunzi kwa majina yao.

Kila mwanafunzi atafanyia kazi **mradi wa kozi** katika kipindi chote cha kozi. Baada ya Somo la 10, watawasilisha darasani au watakusanya **kazi** zao kwa kiongozi wa darasa. Maelekezo kwa ajili ya mawasilisho au **kazi** yametolewa katika sehemu ya Mazoezi ya Somo la 10.

Mazoezi **mengine** kadaa pia yamejumuishwa mwishoni mwa Somo la 2 na 7. Wanafunzi wamuoneshe kiongozi wa darasa kazi zilizokamilika lakini watunze nakala ya kazi zao katika shajala zao.

# Somo la 1
# Utangulizi wa Kutafsiri Maandiko

## Malengo ya Somo

(1) Kufahamu kwa nini kujifunza Biblia kwa kina ni muhimu kwa mkristo.

(2) Kuwa na uwezo wa kutaja hatua tatu muhimu za kujifunza Biblia.

(3) Anza mchakato wa kujifunza kwa umakini kifungu cha andiko kilichochaguliwa.

(4) Kutambua umuhimu wa kuangaziwa na Roho Mtakatifu kwa ajili ya kutafsiri Biblia.

## Utangulizi

Moja ya kusudi ya kozi hii ni kukusaidia kukua katika ujifunzaji wako binafsi na matumizi ya Maandiko. Hatua ya kwanza ni kutathmini kwa uaminifu mwenendo wako wa sasa wa usomaji wa Biblia.

► Chukua dakika kadhaa kujadili mwenendo wako wa sasa wa usomaji wa Biblia. Huu si wakati wa kukosoana; ni wakati wa kutafakari juu ya swali, "Ni kwa namna gani ninasoma Neno la Mungu?" Haya hapa ni maswali ya kutafakari:

- Ni mara mara nyingi kiasi gani ninasoma Biblia?
- Ninaposoma Biblia, ninatumia muda kiasi gani?
- Ni kwa namna gani ninachagua kifungu cha kusoma?
- Je, ninaelewa kile ninachokisoma?
- Je, ninakumbuka ninachokisoma?
- Je, ninaweza kutumia katika Maisha yangu?
- Ni sababu gani 2-3 zinazonifanya nisisome Biblia zaidi ya ninavyosoma sasa?

Tinghao, ni mkristo wa Taiwani, amekuwa mkristo wa miaka 15, lakini anaonesha viashiria vichache vya ukuaji wa kiroho. Huku kukosa ukuaji wa kiroho kulimsumbua sana. Baada ya ibada ya jumapili, masumbufu yake yalikuwa wazi. "Mchungaji, unaniambia kusoma Biblia. Unasema kwamba Mungu atazungumza na mimi kupitia neno lake. Nimekuwa nikijaribu kusoma kila asubuhi, na halisemi chochote kwangu. Shida ni nini?"

Mchungaji akajibu, "Tinghao, niambie unasoma Biblia kwa **namna gani**." Majibu ya Tinghao yalionesha jambo muhimu sana katika masumbufu yake. Alijibu, "Kila asubuhi kabla ya kazi, ninafungua Biblia na ninasoma mstari." Mchungaji akafuata, "Je, unasoma kitabu chote cha Biblia au hata kumaliza sura moja kabla ya kuendelea?" "Hapana, Ninasoma tu mstari mmoja kila asubuhi – popote pale ambapo Biblia yangu itafunukia. Na haijanisaidia sana!"

Ili kumsaidia Tinghao kuelewa tatizo la kusoma Biblia kwa mtindo wake, mchungaji alimuomba afungue Biblia na kusoma mstari wa kwanza aliouona. Tinghao akasoma, "Na

watu wa Negebu wataumiliki mlima wa Esau; na watu wa Shefela watawamiliki Wafilisti; nao watalimiliki konde la Efraimu, na konde la Samaria, na Benyamini atamiliki Gileadi" (Obadia 1:19).

Kisha mchungaji akamuuliza Tinghao maswali kadhaa. "Negebu ni wapi? Shefela ni wapi? Wapi ni nchi ya Efraimu? Samaria? Benyamini? Gileadi?" Jibu kwa kila swali lilikuwa ni "Sifahamu." Juma lililofuata walianza kujifunza Biblia juu ya "Namna ya kusoma Biblia." Katika majuma kadhaa, Tinghao alianza kujifunza kanuni kadhaa za kutafsiri Biblia. Alijifunza kuelewa ni kwa jinsi gani Maandiko yanazungumza na sisi leo.

Lengo la kozi hii ni ili kukusaidia kujifunza na kutendea kazi kanuni za msingi za kutafsiri Biblia. Kupitia masomo na mazoezi haya, utapata nyenzo za kukusaidia kulielewa Neno la Mungu, kulitumia katika maisha yako, na kuwafundisha wengine.

## Kwa nini nijifunze Biblia?

Baadhi ya watu wanakwepa kusoma Biblia kwa sababu wanaamini ni ngumu kuielewa. Wengi wa wanaoamini kwamba Biblia ni neno la Mungu hawafahamu namna ya kuitafsiri na kuitumia. Kujifunza Biblia ni kazi ngumu. Je, inastahili kazi hiyo? Kwa nini tujifunze Biblia?

### Mungu Amejifunua Mwenywe Kupitia Maandiko

Maandiko yanatuonesha sisi Mungu ni nani. Neno la Mungu ni maelezo ya asili ya Mungu (Zaburi 119:15, 27). Maandiko yanatuonesha sisi ni namna gani Mungu anafikiri, nini ni muhimu kwake, ni kwa namna gani anahusiana na watu, na ni kwa namna gani ametenda katika historia ya mwanadamu. Sheria ya Mungu (kile anachohitaji) kinaakisi sifa zake, haki yake, na hekima yake (Zaburi 119:137). Kila wakati tunaposoma Biblia, tunatakiwa kuweka umakini wetu kwenye kile inachoonesha kuhusu Mungu.

Maandiko yanamuonesha Mungu kwa anayeabudu. Pia yanaongoza mwitikio wa anayeabudu kwa Mungu, yakionesha namna tunayotakiwa kuishi.

### Biblia ni Taa

Mzaburi analilinganisha Neno la Mungu na taa ambayo inaongoza njia ya namna ya kuishi (Zaburi 119:105). Biblia ni kweli ya Mungu inayotufundisha sisi namna ya kufikiri na kuishi.

► Soma Zaburi 19:7-11, Zaburi 119:160, na 2 Timotheo 3:16-17.

Neno la Mungu ni chanzo cha mafundisho sahihi. Biblia ina maarifa yote yanayohitajika kwa ajili ya wokovu na utakatifu. Kanuni hii haimaanishi kwamba tunaweza kuelewa kila kitu katika maandiko bila msaada mwingine. Haimaanishi kwamba tamaduni si za muhimu. Inamaanisha kwamba Neno la Mungu ni mamlaka ya mwisho kwa mwamini.

Kwa sababu Neno la Mungu ni chanzo cha kweli, maarifa ya maandiko yanatuandaa na kututengeneza sisi kwa huduma. Tunapolifundisha Neno la Mungu kwa usahihi, tunafundisha kwa mamlaka ya Mungu. Kweli ni yake, sio yetu.

**Biblia ni maziwa ya kiroho**

Petro alisema kwamba tunapaswa kuitamani Biblia kwa kiwango kile ambacho mtoto anayatamani maziwa (1 Petro 2:2). Kama vile ambayo mtoto anayahitaji maziwa ili kukua kimwili, mkristo anatakiwa kuwa na Maandiko ili kukua kiroho. Pasipo kuwa na mlo wa mara kwa mara wa Neno la Mungu, hatutakua kiroho.

Tunapojifunza stadi za kutafsiri Biblia na kufanya mazoezi ya kung'amua kweli ya Mungu kutoka katika Neno la Mungu, tunakua (Waebrania 5:14). Uwezo wetu wa kutumia Neno la Mungu kufundisha wengine utakua.

**Biblia ni asali tamu**

Mzaburi analinganisha Neno la Mungu na asali (Zaburi 19:10, Zaburi 119:103). Asali ni tamu na yenye afya. Tunatakiwa kufurahia kujifunza Neno la Mungu, na si kuona kuwa ni kazi isiyovutia. Kama vile tu mwanajeshi aliye vitani anavyofurahia kusoma barua iliyotoka nyumbani, tunatakiwa kufurahia tunaposoma Biblia, barua ya Mungu kwa watoto wake.

Kijana wa kiyahudi alianza shule ili kwamba aweze kujifunza kusoma sheria, mwalimu aliweka asali katika herufi za kwanza za silabi na mtoto angejitahidi kulamba ukurasa ili aonje utamu wa asali. Mwalimu alitumia somo hili la vitu akitarajia kwamba "mtoto atajifunza kuhusianisha [sheria] na Furaha na ladha njema."[1]

**Biblia ni upanga wa Roho**

Neno la Mungu ni silaha yetu katika vita za kiroho (Waefeso 6:17). Yesu alipata majaribu kule nyikani, aliyajibu mashambulizi ya Shetani kwa kunukuu kutoka Kumbukumbu la Torati (Mathayo 4:1-11).

Maandiko yanatutia nguvu kwa ajili ya ushindi wa kiroho na huduma yenye ufanisi. Kupitia kujifunza Biblia, tunaandaliwa kwa ajili ya kupinga mafundisho potofu, ili kulikuza kundi letu katika mafundisho sahihi, na kuhudumu kwa ufanisi katika ulimwengu wa sasa.

**Sababu zisizo sahihi za kujifunza Maandiko**

► Soma Waebrania 4:12-13.

Zipo sababu nzuri sana za kujifunza Maandiko, lakini kuna wakati watu wanasoma au wanajifunza Maandiko wakiwa na msukumo mbaya.

Baadhi ya watu wanaweza kujifunza Maandiko ili tu kukusanya ushahidi ili kutetea hoja au mawazo yao. Pengine hata wanataka kutumia ufahamu huo ili kuwadhibiti wengine chini ya ushawishi wao.

---

[1] Efraim Rubin, "Honey in Jewish Law, Lore, Tradition, and More," Ilitafutwa November 15, 2023, https://www.chabad.org/library/article_cdo/aid/2697265/jewish/Honey-in-Jewish-Law-Lore-Tradition-and-More.htm

Baadhi ya watu wanajifunza Maandiko kwa sababu za kiburi. Pengine wanafikiri watapata vyeo vya kiroho na kuwa juu ya watu wengine. Pengine wanapenda watu wengine wawafikirie na wawasifu kwa mafanikio yao. Au pengine wanafikiri kwamba kujifunza Maandiko kutawafanya wao kupata upendeleo kwa Mungu.

Hizi zote ni sababu zisizo sahihi za kusoma au kujifunza Neno la Mungu. Waebrania 4:12-13 inaonesha nia njema kuhusiana na Maandiko. Badala ya kutumia Maandiko ili kukamilisha malengo binafsi, tunatakiwa kukumbuka kwamba hili ni Neno la Mungu, na si letu. Tunatakiwa kujifunza tukiwa na mtazamo wa kumuheshimu Mungu. Biblia ni mamlaka yetu, na tunatakiwa tuitii. Tunapolifundisha kwa wengine, tunatakiwa kufanya hivyo kwa unyenyekevu.

Tunapojifunza na kulifundisha Neno la Mungu kwa namna hii, litafunua dhambi na makosa katika maisha yetu na kutuonesha namna ya kuacha. Litabadilisha maisha yetu na maisha ya wale tunaowatumikia na kuwaongoza.

## Ni kwa namna gani nijifunze Biblia?

► Ni mchakato gani ambao unautumia kwa sasa unapojifunza kifungu cha maandiko? Jadili hatua mahususi ambazo unachukua ili kupata maana ya andiko la Biblia.

Tinghao anakubali kwamba kujifunza Biblia ni muhimu. Hata hivyo, hakujua namna ya kujifunza maandiko. Alihitaji njia.

Kozi hii inakusudia kupata njia kwa ajili ya ujifunzaji wa Biblia wenye ufanisi. Wachungaji wanaweza kutumia hatua hizi tatu katika maandalizi ya ujumbe. Waalimu wa Biblia wanaweza kutumia hatua hizi kuandaa masomo ya Biblia. Kila mwamini anaweza kunufaika na kutumia njia hii kwa ajili ya kukua kiroho kibinafsi.

Njia inayofuatwa na kozi hii inahusisha hatua tatu.

### Uchunguzi

Katika hatua hii, tunajiuliza, “Ninaona nini katika Biblia?” katika hatua hii, tunachunguza taarifa nyingi kwa kadiri inavyowezekana kuhusiana na Maandiko. Wasomaji wengi huruka hatua ya Uchunguzi na kwenda moja kwa moja katika tafsiri. Hatuwezi kuelewa Maandiko kikamilifu hadi tumechunguza nini yanasema. Katika mchakato wa Uchunguzi, tunaangalia katika taarifa za ndani za andiko lenyewe. Tutajifunza kutambua taarifa ambazo ni muhimu katika andiko. Mahususi kabisa, tutajifunza maneno, muundo, aina ya fasihi, na mazingira.

#### *Maneno*

Tunapojifunza kitabu cha Biblia, tunaangalia maneno ambayo yametumika mara kadhaa katika kitabu chote. 1 Yohana inatumia namna mbalimbali ya neno kujua zaidi ya mara 30 katika sura 5. Unaposoma waraka wa Yohana, unaweza kuanza kwa kulifuatilia neno hili katika kitabu. Orodha ya mahali ambapo Yohana amelitumia neno hili itatusaidia sisi kuanza

kutafsiri ujumbe wake. Ili kuelewa ujumbe wa Yohana, tunaweza kuuliza, "Yohana anasema tunaweza kujua nini?" na "Zipi ni sifa za wale wanaojua?"

### *Muundo*

Vitabu vya Biblia vimetengenezwa kwa umakini sana chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu. Unaposoma kitabu kama Injili ya Yohana, utaweza kuona kwamba, Yohana ameipanga Injili yake katika alama saba ambazo zinamuonesha Yesu ni nani. Tunapochunguza muundo wa kitabu, unatupa sisi uelewa mzuri wa kusudi la Yohana.

Tunaposoma kifungu cha Maandiko, tunaweza kuona kwamba muundo unafuata habari (kama katika Luka 9:28-36). Kinaweza kutupa sababu ya kuhitimisha (kama katika Warumi 6:1-13). Unaweza kutumia taarifa kutupa orodha ya dondoo (kama katika Waefeso 6:13-18). Pia kuna aina nyingine ya muundo.

### *Aina ya Fasihi*

Paulo aliandika nyaraka zilizopangwa vizuri sana ambazo zilitoa hoja zake kama ambavyo mwanasheria anajenga hoja zake kuelekea juu kileleni kwenye dondoo kuu. Ili kusoma vizuri Warumi au nyaraka nyingine, unatakiwa kufuata mtiririko wa mawazo wa Paulo.

Kinyume chake, Yona ni habari fupi ya kihistoria iliyoandikwa ili kuelezea upendo wa Mungu kwa watu wote. Ili kukisoma vizuri, lazima uulize, "Ni kitu gani kinaifanya habari hii kuwa ya kushangaza, na isiyo ya kawaida?" Hapa sasa unakuwa tayari kutafsiri kitabu cha Yona kwa kuuliza, "Taarifa za kina za habari hii zinamaanisha nini?"

### *Mazingira*

Hapa tunauliza maswali kama, "Paulo alikuwa wapi alipoandika waraka kwa Wafilipi akiwa na ujumbe wake wa furaha?" alikuwa Rumi, akingojea kesi yake na inawezekana akingojea hukumu yake ya kifo. Mazingira yanatufanya tuangalie sababu za Paulo kusema alikuwa na furaha, kwa sababu alikuwa na furaha hata kama binafsi alikuwa katika hali mbaya.

"Yohana alikuwa wapi wakati mbingu zinafunguka kufunua mpango wa Mungu wa milele katika kitabu cha Ufunuo?" alikuwa uhamishoni katika kisiwa cha Patimo. Kipindi cha mateso makali kilifanya ujumbe wa ushindi wa Mungu kuwa wa kutia moyo katika Imani.

## Tafsiri

Katika hatua hii, tunauliza, "Biblia inamaanisha nini?" Baada ya kuwa tumekusanya taarifa nyingi za Uchunguzi kwa kadiri inavyowezekana, tunauangalia ujumbe wa maandiko. Tutajifunza kutafuta mada kuu ambayo inaunganisha kitabu pamoja na ujumbe wa sura na mistari husika. tutauliza, "upi ni ujumbe wa kitabu hiki kwa wapokeaji wa kwanza?" Tutatafuta kanuni ambazo ni kweli kwa nyakati zote, mahali pote, na tamaduni zote.

**Matumizi**

Katika hatua hii, tunauliza, "Ni kwa namna gani ninaitumia Biblia katika maisha na huduma leo?" Haitoshi tu kuelewa maana pasipo kuitendea kazi katika maisha yetu.

Katika kitabu chake, Howard Hendricks anashauri maswali mawili kuhusiana na matumizi:[2]

1. Inafanyaje kazi kwangu? Hii inaangazia matumizi ya andiko katika maisha yangu.
2. Inafanyaje kazi kwa wengine? Hii inaangazia matumizi ya andiko katika maisha ya wale ambao ninawaahudumia.

Kule Uingereza kuna mhadhiri wa chuo kikuu ambaye ni msomi anaheshimika sana wa historia ya kanisa. Kitaaluma, anaifahamu Biblia vizuri sana; kibinafsi, anakana Imani yeyote kuhusiana na Mungu na neno la Mungu. Mtu huyu anafahamu vizuri kuhusiana na Uchunguzi na tafsiri. Kwa bahati mbaya, hajawahi kutumia kweli ya maandiko katika maisha yake.

Yakobo anamuelezea mtu wa aina hii kama hivi: "Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo" (Yakobo 1:23-24). Mhadhiri kule Uingereza ni kisa cha juu sana; hata hivyo, wapo watu wengi sana ambao wanafahamu maandiko yanasema nini, lakini wanashindwa kuyaishi katika maisha yao ya kila siku. Ujifunzaji wa kweli wa Biblia unatakiwa kupelekea katika kutendea kazi kivitendo.

## Kazi ya Roho Mtakatifu katika Tafsiri

► Je, mwamini anaweza kuelewa maana ya maandiko?

Jibu la swali hili ni "ndiyo, lakini kwa kiasi tu." Katika kozi hii, tunajifunza mchakato wa kutuongoza katika tafsiri zetu. Hatua hizi zitatusaidia kuelewa ujumbe wa neno la Mungu. Biblia, kusoma kama vitabu vingine, kutafunua kweli nyingi kwa msomaji yeyote.

Hata hivyo, bila kuangaziwa na Roho Mtakatifu, uelewa wa mtu utakuwa finyu. Usomaji wa kitaaluma pekee kamwe hauwezi kufunua kweli ya Kiroho. Paulo anaandika:

> Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali **yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.** Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni (1 Wakorintho 2:11-14).

---

[2] Howard G. Hendricks and William D. Hendricks, Living by the Book (Chicago: Moody Publishers, 2007)

Asiyeamini anaweza kuelewa baadhi ya ujumbe wa andiko, lakini kweli za ndani za Biblia zinafunuliwa kupitia kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Kusoma maandiko ni zaidi ya kupata taarifa; inahitaji imani na utii. Ni hadi tutakapojitia katika mamlaka ya Neno la Mungu, Roho wa Mungu hataweza kufanya kazi hii ya kutubadilisha katika maisha yetu. Kwa sababu hii:

1. Kujifunza kwetu kunatakiwa kutanguliwa na maombi. Tunatakiwa kumuuliza Roho Mtakatifu kutuongoza katika kujifunza kwetu. Yakobo anaandika, "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa" (Yakobo 1:5).

2. Ujifunzaji wetu wa Maandiko unatakiwa kufuatwa na mwitikio binafsi. Lengo la kujifunza Biblia ni zaidi ya uelewa wa kiakili wa kupata taarifa; lengo ni kubadilishwa kibinafsi. Kama hatutabadilishwa kupitia kujifunza kwetu, tumekosa kusudi la kujifunza. Badiliko linakuja tu kupitia Roho Mtakatifu.

Katika mfano wa Yesu kuhusiana na mpanzi na mbegu. Baadhi ya mbegu zilianguka njiani na zililiwa na ndege. Mbegu nyingine hazikuwa na mizizi zikafa jua lilipokuwa kali. Mbegu nyingine zilisongwa na miiba. Lakini mbegu nyingine zilianguka katika udongo mzuri na kuzaa matunda. Yesu alielezea kwamba udongo mzuri ni yule mtu ambaye analisikia neno la Mungu na kulielewa (Mathayo 13:3-23). Mfano huu unaonesha kwamba inawezekana kulisikia neno la Mungu pasipo kulielewa. Tunalielewa neno la Mungu vema endapo tu tutaiweka wazi mioyo yetu kwa sauti ya Roho Mtakatifu.

**Somo la 1 Dondoo Muhimu**

(1) Sababu za Kujifunza Biblia:

- Mungu Amejifunua Mwenywe Kupitia Maandiko.
- Biblia ni Taa.
- Biblia ni Maziwa ya Kiroho.
- Biblia ni Asali Tamu.
- Biblia ni Upanga wa Roho.

(2) Zipo hatua tatu katika mchakato wa kujifunza Biblia.

- Uchunguzi: Ninaona nini katika Biblia? Jifunze:
    - Maneno
    - Muundo
    - Aina ya Fasihi
    - Mazingira
- Tafsiri: Biblia inamaanisha nini?
- Matumizi: Ni kwa namna gani ninaitumia Biblia katika maisha na huduma leo? Uliza:
    - Inafanyaje kazi kwangu?
    - Inafanyaje kazi kwa wengine?

(3) Tunatakiwa kuangaziwa na Roho Mtakatifu wakati tunajifunza Biblia. Kwa sababu hii

- Kujifunza kwetu kunatakiwa kutanguliwa na maombi.
- Ujifunzaji wetu wa Maandiko unatakiwa kufuatwa na mwitikio binafsi.

## Somo la 1 Zoezi

Kwa kuanza mchakato wa kutafsiri, chagua kifungu kimojawapo kati ya vinavyofuata.

- Kumbukumbu la Torati 6:1-9
- Yoshua 1:1-9
- Mathayo 6:25-34
- Waefeso 3:14-21
- Wakolosai 3:1-16

Utajifunza Maandiko haya wakati wote wa kozi. Kwa somo hili la kwanza, soma maandiko kwa umakini. Tengeneza nakili katika maeneo matatu:

1. Uchunguzi: Orodhesha taarifa nyingi kwa kadiri unavyoweza kuhusiana na andiko ulilochagua. Kwa kutegemea andiko, taarifa zenu zitatofautiana. Baadhi ya maswali ambayo yatakusaidia ni haya:
    - Matukio yaliyonakiliwa katika andiko hili yalifanyika wapi?
    - Nani ni wahusika katika andiko hili?
    - Andiko hili linaagiza nini?
    - Ni maneno gani ambayo yanarudiwa rudiwa katika andiko hili?
2. Tafsiri: Katika sentensi 2-3, fupisha ujumbe wa kifungu cha maandiko.
3. Matumizi: Orodhesha njia 2-3 ambazo unaweza kutumia andiko hili katika maisha na huduma yako.

# Somo la 2
# Uchunguzi: Kuutazama Mstari

## Malengo ya Somo

(1) Kuelewa umuhimu wa kusoma maandiko kwa umakini.

(2) Kuuliza maswali muhimu kwa kila mstari unaojifunza.

(3) Kuwa na mpango wa kujifunza maandiko kwa mpangilio maalumu.

(4) Kufanyia kazi utengenezaji wa Uchunguzi wa kina wa kifungu kilichochaguliwa.

## Utangulizi

> "Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika sheria yako."
>
> - Zaburi 119:18

► Pata mwanakikundi mmoja au wawili kutoka katika kundi lako waelezee safari yao ya kufika katika eneo mnalokutana kwa ajili ya kozi hii. Wajumuishe taarifa nyingi kwa kadiri inavyowezekana. Je, mlipita karibu na migahawa, makanisa, au biashara? Je, mlipita vibao vingapi vya kusimama au mlipita taa za barabarani ngapi? Mlikatisha kona mara ngapi? Je, mlikutana na chochote ambacho si cha kawaida, kitu chochote ambacho kwa kawaida hakiko katika safari yenu? Kila mmoja atakapomaliza kuelezea, jadilini ni kiasi gani kimechunguzwa na kiasi gani hakikuchunguzwa.

Juma anapomaliza kusoma Biblia, humalizia na picha akilini. Ukimuomba Juma asome na kufupisha Marko 1:29-31, angesema, "Yesu aliondoka kwenye Sinagogi kule Galilaya akiwa na wanafunzi wake wanne (Simoni, Andrea, Yakobo na Yohana). Walikwenda nyumbani kwa Simoni ambapo Mama mkwe wake na Simoni alikuwa anaumwa na homa kali. Yesu akamuinua kwa mkono wake na homa ikamwacha mara. Alikuwa mzima sana kiasi kwamba aliwaandalia chakula. Hakuhitaji hata muda wa kupumzika ili kupona."

Yusuf akisoma Biblia, yeye husoma maneno lakini huona taarifa chache. Ukimwambia Yusuf asome na kufupisha Marko 1:29-31, angesema, "Yesu alitembelea nyumbani kwa Simoni na kumponya mtu mmoja."

Ni msomaji gani kati ya hawa wawili alichunguza? Ni msomaji gani ataikumbuka habari kwa muda mrefu? Ni msomaji gani ana taarifa za kutosha ambazo zinaweza kuwa msingi wa tafsiri ya habari hii? Jibu liko wazi. Juma aliona kile kilichotokea katika Marko 1:29-31. Yusuf alisoma sura, lakini hakuchunguza.

Hatua ya kwanza ya kujifunza Biblia ni uchunguzi. Katika hatua hii, tunauliza, "ni nini ninachokiona katika sehemu hii ya maandiko? Msingi wa ufanisi katika kutafsiri Biblia ni kuchunguza sana kwa kadiri inavyowezekana. Katika somo hili, tutajifunza kuchunguza taarifa muhimu katika mstari. Uwe na subira unapofanya hivi, unapochunguza zaidi, ndivyo unavyopata nyenzo kwa ajili ya tafsiri yako.

## Uchunguzi kutoka katika Mstari

Matendo ya Mitume 1:8:

> Lakini mtapokea nguvu
> akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu,
> nanyi mtakuwa mashahidi wangu
> katika Yerusalemu
> na katika Uyahudi wote
> na Samaria,
> na hata mwisho wa nchi.

Ni nini tunaweza kuchunguza katika mstari mmoja?

### Neno la kwanza ni lipi?

"Lakini." *Lakini* ni kiunganishi ambacho kinaunganisha mstari uliopita. katika Matendo ya Mitume 1:6, wanafunzi walimuuliza, "Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?" Sasa kwa sababu umefufuka kutoka wafu, je, utausiamaisha ufalme wako? Yesu anajibu kwa matamko mawili:

- "Si kazi yenu kujua nyakati wala majira…" (Matendo ya Mitume 1:7). Huu ni wajibu wa Baba.
- "Lakini mtapokea nguvu… nanyi mtakuwa mashahidi wangu." Huu ni wajibu wenu.

### Nani Wanahusika?

"Nanyi." Yesu anazungumza na nani? Mitume (Matendo ya Mitume 1:2, 4). Chukua muda kuuliza, "Mitume hawa ni nani?" Orodhesha kila unachofahamu kuhusiana na mitume. Nani katika mstari huu unahusiana, inaonesha nguvu ya ajabu ya kubadilisha ya Pentekoste.

- Wao ni Wayahudi; Yesu anawatuma Samaria!
- Hawakuwa na uwezo wa kumponya kijana aliyepagawa na pepo (Marko 9:14-29); watapokea nguvu.
- Walikimbia kwa hofu wakati Yesu anakamatwa (Mathayo 26:56); watakuwa mashahidi wake hadi mwisho wa nchi.

### Kitendo cha Sentensi ni nini?

"Mtapokea." Kitendo kinatuambia ni nini kitatokea. Katika hali hii, wakati wa kitendo unaagazia kitu ambacho watakipokea baadae.

### Watapoka nini?

"Nguvu." Kitabu cha Matendo ya Mitume kitaonesha nguvu hii katika huduma za mitume.

► Hii inakufanya wewe uanze. Fanyia kazi mistari inayofuata, kwa kujibu maswali haya:

- **Watapokea lini?**
- **Nani atawapa nguvu?**
- **Matokeo ya nguvu ni nini?** (Nguvu inatangulia ushuhuda. Matokeo ya asili ya nguvu itakuwa ni shahuku ya kushirikisha Injili na wengine.)
- **Watakuwa mashahidi wa nani?**
- **Watashuhudia wapi?** (unafahamu nini kuhusiana na maeneo hayo manne? Ni nini maalumu kuhusiana na Samamria, je, mitume hawa wa Kiyahudi wangetaka kwenda huko?)

## Kuza Nguvu zako za Uchunguzi

Neema alikuwa na uoni hafifu. Alipokuwa shuleni, alikuwa hawezi kumuona mwalimu wake vivuri. Alikuwa hawezi kusoma maneno katika ubao wa chaki akiwa mbele kabisa ya darasa. Kisha siku moja, akaanza kuvaa miwani ya macho. Ghafla, aliona vitu ambavyo hakuviona hapo kabla! Aliweza kuona uso wa mwalimu wake vizuri. Aliweza kusoma kwa urahisi kile kilichoandikwa katika ubao. Alikuwa na furaha!

Uchunguzi makini ni sawa na kuvaa miwani ya macho ili kurekebisha uoni hafifu. Kujifunza jinsi ya kuchunguza maandiko kunakuza uelewa wako wa kile ambacho maandiko yanasema.

Kufanyia mazoezi Matendo ya Mitume 1:8 inaonesha ni kwa umakini kiasi gani umechunguza kile unachokisoma. Hebu tujadili maadhi ya dondoo kwa ajili ya kukuza nguvu zako za uchunguzi. Utajifunza maswali ya kuuliza ambayo yataleta maandiko katika uelewa wa wazi. Kisha utafanya mazoezi ya kusoma mistari mingine.

Unaposoma mstari katika Biblia, tafadhali usiseme, "tayari ninaufahamu mstari huu!" badala yake, muulize Mungu afungue macho yako kwa neno lake kwa namna mpya. Stadi katika somo hili zitakusaidia kusoma kwa uelewa mpya.[3]

### Soma ili Kupata Uelewa

Mvulana wa miaka 10 aliamua Kamba atasoma Biblia yote kwa mwaka kila mwaka. Alikuwa ameamua vizuri; kwa bahati mbaya, alikuwa hajui namna ya kusoma Biblia kwa ufanisi. Alikuwa na kalenda inayoonesha kiasi gani cha kusoma kila siku, lakini mara kwa mara aliachwa nyuma. Jumapili mchana, alijaribu kukimbizana nayo. Angeangalia kalenda ili kuona kwamba amechwa nyuma kwa sura 20 (katika Mambo ya Walawi!). Kwa hiyo, angesoma Mambo ya Walawi yote mchana huo. Angesoma kwa haraka kwa kadiri

---

[3] Hatua katika somo hili zinatoka katika Sura ya 8-17 ya *Living by the Book,* by Howard G. Hendricks na William D. Hendricks (Chicago: Moody Publishers, 2007). Unaweza kupata mazoezi ya nyongeza na maelezo kwa kusoma sura hizo.

alivyoweza, akijaribu kufika mwisho. Dakika 10 baada ya kumaliza, asingeweza kukuambia ujumbe wa Mambo ya Walawi. Alikuwa anasoma bila uelewa.

Kusoma ili kuelewa ni kazi ngumu. Biblia inaelezea Kuutafuta ukweli kama hivi: "Ukiutafuta kama fedha, Na kuutafutia kama hazina iliyositirika; Ndipo utakapofahamu kumcha BWANA, Na kupata kumjua Mungu" (Mithali 2:4-5). Soma andiko kwa makini. Uliza maswali. Andika nakili. Soma na akili yako.

Wakati mwingine unaweza kupata uelewa kwa kuyasema maandiko kwa maneno yako. Wakati kuyasema maandiko kwa maneno yako sio kutafsiri, kunaweza kukusaidia kufikiri kwa kina kuhusiana na maana ya andiko.

**Uliza Maswali Unaposoma**

Ufunguo wa kusoma na akili yako ni kuuliza maswali.

► Soma Luka 24:13-35 kabla ya kuendelea na sehemu hii. Wakati unajifunza hili somo, rejea tena katika Luka 24 ili kujibu kila swali.

**(1) Nani?**

Watu hawa ni nani katika andiko? Unafahamu nini kuhusiana na kila mtu?

Watu katika Luka 24:13-35 ni nani? Cleopa na mwenzake ambaye hajatajwa kwa jina[4] walikuwa wanasafiri kwenda Emau siku ya ufufuo. Walikuwa ni wafuasi wa Yesu ambao waliifahamu Miujiza yake na mafundisho yake. Jumapili hii, walikuwa ni watu wa kwanza kuelezewa mateso na ufufuo na Yesu mwenyewe; walikuwa mashuhuda wa kwanza wa ufufuo.

**(2) Nini?**

Nini kinatokea katika andiko? Endapo ni andiko la kihistoria, ni matukio gani yametokea? Endapo ni waraka, mwandishi anajaibu kufundisha nini?

Katika Luka 24, tukio lilikuwa ni kufunuliwa kwa Yesu. Macho ya watu hawa wawili yalifunuliwa kuona uhalisia wa ufufuo wa Yesu (Luka 24:31).

**(3) Lini?**

Kama swali lililopita, muda unatoa muktadha katika kujifunza kwetu. Katika hatua ya Uchunguzi ya kujifunza Biblia, tunaangalia kuhusiana na muda ndani ya andiko lenyewe. Kutoka Luka 24:13, tunajifunza kwamba safari ya kwenda Emau ilikuwa siku ile ile ambayo waligundua kaburi liko tupu.

---

[4] Tamaduni moja Inasema kwamba Luka ndiye aliyekuwa mtu ambaye hakutajwa, ambayo Inatoa maelezo kuhusiana na kiasi cha undani wa habari.

Wanafunzi hawa wawili walikutana na Yesu masaa machache tu baada ya kaburi tupu kugundulika. Hii inatueleza kitu kuhusiana na hisia zao wanapozungumza na kuhojiana (Luka 24:15). Fikiri kuhusiana na hisia zao zilizokuwa juu na chini katika siku tatu zilizopita.

Alhamisi, walijisikia kukata tamaa walipomuona Yesu amekamatwa. Ijumaa, matarajio yao ya ufalme wa kimasihi yalivunjika walipomuona Yesu amekufa. Sasa ni Jumapili, na kaburi liko tupu. Wakiwa wanasafiri kwenda Emau, walikuwa wanajaribu kuelewa uajabu wa mfululizo wa matukio.

**(4) Wapi?**

Inasaidia kuuliza, "haya yalitokea wapi?" Atlasi ya Biblia inakusaidia kutafuta majibu ya swali hili. Baadhi ya Biblia zina ramani nyuma yake.

Katika Luka 24, Cleopa na mwenzake ambaye hajatajwa kwa jina wamesafiri kutoka Yerusalemu kwenda Emau, kijiji kilichokuwa kilometa 11 magharibi kwa mji. Walipokuwa wamemaliza kutembea umbali huu, tayari ilikuwa jioni. Lakini baada ya macho yako kufumbuliwa, watu hawa walirudi Yerusalemu kwa furaha. Habari hizi zisingeweza kungoja hadi siku inayofuata!

**(5) Kwa nini?**

Tunaona kwa nini wanafunzi hawa walikuwa wamevunjika moyo tulipokuwa tunajibu swali la muda. Walikuwa wamevunjika moyo kwa sabau matumaini yao yote kuhusiana na Masihi yalipotea Yesu alipokufa.

**(6) Kwa namna gani?**

Ni kwa nana gani maisha ya wanafunzi hawa yalibadilika baada ya kukutana (na Yesu)? Walirejea Yerusalemu kwa ujasiri kwamba Yesu amefufuka kutoka kwa wafu. Kama watu mamilioni baada ya hapo, maisha yao wamebadilika milele baada ya ufufuo.

**Soma kifungu cha andiko au kitabu hicho mara nyingi**

G. Campbell Morgan alikuwa mmoja wa wahubiri wakubwa sana wa karne ya 20. Morgan hakuwahi kuhudhuria chuo cha Biblia, lakini alikuwa mwalimu mwenye ufanisi wa Biblia. Kabla hajahubiri andiko, Morgan alisoma kitabu chote kilichokuwa na andiko alilolichagua angalau mara 40. Kupitia mchakato huu, Morgan alijifunza ni kwa namna gani kila mstari unakaa vizuri katika kitabu chote. Alijua dhana muhimu katika kitabu; aliuelewa ujumbe wa mwandishi. Kuna wakati Morgan alisema, "Kamwe Biblia haijiachi kwa mvivu." Kujifunza Biblia ni kazi inayohitaji bidii.

Unaweza kujiuliza, "Ni kwa namna gani naweza kukisoma kitabu mara 40? Sitamaliza Biblia." Inaweza kuwa sio ngumu kama unavyofikiria. Watu wazima wengi husoma maneno 200 kwa dakika moja; wanaweza kusoma maneno 12,000 kwa saa moja. Vitabu 44 vya Biblia vina chini ya maneno 12,000. Hii inajumuisha nyaraka za Paulo, nyaraka za watu wote, manabii wadogo, na vitabu vya Agano la Kale vya Ruthu, Ezra, Nehemia, Esta, na

Danieli. Kwa saa moja kila siku, unaweza kusoma kitabu cha Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, na Wathesalonike wa 1 na 2 mara 40 katika siku 40.

Kusoma kitabu chote kunaonesha namna kitabu kilivyopangwa. Hapo kabla tulisoma Matendo ya Mitume 1:8 ambapo wanafunzi walitumwa kuwa mashahidi Yerusalemu, Yudea, Samaria, na hata mwisho wa dunia. Unaposoma Matendo ya Mitume mara kwa mara, hii Inatoa kielelezo kwa ajili ya kitabu chote. Katika sehemu ya mwanzo ya Matendo ya Mitume, mateso yaliwachukua wanafunzi kutoka Yerusalemu hadi sehemu nyingine za Yudea; katika Matendo ya Mitume 8, Filipo anachukua Injili hadi Samaria; hadi mwisho wa Matendo ya Mitume, Paulo anahubiri Rumi, kutoka hapo Injili itakwenda hadi mwisho wa ulimwengu uliokuwa unajulikana.

***Baadhi ya Dondoo za Kusoma kwa Kurudia Rudia.***

1. **Soma Biblia kwa sauti au sikiliza ikiwa inasomwa.** Watu wanaoishi katika utamaduni wanaotegemea sana maandishi wanasahahu kwamba wakristo wengi wa kwanza *walisikia* Biblia ikisomwa. Kanisa la Efeso lilipopokea waraka wa Paulo, hawakutoa nakala kwa kila mwamini! Kiongozi angesoma waraka huo kwa waamini. Kupitia historia, watu wengi walipokea neno la Mungu kwa kusikia kuliko kusoma. Nyaraka za Paulo zilisomwa kanisani; manabii walizungumza jumbe zao. Kwa kusoma waraka kwa sauti au kwa kusikiliza kitabu kilichorekodiwa kwa sauti, utalisikia neno la Mungu likizungumzwa kama vile kanisa la kwanza walivyosikia maandiko.[5]

2. **Soma Biblia katika tafsiri tofauti tofauti (Endapo kuna tafsiri Zaidi ya moja katika lugha yako)**. Baadhi ya tafsiri ni ngumu katika njia iliyotumika; nyingine zimelenga katika uelewa kwa urahisi. Kwa kusoma zaidi ya tafsiri moja, utapata uelewa zaidi wa ujumbe. Kama unafahamu zaidi ya lugha moja, inaweza kuwa ya msaada endapo utasoma maandiko katika lugha ya pili.[6]

3. **Kila wakati unaposoma kuwa makini na vitu tofauti tofauti.** Kwa mfano, mtu anaweza kusoma Mwanzo 3 mara moja kila siku kwa juma moja, kuiangalia habari katika mtazamo tofauti tofauti kila wakati:

   Jumatatu: Soma Mwanzo 3 katika mtazamo wa Baba wa mbinguni. Baba anajisikiaje anapoona dhambi ya watoto wake?

   Jumanne: Mstari muhimu katika sura hii ni upi?

   Jumatano: Soma Mwanzo 3 katika mtazamo wa Shetani. Ni kwa namna gani anajaribu kuharibu mahusiano ya Mungu na watoto wake?

   Alhamisi: Soma Mwanzo 3 ukiwa unaiangalia sadaka ya Yesu msalabani.

[5] www.faithcomesbyhearing.com ina Biblia za sauti katika lugha zaidi ya 700.
[6] www.biblegateway.com inakupa wewe kupata tafsiri za Biblia katika lugha nyingi.

Ijumaa: Soma Mwanzo 3 katika mtazamo wa Adamu na Eva. Walijisikiaje walipokuwa wanapokea hukumu ya Mungu?

Jumamosi: Soma Mwanzo 3 katika mtazamo wa mtu ambaye anasoma Biblia kwa mara ya kwanza. Ni kwa namna gani habari hii ni muhimu ili kuelewa sehemu nyingine yote ya Biblia?

Machaguzi ya mpango yanapatikana katika www.bible.com ili kukusaidia wewe kusoma Biblia mwaka mzima. Mpango mwingine, unajikita katika Muundo wa G. Campbell Morgan, ni wa kusoma kitabu kimoja mara kadhaa katika mwezi mmoja. Kwa sababu vitabu 44 vya Biblia vinaweza kusomwa chini ya saa moja au ndani saa moja kila siku, unaweza kusoma kitabu chote mara 30 katika mwezi kwa saa moja kila siku. Wakati mchakato huu unaweza kuonekana ni wa polepole, kurudia rudia kusoma kitabu kutakupa uelewa wa Neno la Mungu. Kusoma kwa namna hii, unaweza kusoma Biblia yote mara 30 ndani ya miaka sita.[7]

## Jifunze Sarufi

Mungu anawasiliana na sisi kwa njia nyingi, kuu ni kupitia neno lilioandikwa. Ni kweli hauhitaji kuwa mwana lugha ili kuelewa maandiko, lakini kwa kadiri unavyoelewa lugha iliyoandikwa, ndivyo utakavyopata ukweli wa Neno la Mungu kwa usahihi.

Kama mfano, tutajifunza sarufi ya moja kati ya mistari wa Paulo inayojulikana sana. "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana" (Warumi 12:1). Katika kuchunguza sarufi ya andiko, tunaangalia:

### *Vitenzi*

Vitenzi vinawasilisha kitendo au hali ya kuwa. Kuna vitenzi viwili vinavyoonesha matendo katika Warumi 12:1:

- **Nawasihi** inamaanisha "kuomba" au hata "kusihi." Je, unaona uharaka wa ombi la Paulo? Hili si pendekezo la kawaida; kuna hisia nzito wakati Paulo anawasihi wasomaji wake wajitoe kikamilifu kwa Mungu.
- **Itoeni** ni kitenzi kinachoonesha tendo. Inahitaji kuweka ahadi. Paulo anawataka wasomaji wake waitoe miili yao, wajitoe wao wenyewe kwa Mungu.

### *Majina*

Katika Warumi 12:1, majina ambayo ni muhimu katika kujifunza kwetu yanajumuisha:

- **Ndugu.** Pauo anawaandikia waamini. Hawaiti wenye dhambi kubadilika; anawaita waamini katika kujitoa kikamilifu.

[7] Vitabu virefu vitawekewa usawa na vitabu vifupi kama Filemoni na Tito kwamba vinaweza kusomwa mara thelasini ndani ya siku chache.

- **Miili.** Sehemu iliyobaki ya Warumi 12 inaonesha kwamba *miili* inawakilisha utu wetu kwa ujumla. Tunaweza tukalisema kwa namna nyingine kama hivi, "Jitoe utu wako wote."

- **Huruma.** Wito wa Paulo unamsingi katika huruma za Mungu. Katika kifungu kilichotangulia kabla ya mstari huu, Paulo amekuwa anauelezea wema wa Mungu unaoneshwa kwa watu, wote wawili Wayahudi na Wamataifa (Warumi 11:32).

- **Dhabihu.** Chini ya sheria ya Musa, anayeabudu alileta mnyama kama sadaka. Katika Ufalme wa Kristo, tunaitwa kujitoa wenyewe kama sadaka inayoshi.

***Vivumishi***

Vivumishi na vielezi ni maneno ya ufafanuzi ambayo "hukuza maana ya maneno wanayoyavumisha na kuyaelezea."[8] Katika Warumi 12:1, *dhabihu* inaelezewa kwa mfululizo wa maneno.

- Dhabihu yetu ni **hai**. Hatutoi tena dhabihu mnyama aliyekufa; tunatoa maisha yetu kwa kujisalimisha kila siku.

- Sadaka zetu lazima ziwe **takatifu**. Mwabudu wa Agano la Kale asingeweza kuleta sadaka ambayo ni kilema au hata isiyofaa; mwamini wa Agano Jipya hawezi kuleta sadaka ya maisha machafu, yasiyo na utii kama dhabihu.

- Ni dhabihu iliyokamilika tu na iliyo tayari ndiyo **ya kumpendeza Mungu**.

***Vishazi Vihusishi***

Vihusishi ni maneno kama vile ndani, juu, kupitia, ndani ya, na kwa. Maneno haya madogo yanabeba maana kubwa. Katika Warumi 12:1, vishazi vihusishi viwili ni muhimu:

- "Kwa huruma zake Mungu" Inatoa msingi wa kusihi kwa Paulo. Hapa si kama mwanajeshi anamlazimisha adui kujisalimisha; badala yake, ni mtoto kujisalimisha kwa furaha kwenye mapenzi ya baba yake anayependa.

- Dhabihi zetu ni lazima ziwe za kukubalika "kwa Mungu." Kwa mkristo, kukubalika na Mungu ni zawadi kuu sana.

***Maneno Yanayounganisha***

Maneno yanayounganisha *na* au *lakini* yana nguvu sana. Mwandishi mmoja analinganisha maneno yanayounganisha na udongo wa kujengea unaounganisha matofali pamoja.[9] Katika Matendo ya Mitume 1:8, tuliona kwamba *lakini* inarejelea nyuma katika kutoelewa kwa mitume.

---

[8] Howard G. Hendricks na William D. Hendricks, *Living by the Book* (Chicago: Moody Publishers, 2007), 121

[9] J. Scott Duvall na J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012), 59

Katika Warumi 12:1, *Basi* inarejelea nyuma katika kifungu kilichopita. Endapo utasoma kitabu chote cha Warumi, kwa haraka utaona kuna migawanyo mikubwa miwili:

- Warumi 1-11 inafundisha mafundisho: hukumu ya dhambi, kuhesabiwa haki kwa imani, utakaso wa mwamini, kutukuzwa kama lengo kuu la Mungu kwa watoto wake, na kuchaguliwa kama njia ya Mungu kutimiliza kusudi hili.
- Warumi 12-16 inaonesha matumizi ya kivitendo ya mafundisho haya. Kwa sababu tumekuwa sawa na Mungu, tunatakiwa kuishi kwa namna hii. Kwa sababu ya kile tunachokiamini (Warumi 1-11), hivi ndivyo tunatakiwa kufanya (Warumi 12-16). Mstari unaounganisha ni Warumi 12:1.

*Basi* ni kiashiria muhimu cha alama katika nyaraka nyingi za Paulo. Baada ya kuwakumbusha waamini wa Galatia kuhusiana na kweli kuhusu kuhesabiwa haki kwa imani pekee, Paulo anawaita kuiishi haki yao katika maisha yao ya kila siku; "Katika ungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni" (Wagalatia 5:1). Baada ya kuwafundisha Waefeso kweli mkuu ya mafundisho ya kuchaguliwa kwao katika Kristo Yesu, Paulo anawaita wao kuishi maisha yanayostahili wito wao; "Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa" (Waefeso 4:1). Paulo aliwaambia Wakolosai kwamba wao walikuwa wamekufa na maisha yao yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Ni kwa namna gani wao wanatakiwa kuishi kama matokeo? "Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi" (Wakolosai 3:5).

### Tafuta Taarifa Maalumu Katika Andiko[10]

Kutambua stadi ambazo waandishi wa Biblia wanazitumia kuonesha wazo kuu katika andiko kunaweza kuleta uelewa mpya katika kujifunza kwako. Taarifa za kina za kuziangalia ni pamoja na:

#### *Maneno Yaliyorudiwa Rudiwa*

Mwandishi anaporudia maneno mara kwa mara, inaonesha wazo muhimu. Katika hatua ya uchunguzi, hautaweza kwenda kwa kina sana kutafuta maana za maneno yaliyorudiwa rudiwa, lakini unaweza kuliwekea alama neno na kujiuliza, "Kwa nini neno hili limerudiwa rudiwa?"

► Soma vifungu vifuatavyo na wekea alama maneno yaliyorudiwa rudiwa:

> **2 Wakorintho 1:3-7**. Ni mara ngapi neno *faraja* limerudiwa katika kifungu hiki? Mifano ya maswali ambayo unaweza kuyauliza wakati unapogundua kurudiwa rudiwa katika kifungu:
>
> - Je, neno *faraja* limetumika kwa namna ile ile kila wakati?
> - Ni vielezi vipi vimetumika? (faraja *yote*; faraja *yetu*; faraja *yenu*.)

---

[10] Hii imechukuliwa kutoka kwa J. Scott Duvall na J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012).

**Yohana 15:1-10.** Ni mara ngapi neno *kaeni* nimerudiwa katika kifungu hiki? Mifano ya maswali ambayo unaweza kuyauliza wakati unapogundua kurudiwa rudiwa katika kifungu:

- Ni masharti gani ya kukaa ndani yake?
- Je, maonyo katika kifungu hiki yanaonesha kwamba inawezekana kwa mtu kutokaa ndani yake?
- Ni nini matokeo ya kutokaa ndani yake?
- Ni nini Baraka za kukaa nadani yake?

### *Ukinzani*

Waandihi wengi wa Biblia walikinzanisha watu na mawazo. Unaliona neno *lakini* katikati ya mstari, linaweza kuwa linaunganisha mawazo mawili tofauti. Mithali nyingi zinatumia aina hii ya ukinzani.

- Kuna namna mbili za kukabiliana na ukosoaji: "Jawabu la upole hugeuza hasira; Bali neno liumizalo huchochea ghadhabu" (Mithali 15:1).
- Kuna namna mbili za kufanya maamuzi muhimu: "Pasipo mashauri taifa huanguka; Bali kwa wingi wa washauri huja wokovu" (Mithali 11:14).
- Namna tunavyowatendea masikini inaonesha mitazamo yetu kuhusiana na Mungu: "Amwoneaye maskini humsuta Muumba wake; Bali yeye awahurumiaye wahitaji humheshimu" (Mithali 14:31).

Waandishi wa Agano Jipya pia wanatoa ukinzani. Paulo alitoa tofauti kati ya maisha yetu ya kale (giza) na maisha yetu mapya (nuru); "Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana…" (Waefeso 5:8).

Katika 1 Yohana 1:5-7, Yohana anatofautisha kati ya giza na nuru katika namna mbili:

- Mungu ni Nuru na hamna giza ndani yake.
- Endapo tunaushirika na Mungu, tutatembea nuruni, na si gizani.

### *Ulinganifu*

Ukinzani unaangazia tofauti; ulinganifu unaangazia mfanano.

- "Kama siki menoni, na kama moshi machoni, Ndivyo alivyo mtu mvivu kwao wamtumao" (Mithali 10:26).
- "Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana" (Mithali 25:25).

► Soma Yakobo 3:3-6. Ulimi unalinganishwa na mambo gani matatu? Unajifunza nini kutokana na ulinganifu huu?

► Kila mstari wa Mithali 26:8-11 unajumuisha neno *kama.* Kwa kila mstari, jifunze ulinganifu. Kwa mfano, kama unaangalia Mithali 26:8, unaweza ukajiambia mwenyewe: "Kama mfuko wa vito katika chungu ya mawe kadhalika mtu amheshimuye mpumbavu **kwa sababu**…." Ni mfanano gani unaouona katika ya mithali iliyozungumzwa na kumuheshimu mpumbavui?

### *Orodha*

Unaposoma Biblia, unatakiwa kuonesha orodha na kujifunza hizo kwa ajili ya sifa muhimu.

► Kabla ya kuendelea na somo, chukua muda kusoma orodha ifuatayo:

- Katika 1 Wakorintho 3:6, Paulo anaonesha kazi za huduma yake huko Korintho.
- 1 Yohana 2:16 inaorodhesha mambo ambayo yanatokea katika ulimwengu na si yanayotoka kwa Baba.
- Wagalatia 5:19-21 inaorodhesha matendo ya mwili.
- Wagalatia 5:22-23 inaorodhesha tunda la Roho Mtakatifu.

### *Tamko la Kusudi*

Maneno kama *kwamba, ili kwamba* au *kwa* mara nyingi yanaelezea msukumo kwa ajili ya tendo au matokeo ya; kitendo. Chukua muda kufikiri mahusiano kati ya makusudi na matokeo; uliza ni kwa nini maandiko yanatupa maelekezo.

- "Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka," (kwa nini?) "mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa" (Yohana 15:16).
- "Moyoni mwangu nimeliweka neno lako," (kwa nini?) "Nisije nikakutenda dhambi" (Zaburi 119:11).
- "kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu" (kwa nini Mungu alituchagua sisi?), "ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake" (Waefeso 1:4).

Wakati mwingine, tamko linaonesha ni kwa namna gani kusudi linatimizwa:

- "Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno lako" (Zaburi 119:9).
- Ni kwa namna gani tunaweza kupata uhakika wa maisha? "kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi" (Warumi 8:13).

### *Vishazi Masharti*

Vishazi vinavyoanza na *kama* vinatoa sharti. Wakati mwingine msomaji wa Biblia anatarajia ahadi zitimilizwe pasipo kutimiza masharti; hata hivyo, ahadi yenye sharti inategemea kutimilizwa kwa masharti mahususi. Hii inaonekana mara kwa mara kupitia vishazi masharti.

> **Sharti**: "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo,"
> **Matokeo**: "amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17).
>
> **Sharti**: "Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu,"
> **Matokeo**: "nitalifanya" (Yohana 14:14).

### Omba Unaposoma

Maelekezo haya ya mwisho yanaonekana ya kawaida, lakini ni muhimu. Mkristo kujifunza Biblia na maisha ya maombi hayatakiwi kutenganishwa. Kutenganisha kusoma Biblia na maombi ni kutenganisha nyanja mbili za maisha yetu ya kila siku ya mawasiliano na Mungu.

Yakobo anatuhakikishia sisi kwamba tunaweza kuomba msaada wa Mungu tunapopungukiwa hekima; "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa" (Yakobo 1:5). Hii ni ahadi ya ajabu sana tunapohitaji msaada wa Mungu ili kulielewa neno la Mungu.


Zaburi 119 inaonesha daraja au muunganiko kati ya maombi na andiko. Mzaburi anarudia rudia kumuomba Mungu kuongoza kujifunza kwake neno la Mungu. Katika namna hiyo hiyo, tunaweza kutafuta usaidizi wa Mungu tunapojifunza.

- "Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika sheria yako" (Zaburi 119:18).
- "Unifahamishe njia ya mausia yako" (Zaburi 119:27).
- "Ee BWANA, unifundishe njia ya amri zako" (Zaburi 119:33).

Watu wengi wamejifunza nguvu ya kugeuza maneno ya maandiko na kuwa maombi. Jaribu kugeuza vifungu hivi ili kuwa maombi binafsi:

- Zaburi 23 – ombi kwa ajili ya uongozi wa Kimungu na ulinzi
- Isaya 40:28-31 – ombi kwa ajili ya nguvu za Kimungu
- Wafilipi 4:8-9 – ombi kwa ajili ya akili njema ya kimungu

**Mfano: Uchunguzi wa 1 Yohana 1:5-7**



**1 Yohana 1:5-7**

Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lolote hamna ndani yake.

Tukisema kwamba tunashirikiana naye, huku tukienenda katika giza, tunasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli.

Bali tukienenda katika nuru, kama yeye alivyo katika nuru, tunashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake yatusafisha Dhambi yote.

## Somo la 2 Dondoo Muhimu

(1) Anza mchakato wa Uchunguzi kwa kujifunza mstari mmoja. Jiulize maswali mengi kwa kadiri unavyoweza kuhusiana na mstari.

(2) Hatua za kukuza nguvu zako za uchunguzi zinajumuisha:

- Soma ili kupata uelewa.
- Uliza maswali unaposoma.
    - Nani?
    - Nini?
    - Lini?
    - Wapi?
    - Kwa nini?
    - Kwa namna gani?
- Soma kifungu cha andiko au kitabu hicho mara nyingi.
- Jifunze sarufi. Angalia:
    - Vitenzi
    - Majina
    - Vivumishi
    - Vishazi Vihusishi
    - Maneno Yanayounganisha
- Tafuta Taarifa Maalumu katika Andiko. Angalia:
    - Maneno yaliyorudiwa rudiwa
    - Ukinzani
    - Ulinganifu
    - Orodha
    - Tamko la kusudi
    - Vishazi Masharti
- Omba unaposoma.

## Somo la 2 Mazoezi

(1) Tengeneza orodha ya uchunguzi wa Yoshua 1:8. Andika mstari katika karatasi na kisha uanze kujiuliza maswali: "Nani? Nini? Lini? Wapi? Kwa nini? Kwa namna gani?" Kwa kutumia mfano uliopewa katika sehemu ya mwisho na mwongozo katika somo hili, fanya uchunguzi mwingi wa kina kwa kadiri utakavyoweza. Katika hatua hii, hautafsiri mstari au hauandai muhtasari wa ujumbe. Unaangalia tu taarifa za kina katika mstari.

(2) Kwa mazoezi zaidi, fuata mchakato ule ule kwa Mathayo 28:18-20.

# Somo la 3
# Uchunguzi: Kuangalia Sehemu Kubwa

## Malengo ya Somo

(1) Kutambua umuhimu wa muktadha wakati wa kusoma Maandiko.

(2) Kuwa makini sana na kusudi na nia ya waandishi wa Biblia kwa kuchunguza taarifa za kina ambazo zinasisitizwa katika kitabu.

(3) Kutendea kazi Uchunguzi wa sehemu kubwa ya Maandiko.

(4) Kukusanya taarifa katika jedwali kwa ajili ya kujifunza zaidi.

## Utangulizi

Baadhi ya usomaji si wa muhimu; tunasoma riwaya ili kupitisha muda wakati tunasafiri. Baadhi ya usomaji una umuhimu mdogo; tunasoma maganeti ili kufahamu yanayoendelea katika ulimwengu wetu. Baadi ya usomaji una umuhimu wa milele; tunasoma Maandiko ili kusikia sauti ya Mungu. Paulo aliandika kwamba kila andiko lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki (2 Timotheo 3:16-17). Kwa sababu hii, tunasoma Biblia kwa umakini, ili kumsikia Mungu akisema.

Katika somo la 2, tulifanya uchunguzi kuhusiana na mstari husika. Katika somo hili, tutaviangalia vifungu kikubwa. Hivi vinaweza kuwa kifungu cha andiko, sura, au hata kitabu chote. Katika simulizi za kihistoria, kifungu kikubwa kinaweza kuwa ni habari yote. Katika injili, tunaweza kujifunza mfano, muujiza, au mahubiri. Kifungu kikubwa kinaweza kuwa ni sehemu kuwa ambayo inajikita katika wazo au dhana moja.

Kwa asili, Biblia ilikuwa haijagawanywa katika sura na mistari. Katika karne ya 13, Stephen Langton aligawanya Biblia katika sura ili iwe rahisi kujifunza. Katika karne ya 16, Robert Estienne alichapisha Biblia ilkiwa imegawanywa katika mistari. Mgawanyo wa sura na mistari inatusaidia sisi kujifunza Biblia; hata hivyo, wakati mwingi mgawanyo haukubaliani na mgawanyo wa asili wa andiko. Usiruhusu mgawanyo wa sura kudhibiti kujifunza kwako; fuata mgawanyo wa asili wa andiko na mtiririko wa wazo katika kifungu cha maneno.

Katika somo hili, tutajifunza kifungu cha andiko, Nehemia 1:4-11. Hiki kitakuwa kielelezo kwa ajili ya kujifunza kwako hapo baadae. Tutajifunza njia kadhaa za kujifunza kifungu. Tambua kwamba si kila aina ya ujifunzaji itafanya kazi katika kila kitabu. Somo hili litakupa sanduku za zana au vifaa vya kutumia. Unapojifunza kitabu cha Biblia, utahitaji kuamua, “ni zana gani ni sahihi kwa kitabu hiki?”

## Kutafuta Muktadha wa Kifungu cha Maandiko

Nehemia 1:4-11:

> Hata ikawa niliposikia maneno hayo, nikaketi, nikalia, nikaomboleza siku kadha wa kadha; kisha nikafunga, nikaomba mbele za Mungu wa mbinguni.
>
> nikasema, Nakusihi, Ee BWANA, Mungu wa mbinguni, Mungu mkuu, mwenye kuogofya, mwenye kutimiza agano lake na rehema zake kwa hao wampendao na kuzishika amri zake; tega sikio lako, macho yako yakafumbuke, upate kuyasikiliza maombi ya mtumishi wako, ninayoomba mbele zako wakati huu, mchana na usiku, kwa ajili ya wana wa Israeli, watumishi wako; hapo ninapoziungama dhambi za wana wa Israeli, tulizozifanya juu yako; naam, mimi na nyumba ya baba yangu tumefanya dhambi. Tumetenda maovu mengi juu yako, wala hatukuzishika amri, wala sheria, wala hukumu, ulizomwamuru Musa, mtumishi wako.
>
> Nakuomba, likumbuke neno lile ulilomwamuru Musa, mtumishi wako, ukisema, Mkikosa, nitawatawanya kati ya mataifa; bali mkinirudia mimi, na kuzishika amri zangu na kuzitenda, watu wako waliofukuzwa wajapokuwa katika pande za mwisho za mbingu, hata hivyo nitawakusanya kutoka huko, na kuwaleta mpaka mahali pale nilipopachagua ili kuliweka jina langu hapo.
>
> Basi watu hao ni watumishi wako na watu wako, uliowakomboa kwa uweza wako mwingi, na kwa mkono wako hodari. Ee Bwana, nakusihi, litege sikio lako, uyasikilize maombi ya mtumishi wako, na maombi ya watumishi wako, wanaofurahi kulicha jina lako; nakuomba sana; unifanikishe mimi, mtumishi wako, leo, ukanijalie rehema mbele ya mtu huyu.
>
> Maana, nalikuwa mnyweshaji wa mfalme.

Tunapojifunza Kifungu cha andiko, tunahitaji kuutambua muktadha ambao kifungu cha andiko kinapatikana. Nehemia 1:4 inarejelea mwanzoni mwa sura

> Hata ikawa niliposikia maneno hayo....

“maneno hayo” yanatuhitaji sisi turudi katika mistari ya nyuma ili kutafuta ni **maneno gani** ambayo Nehemia aliyasikia yaliyosababisha mwitikio wake.

Nehemia 1:1 inatoa muktadha wa kitabu cha Nehemia:

> Habari za Nehemia, mwana wa Hakalia. Ikawa katika mwezi wa Kisleu, mwaka wa ishirini, nilipokuwapo Shushani ngomeni.

Somo la 2 lilitupa maswali ya kuuliza tunapojifunza mstari.

**Nani?** “Nehemia, mwana wa Hakalia.” Kuna Nehemia mwingine aliyetajwa baadae katika kitabu hiki (Nehemia 3:16). Jina la familia (“mwana wa Hakalia”) linaonesha ni Nehemia yupi anayerejelewa hapa.

**Lini?** "…katika mwezi wa Kisleu, mwaka wa ishirini." Kutoka katika Kamusi ya Biblia, tunajifunza kwamba mwezi wa Kiebrania wa Kislev ni sawa na mwezi Novemba kwenda wa Desemba.[11] "katika...mwaka wa ishirini" haituelezi kwa uwazi kwa sababu hatujui kama mwandishi alirejelea mwaka wa ishirini wa Maisha ya Nehemia, mwaka wa ishirini wa matukio ya kihistoria, au rejea nyinginezo. Katika wakati huu, tunaweza kuwekea alama ya kuuliza pembezoni mwa kifungu hiki. Katika Nehemia 2, tunajifunza jibu; "mwaka wa ishirini wa mfalme Artashasta." Nehemia alianza Novemba/Desemba mwa mwaka wa ishirini wa utawala wa mfalme Artashasta.

**Wapi?** Nehemia alikuwa "Shushani ngomeni." Kutoka katika atlasi au kamusi ya Biblia, tunajifunza kwamba kulikuwa na ikulu mbili katika Uajemi. Ikulu ya wakati wa kiangazi ilikuwa Ek-batana. Ikulu ya masika ilikuwa ya kifahari na ilikuwa Shushani Ngomeni. Kitabu kinaanza wakati Nehemia alikuwa na mfalme Artashasta katika ikulu yake ya wakati wa masika huko Shushani Ngomeni.

Endapo unajifunza neno katika kompyuta yako, inaweza kuwa ya msaada sana endapo kompyuta yako itakitengeneza kwa mtindo mwingine kifungu cha andiko ili kuonesha mahusiano kati ya vishazi hivi. Kifungu cha andiko cha (Nehemia 1:1) kitaonekana kama hivi;

> Habari za Nehemia, mwana wa Hakalia. Ikawa
> katika mwezi wa Kisleu,
> mwaka wa ishirini,
> nilipokuwapo Shushani ngomeni...

Mstari wa 1 unatoa mazingira ya kitabu cha Nehemia. Mistari ya 2 na 3 zinaonesha mazingira kwa ajili ya maombi ya Nehemia. Akiwa Shushani Ngomeni, "Hanani, mmoja wa ndugu zangu, akanijia, yeye na watu wengine waliotoka Yuda." Nehemia aliulizia habari ya mambo mawili.

> Nami nikawauliza
> habari za Wayahudi waliopona, hao watu wa uhamisho waliosalia; na habari za Yerusalemu.

Katika mwitikio, watu kutoka Yuda waliripoti matatizo mawili:

- "Watu wa uhamisho, waliosalia huko katika wilaya ile, wamo katika hali ya dhiki nyingi na mashutumu."
- "Tena ukuta wa Yerusalemu umebomolewa, na malango yake yameteketezwa kwa moto."

---

[11] *International Standard Bible Encyclopedia*, 'Kislev', ilitafutwa October 6, 2023, https://www.studylight.org/encyclopedias/eng/isb/k/kislev.html.

Hii inaonesha matatizo ambayo yalimsukuma maombi ya Nehemia. Baada ya kujifunza muktadha, tupo tayari kufanya uchunguzi kuhusiana na maombi yenyewe.

## Nini cha Kuangalia Unapojifunza Kifungu

Uchunguzi wako katika kifungu utategemea mtindo wa kifungu. Simulizi ya kihistoria itajumuisha maswali ya *nani*, *nini*, *lini*, na *wapi*. Kifungu cha mafundisho kitajumuisha maswali yanayohusiana na mafundisho.[12]

Nehemia 1:5-11 ni maombi. Maombi yake yanajumuisha:

- **Sifa** kwa Mungu "Mungu mkuu, mwenye kuogofya, mwenye kutimiza agano lake."
- **Toba** kwa ajili ya "dhambi za wana wa Israeli, tulizozifanya juu yako."
- **Maombi** kwa msingi wa ahadi za Mungu "mkinirudia mimi…nitawakusanya kutoka huko, na kuwaleta mpaka mahali pale nilipopachagua ili kuliweka jina langu hapo."

Katika hatua hii ni muhimu kuwa makini na taarifa ambazo si za kawaida. Maombi ya Nehemia yanafuatiwa na taarifa ya wasifu: "Maana, nalikuwa mnyweshaji wa mfalme." Hii kwa mara ya kwanza inaonekana si muhimu, lakini taarifa hii inakuwa ya muhimu kwa kadiri habari inavyosimuliwa.

Kama tukisoma neno *mnyweshaji* katika kamusi ya Biblia,[13] tunajifunza kwamba mnyweshaji alikuwa ni zaidi ya mtumishi wa kawaida; alikuwa ni afisa wa juu na kwa ujasiri aliaminiwa na mfalme.[14]

Taarifa gani tunaweza kuzichunguza katika kifungu? Angalia:

### Mahusiano ya Jumla kwenda Mahususi

Vifungu vingi vinaanza na mtazamo wa jumla ambao baadae unaendelezwa kwa kutumia taarifa mahususi. Taarifa hizi zinaunga mkono tamko la jumla kwa maelezo zaidi.

Mahusiano ya jumla kwenda mahususi ni ya kawaida katika nyaraka za Paulo. Wagalatia 5:16 inatoa ukinzani wa maisha katika Roho na maisha katika mwili; "Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili." Tamko hili la jumla baadae linaumgwa mkono na mfuflulizo wa mambo mahususi. Wagalatia 5:19-21 inatambulisha matendo ya mwili; Wagalatia 5:22-23 inatambulisha tunda la Roho.

Baadhi ya simulizi zinafuata kielelezo cha jumla kwenda mahususi. Mwanzo 1 na 2 inafuata kielelzo hiki, kutembea toka tamko la jumla kwenda kwenye taarifa mahususi. Hii inakuja katika hatua tatu:

---

[12] Nyenzo nyingi katika sehemu hii yamechukuliwa kutoka katika Sura ya 4 ya kitabu cha J. Scott Duvall and J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012).
[13] *Holman Bible Dictionary*, 'Cupbearer', ilitafutwa October 6, 2023, https://www.studylight.org/dictionaries/eng/hbd/c/cupbearer.html.
[14] J. D. Douglas, *New Bible Dictionary*, (2nd edition), (Wheaton: Tyndale House, 1982)

1. Mwanzo 1:1 inatoa tamko la jumla: "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi."
2. Mwanzo 1:3-31 inatoa taarifa za kina kuhusiana na uumbaji. Siku ya kwanza, Mungu aliumba Nuru, siku ya pili Mungu alitenganisha maji na anga; na kuendelea.
3. Mwanzo 2 ni mahususi zaidi. Msimuliaji anatembea kutoka uumbaji wa jumla wa ulimwengu kwenda uumbaji mahususi wa mwanadamu. Habari inajikita kutoka ulimwengu wote na kwenda mahali mahususi, bustani ya Edeni. Hata jina la Mungu limebadilika. Mwanzo 1 inatumia jina *Mungu*, jina la jumla la nguvu. Mwanzo *BWANA MUNGU*, jina la kibinafsi kuonesha mahusiano yake ya ndani na Adamu na Eva.[15]

Mara nyingi kielelezo kinaenda kutoka jumla kwenda mahususi. Wakati mwingine hubadilika, kutoka mahususi kwenda jumla. Katika 1 Wakorintho 13, Paulo anatoa mambo mahususi kuhusiana na upendo katika mstari wa 1-12. Sura inamalizika kwa Paulo kutoa tamko la jumla ambalo linafupisha fundisho la Paulo: "Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo."

### Sehemu za swali na jibu

Kifungu kinapoanza na swali, swali linaonesha umuhimu wa sehemu iliyobaki ya kifungu. Mfumo huu ni wa kawaida katika kitabu cha Warumi. Kwa wanaofundisha kwamba neema inaruhusu maisha ya dhambi, Paulo anauliza, "Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?" (Warumi 6:1). Kisha anaonesha kwamba neema ya Mungu inampa nguvu mkristo ya kushinda dhambi, "Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?" (Warumi 6:2).

Injili ya Marko mara kwa mara imetumia muundo huu. Katika Marko 2:1–3:6, matukio matano yameanza na mswali. Mara nne, wapinzani wameuliza swali. Kila wakati, Yesu alijibu kwa utetezi. Katika tukio la mwisho, Yesu anauliza swali ambalo mafarisayo walishindwa kulijibu. Kuwa makini namna ambavyo hii inatoa muundo wa sehemu kubwa. Pasipo hii, tunasoma habari tano binafsi. Tunapoona muundo unaoundwa na maswali na majibu, habari tano zinatoa ushuhuda kwa mamlaka ya kimasihi ya Mwana wa Adamu.

1. Kumponya mtu aliyepooza (Marko 2:1-12)

   Swali: "Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?"
   Jibu: Yesu anaonesha mamlaka yake kwa kumponya mtu aliyepooza.

2. Kula na wenye dhambi (Marko 2:13-17)

   Swali: "Mbona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?"
   Jibu: "sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."

[15] Jina la Kiebrania *Elohim* linatafsiriwa *Mungu* katika Biblia za Kiswahili; ni jina la jumla, lenye utisho. Jina la Kiebrania *Yahweh* is limetafsiriwa "BWANA" katika Biblia za Kiswahili; ni jina la kibinafsi lililofunuliwa katika in Kutoka 3:14.

3. Kufunga (Marko 2:18-22)

   Swali: “Kwani wanafunzi wa Yohana na wanafunzi wa Mafarisayo hufunga, bali wanafunzi wako hawafungi?”

   Jibu: “Muda wote walipo na bwana-arusi pamoja nao hawawezi kufunga.”

4. Sheria za Sabato (Marko 2:23-28)

   Swali: “mbona wanafanya lisilokuwa halali siku ya sabato?”
   Jibu: “Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato pia.”

5. Uponyaji siku ya Sabato (Marko 3:1-6)

   Swali: “Ni halali siku ya sabato kutenda mema, au kutenda mabaya?”
   Jibu: Wapinzani wa Yesu alibaki kimya.

**Mahojiano**

Injili mara nyingi zinaonesha mahojiano kati ya Yesu na wale wanaomzunguka. Tunaweza kupata uelewa zaidi wa mafundisho ya Yesu kwa kuuliza maswali kama:

- Washiriki ni kina nani katika mahojiano?
- Nani walikuwa watazamaji waliokuwa wanasikiliza mazungumzo hayo? Waliitikia kwa namna gani?
- Ni mgogoro gani ambao ulisababisha mahojiano?

Mathayo 21:23–22:46 inaonesha mfululizo wa mahojiano kati ya Yesu na wapinzani wake. Kila kundi liliuliza maswali ili kumnasa Yesu.

- Kwanza, viongozi wa kidini walihoji mamlaka yake (Mathayo 21:23-46).
- Mafarisayo na maherode (mara nyingi walikuwa maadui) waliungana pamoja ili kumnasa Yesu kwa kuuliza maswali kuhusiana na kodi (Mathayo 22:15-22).
- Masadukayo (ambao hawakuamini ufufuo) walimuuliza Yesu swali kuhusiana na ndoa baada ya ufufuo (Mathayo 22:23-32).
- Mafarisayo walijaribu tena kwa swali lingine kuhusiana na amri (Mathayo 22:34-40).
- Mwisho, Yesu anamaliza mgogoro kwa kuuliza swali ambalo hawakuweza kujibu (Mathayo 22:41-46).

Makutano walikuwa wakiangalia wakati makundi yote yalipokuwa yanajaribu kumnasa Yesu, na walikuwa waliangalia wakati Yesu alipowafumba vinywa kila wauliza swali. “Na makutano waliposikia, walishangaa kwa mafunzo yake” (Mathayo 22:33).

Mahojiano ni muhimu katika kitabu cha Ayubu. Kitabu hiki kinajumuisha mazungumzo kati ya Mungu na Shetani, kati ya Ayubu na marafiki zake, na kati ya Ayubu na Mungu.

Kitabu chote cha Habakuki kinajumuisha mahojiano kati ya nabii na Mungu. Kitabu kimeundwa kama hivi:

> **Habakuki anauliza maswali**: Kwa nini Mungu anavumilia dhambi ya Yuda (1:1-4)?
>
> **Mungu anajibu**: Babeli watawashinda Yuda (1:5-11).
>
> **Habakuki anauliza maswali**: Mungu anawezaje kuwatumia Babeli waovu ili kuhukumu Yuda (1:12-2:1)?
>
> **Mungu anajibu**: Habakuki lazima aishi kwa imani katika makusudi ya Mungu (2:2-20).

**Toni ya Kihisia**

Toni ya kihisia inarejelea hisia ambazo mwandishi anaonesha. Maandiko ni zaidi ya habari ya kufikirika; ni hadithi ya uhusiano kati ya Mungu mwenye upendo na watu aliowaumba. Uhusiano huo wa karibu unahusisha hisia. Wasomaji makini huzingatia hisia za mwandishi.

Ili kutafuta toni ya kihisia ya kifungu cha andiko, angalia maneno ambayo yanaonesha hisia (furaha, dharau, maombolezo) au mahusiano (baba, mwana, binti). Sikiliza roho ya mwandishi na ya wapokeaji katika simulizi.

► Soma Wafilipi 1:1-8 ikifuatiwa na Wagalatia 1:1-9. Ni toni gani za hisia zinazoonekana katika kila kifungu? Kutoka katika utangulizi, unaweza kuhitimisha nini kuhusu uhusiano wa Paulo na kanisa la Filipi na makanisa ya Galatia?

## Nini cha kuangalia unaposoma kitabu chote

Tunaposoma kitabu chote, tunaangalia muundo na dhana kuu katika kitabu. Mambo ya kuchunguza katika hatua hii yanajumuisha:

### Mambo Yanayosisitizwa

Tunaweza kupata kile kinachosisitizwa na kitabu kwa kuchunguza:

#### *Kiwango cha Nafasi*

Kiwango cha nafasi ambacho kitabu kinatoa kwa mada mara nyingi kinaonesha nini ni muhimu kwa mwandishi. Katika Mwanzo, watu wanne (Ibrahimu, Isaka, Yakobo, na Yusufu) wamesomwa katika sura ya 12-50. Hii ikilinganishwa na sura 11 tu ambazo zinaelezea habari ya Uumbaji, Anguko, gharika, na mnara wa Babeli. Kuwa makini na taarifa hizi katika hatua ya Uchunguzi kutatuandaa sisi kujiuliza “kwa nini?” katika hatua ya kutafsiri.

Tunaposoma kitabu cha Nehemia, tunagundua kwamba maombi yamechukua nafasi kuu katika kitabu. Katika kila wakati muhimu katika maisha ya Nehemia, aliomba. Kwa kutambua hili, tunaandaliwa kuelewa vizuri tabia ya Nehemia.

### *Kusudi Lililotamkwa*

Katika baadhi ya vitabu, mwandishi anatuambia kusudi la kiandika kwake. Mithali inaanza na tamko refu la kusudi la Sulemani katika kuandika mkusanyiko wake wa hekima (Mithali 1:2-6). Injili ya Yohana inatamka kusudi lake: "ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake" (Yohana 20:31).

### *Mpangilio wa Nyenzo*

Katika simulizi ya kihistoria, mpangilio wa nyenzo unaweza kuonesha kusudi la mwandishi. 2 Samweli 1-10 inaelezea habari ya ushindi wa ufalme wa Daudi. 2 Samweli 11 inarekodi dhambi ya Daudi na Bathsheba. Kutoka hapo, 2 Samweli inafuatilia matatizo yaliyokuja katika ufalme wa Daudi. Mwandishi wa 2 Samweli anaonesha kwamba matatizo ni hukumu ya Mungu kwa dhambi ya Daudi.

Nehemia imegawanywa katika sehemu kuu tatu. Katika Nehemia 1-6, Nehemia anajenga tena ukuta wa mji. Nehemia 7-12 inaorodhesha watu waliorudi Yerusalemu na inasimulia kufanya agano upya. Nehemia 13 inaangazia matatizo yaliyotokea baada ya Nehemia kurudi Yerusalemu mara ya pili. Mpangilio huu unaonesha kwamba ujenzi wa ukuta haukutosheleza; Yuda walihitaji uamsho ili kuangazia tatizo la asili ambalo lilipelekea uhamisho.

### Mambo Yaliyorudiwa Rudiwa

Kujirudia rudia ni njia ambayo waandishi wa Biblia wanaweza kuitumia kusisitiza nyenzo.

### *Maneno na vishazi vilivyorudiwa rudiwa*

Neno *kumbuka* limerudiwa rudiwa katika kitabu chote cha Nehemia. Nehemia anamuuliza Mungu "likumbuke neno lile ulilomwamuru Musa, mtumishi wako" (Nehemia 1:8). Wakati watu wa Yerusalem wametishiwa, Nehemia anawauliza "mkumbukeni Bwana, aliye mkuu mwenye kuogofya" (Nehemia 4:14). Mara tatu, Nehemia anaomba Mungu amkumbuke yeye na uaminifu wake. Kumbukumbu ni muhimu kwa Nehemia; kile Mungu amefanya huko nyuma kinatoa ujasiri katika uaminifu wa Mungu huko mbeleni.

► Soma Zaburi 119:1-32. Kila mstari unatumia baadhi ya maneno yanayorejelea Neno la Mungu. Kutokana na hili, tengeneza orodha inayoonesha kile ambacho mzaburi anaamini kuhusiana na umuhimu wa Neno la Mungu.

### *Watu waliorudiwa rudiwa*

Barnaba ametokea tena katika maeneo muhimu sana wakati wote katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Kila wakati Barnaba alipotokea, aliliishi jina lake alilopewa, "Mwana wa faraja" (Matendo ya Mitume 4:36). Barnaba anamleta Paulo kwa mitume na kushuhudia ukweli wa badiliko la Sauli (Matendo ya Mitume 9:27). Akiwa na Paulo, Barnabas analijenga kanisa la Antiokia (Matendo ya Mitume 11:22-26). Pasipo kujali mashaka ya Paulo, Barnaba anamtia moyo kijana mdogo Yohana Marko (Matendo ya Mitume 12:25 na Matendo ya

Mitume 15:36-39). Barnaba kuonekana kwa kujirudia katika kitabu cha Matendo ya Mitume kunaonesha ni kwa namna gani kanisa la kwanza lilitimiza Agizo kuu la kufanya waamini kuwa wanafunzi.

***Matukio au Mazingira yaliyorudiwa rudiwa***

Kitabu cha Waamuzi kinajumuisha mfululizo wa habari za kuanguka kwa Israeli kutoka ushindi mkuu chini ya uongozi wa Yoshua hadi kwenye ghasia za kijamii. Mara saba mzunguko umerudiwa ambapo wana wa Israeli wanafanya yaliyo mabaya mbele za Mungu na wanashindwa na adui zao. Kila wakati Mungu alimwinua mwamuzi ili kuwakomboa. Habari hii inayorudiwa rudiwa inaonesha kuanguka kwa taifa la Israeli.

**Kuhama kwa Mwelekeo**

Kuhama kwa mwelekeo ni mabadiliko katika msisitizo wa mwandishi. Kwa mfano, mwelekeo wa Paulo mara nyingi hubadilika karibu na katikati ya kitabu. Waefeso inaanza na msisitizo wa nini Mungu amefanya kwa watu wake; sehemu ya pili ya Waefeso inasisitiza nini watu wa Mungu wanatakiwa kufanya kama utii kwa Mungu.

Katika Waefeso 1-3, vitenzi vielezi vinaonesha nini ambacho Mungu amefanya kwa watu wake. Mungu:

- Aliyetubariki (Waefeso 1:3, 6)
- Alivyotuchagua (Waefeso 1:4)
- Alitangulia kutuchagua (Waefeso 1:5)

Kuanzia Waefeso 4:1, Paulo anaangazia wajibu wa mwamini wa kuishi katika namna inayopasa kazi ya wokovu ndani yetu. Katika Waefeso 4–6, vitenzi vingi vinaonesha maagizo. Paulo anatuagiza sisi:

- Mkaseme kweli (Waefeso 4:25)
- Msimuhuzunishe Roho Mtakatifu (Waefeso 4:30)
- Mkaenende katika upendo (Waefeso 5:2)
- Mnavyoenenda (Waefeso 5:15)
- Waheshimu baba yako na mama yako (Waefeso 6:2)
- Vaeni silaha zote za Mungu (Waefeso 6:11)

Mabadiliko ya mwelekeo kutoka kufurahia kile ambacho Mungu amefanya kwa ajili yetu kwenda kwenye vile ambavyo sisi tunatakiwa kuishi kama mwitikio wa neema yake unaonekana katika vitenzi. Kuchunguza kwa makini mabasiliko hayo kutatuandaa sisi kutafsiri kwa usahihi ujumbe wa Paulo katika Waefeso.

**Muundo wa Uandishi**

Ingawa kuna njia nyingi tofauti tofauti ambazo kitabu kinaweza kupangwa, aina tatu za muundo wa uandishi ni rahisi kutambua.[16]

***Muundo wa Kiwasifu***

Vitabu vya historia mara nyingi vimepangwa kuzunguka watu mahususi. Habari inamsingi katika matukio ya maisha ya mtu. Kwa mfano:

| **Mwanzo 12-50: Watu Wanne Mashuhuri** | |
|---:|---|
| **Sura** | **Mtu** |
| Mwanzo 12-25 | Ibrahimu |
| Mwanzo 25-26 | Isaka |
| Mwanzo 27-36 | Yakobo |
| Mwanzo 37-50 | Yusufu |

Samweli wa 1 na 2 inafuatilia kupanda na kuanguka kwa wafalme wawili wa kwanza wa Israeli, Sauli na Daudi.

| **1 & 2 Samweli: Wafalme wa Kwanza wa Israeli** | |
|---:|---|
| **Sura** | **Kupanda/kuanguka kwa wafalme** |
| 1 Samweli 1-8 | Nabii Samweli |
| 1 Samweli 9-12 | Kupanda kwa Sauli |
| 1 Samweli 13-31 | Kuanguka kwa Sauli & Kupanda kwa Daudi |
| 2 Samweli 1-10 | Mfanikio ya Daudi |
| 2 Samweli 11-24 | Mapambano ya Daudi |

***Muundo wa Kijiografia***

Jiografia inatoa muundo wa baadhi ya vitabu. Habari inaendelea kwa kadiri matukio yanavyotokea katika maeneo tofauti tofauti ya kijiografia. Atlasi ya Biblia itakusaidia kuweka muundo wa yaliyomo katika vitabu hivi.

[16] Nyenzo hizi zimechukuliwa kutoka katika sura ya 15 ya Howard G. Hendrick na William D. Hendricks, *Living by the Book* (Chicago: Moody Publishers, 2007).

| Kutoka: Safari ya Israeli | |
|---|---|
| **Kifungu** | **Eneo** |
| Kutoka 1:1-3:16 | Israeli Misri |
| Kutoka 13:17-18:27 | Israeli jangwani |
| Kutoka 19-40 | Israeli katika mlima Sinai |

Yesu aliwaagiza wanafunzi wake kuwa mashahidi wake "katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Matendo ya Mitume 1:8). Kitabu cha Matendo ya Mitume kinafuatilia kanisa la kwanza linavyotimiza Agizo hili.

| Matendo ya Mitume: Injili Inafikia Mataifa | |
|---|---|
| **Sura** | **Eneo** |
| Matendo ya Mitume 1-7 | Yerusalemu |
| Matendo ya Mitume 8-12 | Yudea & Samaria |
| Matendo ya Mitume 13-28 | Mwisho wa nchi |

***Muundo wa Kihistoria au Kiwakati***

Baadhi ya vitabu vimeundwa kwa kuzingatia mpangilio wa matukio muhimu ya kihistoria, mara nyingi ni mpangilio wa muda. Kuwekea alama matukio haya kutatupatia mtazamo wa jumla wa kitabu.

Kitabu cha Yoshua kinafuatilia kuteka na kukaa Kanaani. Muundo wa Yoshua unafuata matukio ya msingi ya kuteka (nchi ya Kanaani).

- Kuvuka kwenda Kanaani (Yoshua 1–5)
- Kuuteka Yeriko (Yoshua 6)
- Kushindwa kule Ai (Yoshua 7–8)
- Kufanya agano upya huko Shekem (Yoshua 9)
- Kampeni ya vita ya kusini (Yoshua 10)
- Kampeni ya vita ya Kaskazini (Yoshua 11–12)
- Mgawanyo wa ardhi na makazi (Yoshua 13–23)
- Kufanya agano upya huko Shekem (Yoshua 24)

Kusudi la Yohana kuandika injili yake limetamkwa mwishoni mwa kitabu. "Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake" (Yohana 20:30-31). Injili ya Yohana

imepangwa kuzunguka miujiza saba ambayo inatimiza kusudi lake. Ishara hizi saba zinatoa muundo wa kitabu chote:

- Kubadili maji kuwa divai (Yohana 2:1-12)
- Kumponya mwana wa Afisa (Yohana 4:46-54)
- Uponyaji katika Bethzatha (Yohana 5:1-47)
- Kulisha watu 5,000 (Yohana 6:1-4)
- Kutembea juu ya maji (Yohana 6:15-21)
- Kumponya mtu aliyezaliwa kipofu (Yohana 9:1-41)
- Kumfufua Lazaro (Yohana 11:1-57)

## Kuona Picha Kubwa

Hadi sasa, tumechunguza taarifa kuhusiana na mstari, kifungu kikubwa cha maandiko, na vitabu vyote.[17] Hatua ya mwisho ni hatua ya Uchunguzi ni kupanga taarifa ya uchunguzi katika mfumo ambao ni rahisi kutumia. Njia mojawapo nzuri ya kutumia ni kuweka nyenzo katika jedwali la ufupisho. Hii inaonesha muunganiko baina ya sehemu kubwa katika maandiko. Pia inatoa ufupisho katika maandalizi ya hatua ya tafsiri katika kujifunza Biblia.

Zipo njia nyingi tofauti tofauti za kupanga jedwali hili. Mgawanyo katika jedwali unategemea mtindo wa kifungu unachojifunza. Katika sehemu hii, tutatumia aina kadhaa za majedwali ili kuonesha namna ambavyo jedwali linaweza kukusaidia kujifunza Biblia.

### Kuweka Kwenye Jedwali Matukio Yanayohusiana

Ilikuwa imetajwa hapo awali kwamba mgawanyo wa sura mara nyingine hauendani na muundo wa kitabu. Jedwali linaloonesha mahusiano baina ya matukio linaonesha umoja wa mfululizo wa matukio ambayo yanatokea katika sura kadhaa. Mara nyingi hii itaonesha ulinganifu au ukinzani baina ya matukio.

Marko 4:35—Marko 5:42 inaonesha mfululizo wa Miujiza minne. Kama ukilinganisha habari nne, utaona kwamba habari zinaonesha kukosa imani kwa wanafunzi wa Yesu katikati ya dhoruba na imani ya watu ambao hawakutegemewa: mtu aliyepagawa na pepo, mwanamke aliyetokwa na damu, na kiongozi wa sinagogi. Marko inaonesha kwamba wanafunzi walikuwa mashuhuda wa kuona kwa macho kwa kila habari hizi kubwa za imani kubwa. Zitazame habari hizi upande kwa upande:

---

[17] Nyenzo katika sehemu hii yana msingi katika sura ya 24-25 ya Howard G. Hendricks na William D. Hendricks, *Living by the Book* (Chicago: Moody Publishers, 2007).

| Miujiza Minne | | |
|---|---|---|
| **Muujiza** | **Watu katika Habari** | **Jukumu la Imani** |
| Kutuliza dhoruba | • Yesu<br>• Wanafunzi | Wanafunzi hawakuwa na imani (Marko 4:40). |
| Kumponya aliyepagawa na pepo | • Yesu<br>• Mtu aliyepagawa na pepo<br>• Watu wa mji<br>• Wanafunzi (wakishuhudia) | • Mtu alimwabudu Yesu (Marko 5:6) na kumshuhudia Yesu (Marko 5:18-20).<br>• Watu wa mji walimkataa Yesu (Marko 5:10). |
| Kumponya mwanamke aliyetokwa na damu | • Yesu<br>• Mwanamke<br>• Wanafunzi (wakishuhudia) | Mwanamke alikuwa na imani na akachukua hatua ya kumgusa Yesu (Marko 5:28, 34). |
| Kumfufua binti Yairo | • Yesu<br>• Yairo na binti yake<br>• Waombolezaji<br>• Petro, Yakobo, na Yohana | Yairo alikuwa na imani (Marko 5:23). |

***Zamu Yako***

Andaa jedwali kwa msingi wa Mathayo 13:1-23.


1. Soma habari mara tatu.
2. Wekea alama Uchunguzi kwa kadiri unavyopata.
3. Jaza jedwali na mawazo wa msingi katika mfano.

Kumbuka kwamba Jedwali sio lengo; jedwali ni nyenzo ya kukuwezesha wewe kujifunza na kulitendea kazi neno la Mungu katika maisha yako. Lengo la kujifunza Biblia ni kubadilika. Katika kujifunza mfano huu, uliza, "Mimi ni udongo wa aina gani? Je, ninaliruhusu neno la Mungu kuzaa matunda katika maisha yangu?"

| **Mathayo 13:1-23 – Mfano wa Udongo** | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina za Udongo** | **Ukuaji** | **Vikwazo vya Ukuaji** | **Matokeo** |
| Njia | Hakuna ukuaji – mbegu imechukukuliwa. | Kukosa uelewa wa kweli. Udongo ni mgumu sana. | Hakuna matunda |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

***Zamu Yako***

Soma Marko 5:21-43. Ni habari moja ambayo ina miujiza miwili. Habari ya mwanamke aliyetokwa damu inaingilia kati habari ya Yairo na binti yake. Ni nini ulinganifu na ukinzani kati ya habari hizi mbili? Muundo unaonekana kama hivi:




| Marko 5:21-43: Ulinganifu na Ukinzani | | |
|---|---|---|
| | **Yairo** | **Mwanamke aliyetokwa na damu** |
| **Ulinganifu** | Anaonesha imani kubwa | Anaonesha imani kubwa |
| | | |
| | | |
| **Ukinzani** | Mtu mwenye mamlaka | Mwanamke asiye na hadhi yeyote |
| | Anamwendea Yesu hadharani | Anamwendea Yesu kwa siri |
| | | |
| | | |

**Jedwali la kitabu chote**

Jedwali linaweza kukusaidia kufupisha kitabu chote. Hili linaonesha picha kubwa ya kitabu. Katika kuandaa jedwali, soma kitabu chote mara kadhaa. Angalia sehemu kubwa. Unaposoma, wekea alama maneno yaliyorudiwa rudiwa, maswali na majibu, na mahusiano mengine yanaoonesha muundo wa kitabu.

| **Kujifunza 1 Petro – Kutia Moyo kwa Watakatifu Wanaoteseka** | | |
|---|---|---|
| **Wokovu (1:1–2:10)** | **Kutii (2:11–3:12)** | **Mateso (3:13–5:11)** |
| • Nafasi ya Wokovu (1:2-12)<br>• Matokeo ya Wokovu (1:13-25)<br>• Mchakato wa Wokovu (2:1-10) | • Katika serikali (2:13-25)<br>• Katika familia (3:1-12) | • Kama mwananchi (3:13–4:6)<br>• Kama mwamini (4:7-19)<br>• Kama mchungaji (5:1-11) |
| **Hatma ya Mkristo** | **Wajibu wa Mkristo** | **Maadili ya Mkristo** |

Sehemu tatu kubwa za 1 Petro zinahusiana. Hatutaweza kuelewa mateso (3:13–5:11) hadi tuwe tumejitiisha katika mapenzi ya Baba (2:11–3:12); hatutaweza kujitiisha kwa Baba hadi tuwe tumeelewa nguvu yake ya kuokoa (1:1–2:10).

***Zamu Yako***

Andaa jedwali lako kuhusiana na Waefeso. Jedwali hili litakusaidia kufuatilia dhana katika waraka wa Paulo. Mfano mmoja umetolewa. Unapomaliza, jiulize:

- Kuna mahusiano gani kati ya kila mada kuu?
- Je, kuna mada moja kati ya hizi ambayo imezungumzwa sana kuliko zingine?
- Ni kwa namna gani kila mada inahusiana na muundo mzima wa kitabu?

| Mada | Mistari juu ya mada hii | Ufupisho wa mafundisho ya Paulo |
|---|---|---|
| **Neema** | | |
| **Shetani** | 2:1-2 | |
| **Mwenendo wetu** | | |
| **Maombi** | | |

## Somo la 3 Dondoo Muhimu

(1) Unaendelea na mchakato wa Uchunguzi kwa kusoma kifungu cha maandiko na kisha kitabu chote. Kwa asili, Biblia ilikuwa haijagawanywa katika sura na mistari. Ni lazima uhakikishe kwamba unafuata mgawanyo wa asili wa andiko katika kujifunza kwako.

(2) Unaposoma kifungu cha maandiko, angalia:

- Mahusiano ya jumla kwenda mahususi
- Sehemu za swali na jibu
- Mahojiano
- Toni ya kihisia

(3) Unaposoma kitabu chote, angalia:

- Mambo Yanayosisitizwa. Mwandishi anaweza kusisitiza mambo akijumuisha:
    - Kiwango cha Nafasi
    - Kusudi lililotamkwa
    - Mpangilio wa nyenzo
- Mambo Yaliyorudiwa Rudiwa
    - Maneno na vishazi vilivyorudiwa rudiwa
    - Watu waliorudiwa rudiwa
    - Matukio au mazingira yaliyorudiwa rudiwa
- Kuhama kwa Mwelekeo
- Muundo wa Uandishi
    - Muundo wa Kiwasifu
    - Muundo wa Kijiografia
    - Muundo wa Kihistoria au Kiwakati

(4) Kutengeneza jedwali katika sehemu ya maandiko au kitabu chote kunaweza kuelezea muundo.

## Somo la 3 Zoezi

Katika Somo la 1, ulichagua kifungu cha maandiko ambayo utayasoma wakati wote wa kozi hii. Kwa kufuata hatua zilizotolewa katika somo hili, fanya uchunguzi kwa kiasi kikubwa juu ya kifungu ulichochagua. Kumbuka, haujaanza kutafsiri mstari au hauandai muhtasari wa ujumbe. Unaangalia tu taarifa za kina katika kifungu. Ikiwa ni muhimu, tayarisha jedwali linalofupisha Uchunguzi wako. Ikiwa unasoma kwenye kikundi, shirikisha Uchunguzi wako kwenye mkutaniko wenu unaofuata.

# Somo la 4
# Tafsiri: Utangulizi

## Malengo ya Somo

(1) Kuelewa umuhimu wa kutafsiri Biblia kwa usahihi.

(2) Kutambua baadhi ya changamoto ambazo zinafanya utafsiri wa Biblia kuwa mgumu.

(3) Kuelewa makossa yaliyozoeleka ambayo yanapelekea tafsiri isiyo sahihi.

(4) Kutunza unyenyekevu na uvumilivu kwa mawazo tofauti ya utafsiri wa Biblia.

## Utangulizi

Unamkumbuka Tinghao kutoka Somo la 1? Tinghao alisoma Biblia kila siku, lakini hakuweza kusikia sauti ya Mungu kupitia kile ambacho anakisoma. Shida ilikuwa ni nini? Tinghao hakuwa na mchakato wa kutafsiri kile ambacho anakisoma. Alisoma, lakini hakuweza kuelewa.

Matendo ya Mitume 8 inatueleza habari ya mtu mwingine alikuwa anasoma lakini hakuweza kuelewa. Filipo, shemasi katika kanisa la kwanza, aliongozwa na Roho Mtakatifu katika njia ya jangwa kutoka Yerusalemu kwenda Gaza. Huko alikutana na towashi mwenye mamlaka wa Kushi ambaye alikuwa anatoka hekaluni Yerusalemu kuabudu. Afisa yule alikuwa anasoma kutoka kitabu cha Isaya alipokuwa anasafiri.

> "Unifahamishe nami nitaishika sheria yako, Naam, nitaitii kwa moyo wangu wote."
>
> - Zaburi 119:34

Filipo alimuuliza towashi, "Je! Yamekuelea haya unayosoma?" (Matendo ya Mitume 8:30). Towashi alijibu, "Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza?" (Matendo ya Mitume 8:31). Filipo alipokuwa analielezea neno la Mungu, yule mtu alimwamini Yesu kwamba ni mwana wa Mungu na akabatizwa kama mwamini mpya.

Kufahamu jinsi ya kutafsiri kile unachokisoma ni muhimu. Katika masomo machache yajayo tutajifunza mchakato wa kutafsiri maandiko. Tutajifunza hatua za kivitendo kwa ajili ya kutafsiri.

## Umuhimu wa Tafsiri

Mahakimu watatu walikuwa wanajadiliana kuhusiana na kazi zao mahakamani. Hakimu wa kwanza anasema, "Kuna watu wenye hatia na kuna watu wasio na hatia. Ninawatambua kwa jinsi walivyo." Hakimu huyu anaamini kuwa kuna ukweli kuu. Kuna watu wenye hatia na watu wasio na hatia, na kazi ya hakimu ni kutangaza kile kilicho ukweli.

Hakimu wa pili anasema, "Kuna watu wenye hatia na watu wasio na hatia. Ninajaribu kutambua endapo mtu ana hatia au hana hatia. Hakimu huyu anajua kwamba kuna ukweli

kabisa, lakini pia anatambua kwamba anaweza kuwa na makosa katika maoni yake kuhusu mtu fulani.

Hakimu wa tatu alisema, “Mtu ana hatia au hana hatia hadi nitakapotoa tamko langu.” Hakimu huyu haamini juu ya kweli kuu. Anafikiri kwamba tamko lake ndilo linafanya kitu kuwa kweli.

Kwa huzuni, wakristo wengi hawaamini kwamba maandiko ni kweli kuu. Kisha wanasema, “Kile kilicho kweli kwako kinaweza kisiwe kweli kwangu.” Katika mtazamo huu, kila msomaji anatengenza “kweli” yake. Wanafikiria kuwa matamko ya kibiblia yanamaanisha vyovyote ambavyo yeyote anataka yamaanishe.

Kama hakimu wa pili katika habari. Wakristo wanahitaji kuelewa kweli mbili muhimu:

1. Maana ya maandiko ni kweli, na wajibu wetu ni kujaribu kuielewa kweli ya Mungu katika andiko.
2. Uelewa wetu una mipaka. Kwa sababu, tafsiri zetu zinaweza kuwa si sahihi. Tunatakiwa kuwa wanyenyekevu.


Katika hatua ya **Uchunguzi**, tuliuliza, “Ninaona nini katika andiko?” Katika hatua ya **Tafsiri** tunauliza, “Andiko linamaanisha nini?” Baadae, tunaangalia **matumizi** ya andiko katika maisha yetu.

Tunaanza mchakato wa tafsiri kwa kuuliza, “Mwandishi alikusudia kusema nini?” hii itatuandaa sisi kuuliza, “Maandiko yanamaanisha nini kwangu?”

### Changamoto Zinazokabili Tafsiri Sahihi

Zipo changamoto nyingi kwa wasomaji wa leo wanaotafsiri maandiko ya kale kama Biblia. Muda na nafasi inayotutenga sisi kutoka kwa waandishi wa asili inafanya kutafsiri kuwe kugumu. Tunazungumza lugha tofauti. Tamaduni zetu ni tofauti na tamaduni za waandishi wa Biblia.

**Kutafsiri Biblia**[18]




Picha hii inaonesha changamoto inayohusika katika kutafsiri Biblia katika siku zetu. Biblia iliandikwa kwa ajili ya ulimwengu wa kale (1). Wasomaji wa kwanza waliishi katika utamaduni tofauti na msomaji wa leo. Mto (2) ambao unatenganisha ulimwengu wao na wetu unafanya iwe ngumu kwa sisi kuelewa Biblia. Mto huu unaundwa na utofauti kati ya tamaduni zetu na ulimwengu wa Biblia. Ni tofauti gani kati ya msomaji wa leo na mwandishi?

### Tofauti ya Lugha

Biblia iliandikwa katika lugha tatu: Kiebrania, Kiyunani, na Kiaramu. Leo, wengi wetu husoma Biblia katika lugha yetu wenyewe. Hii inatengeneza umbali mkubwa kati yetu na mwandishi. Yeyote anayezungumza lugha ya pili anaelewa ugumu wa lugha.

### Tofauti ya Utamaduni

Ikifanana na ugumu wa lugha ni ugumu wa utofauti wa tamaduni. Waandishi wa maandiko walikuwa sehemu ya utamaduni ambao ni toauti na ulimwengu wetu. Tunaposoma maandiko, tunatakiwa kujiuliza, "Ninajifunza nini kuhusiana na utamaduni wa ulimwengu wa kale ambacho kitanisaidia mimi kuelewa na kuutafsiri ujumbe wa Biblia?"

[18] Picha: "Interpreting the Bible" imechorwa na Anna Boggs, inapatikana katika https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52377290578, licensed under CC BY 2.0. Concept from J. Scott Duvall and J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012)

**Jiografia Isiyojulikana**

Matukio ya Biblia yalitokea kwa watu halisi wanaoishi katika maeneo halisi. Kadiri tunavyoelewa jiografia, ndivyo tunavyoweza kuvuka vizuri mto unaogawanya ulimwengu wetu na ulimwengu wao.

Kujua kwamba barabara kati ya Yeriko na Yerusalemu inapita katika eneo hatari la milimani inaeleza tahadhari ya kuhani na Mlawi (Luka 10:31-32). Pia inatoa shukrani kwa ajili ya huruma ya Msamaria ambaye alihatarisha usalama wake ili kusaidia mgeni aliyejeruhiwa (Luka 10:33-34).

Wasomaji wameuliza, "Kwa nini wanafunzi walitilia shaka uwezo wa Yesu wa kulisha 4,000 katika Marko 8 baada ya kuwalisha 5,000 katika Marko 6?" Ramani inatoa jibu. Katika Marko 7, Yesu anasafiri hadi Dekapoli, eneo lenye watu wa Mataifa. Swali kwa wanafunzi halikuwa, "Je, Yesu **anaweza** kuwalisha watu hawa?" lakini "Je, atawalisha?" Hawakuamini kwamba watu wa mataifa mengine walistahili muujiza huo. Bado hawakuelewa kwamba Yesu amekuja kwa ajili ya watu wote.

| | **Marko 6** | **Marko 7** | **Marko 8** |
|---|---|---|---|
| **Nafasi** | Galilaya | *SAFARI* | Dekapoli |
| **Watu** | Wayahudi | - | Wamataifa |

Marko 4 inazungumza namna ambavyo Yesu alituliza dhoruba kwenye Bahari ya Galilaya. Katika atlasi ya Biblia, tunajifunza kwamba Bahari ya Galilaya ni ziwa kubwa, mita 210 chini ya usawa wa bahari. Kwa sababu sehemu iliyoinuka kuzunguka ziwa huelekeza upepo kama mtaro mwembamba, upepo hutengeneza dhoruba kali ndani ya dakika chache. Wakiwa ni wavuvi waliotumia maisha yao kwenye bahari hii, wanafunzi walizoea dhoruba kali. Ule ukweli kwamba walihofia maisha yao unatuambia kwamba dhoruba hii haikuwa ya kawaida. Hii ilikuwa dhoruba yenye nguvu isiyo ya kawaida, lakini ilichukua maneno machache tu kwa Yesu kuituliza bahari. Ndio maana walisema, "Ni nani huyu, basi, hata upepo na bahari humtii?" (Marko 4:36-41).

**Aina ya Fasihi Isiyofahamika**

Kila aina ya uandishi ni lazima isomwe kwa namna tofauti. Tunaposoma Warumi, ni lazima tufuatilie kwa makini hoja ya Paulo anapoonyesha jinsi tunavyofanywa kuwa sawa mbele za Mungu. Tunaposoma mfano, tunamsikiliza anayesimulia habari akifundisha kupitia habari ya ajabu.

**Hitimisho**

Angalia tena picha. Hata kama mto wa lugha, tamaduni, jiografia, na fasihi unatutenga sisi, Biblia ina ujumbe ambao unazungumza katika tamaduni zote. Hili ni daraja (3)

linalounganisha mto. Daraja linaundwa na kanuni ambazo Biblia inafundisha. Kanuni hizi ni kweli kwa tamaduni zote katika vizazi vyote.

Ramani (4) inatuuliza sisi wapi tupo katika habari ya Biblia. Ujio wa Kristo umetimiliza unabii na sheria za Agano la Kale. Kwa kukumbuka hili tutabadilisha namna ambayo tutatafsiri na kutumia vifungu hivi vya maandiko.

Mwisho, tunafika katika ulimwengu wetu leo (5). Katika hatua hii, tunauliza ki kwa namna gani kanuni tulizozipata (3) zitatumika katika ulimwengu wetu.

Tutakuja tena katika picha hii katika masomo yanayofuata. Kwa sasa, unatakiwa kuelewa hatua.

## Makosa Yaliyozoeleka ya Watafsiri wa Biblia

Yapo makossa kadhaa yaliyozoeleka ambayo watafsiri wa Biblia wanaweza kufanya.

### Kusoma Andiko Kimakosa

Baadhi ya wahubiri wamehubiri kwamba Paulo alisema, "Fedha ni shina la mabaya yoye." Lakini Paulo hakusema hivyo. Alisema, "Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha" (1 Timotheo 6:10). Inawezekana kuwa na fedha pasipo kuzipenda, na inawezekana kuipenda fedha, hata kama hauna fedha nyingi. Onyo la Paulo kimsingi si kuwa na fedha; ni kuhusiana na moyo ambao unatawaliwa na fedha.

Baadhi ya wakristo wanasoma kimakosa Zaburi 37:4 ikisema, "Mungu amehaidi kunipa haja za moyo wangu. Ninataka kuwa tajiri, kwa hiyo Mungu atanifanya mimi kuwa tajiri" Mzaburi anasema, "Nawe utajifurahisha kwa BWANA, Naye atakupa haja za moyo wako." Zaburi inahaidi kwamba kama tutajifurahisha kwa Bwana, Bwana atatupatia haja zetu – Bwana. Baadae, anaahidi kwamba kama tukiwa na njaa na kiu ya haki, tutajazwa - na haki (Mathayo 5:6). Hii si ahadi kwa mafanikio ya kiuchumi; ni ahadi kwa ajili ya jambo zuri zaidi – mafanikio ya kiroho.

Hatua ya kwanza tuliyojifunza katika kozi hii ni Uchunguzi. Uchunguzi wetu ni lazima uwe sahihi au tafsiri yetu haitakuwa sahihi. Kuwa makini usisome andiko kimakosa. Mtu mmoja alisema kwamba hatua tatu za kwanza za kujifunza Biblia ni:

1. Kusoma andiko.
2. Kusoma andiko tena.
3. Baada ya hatua ya pili, soma andiko tena!

### Kupindisha Andiko

Katika historia yote, waalimu wa uongo wamekuwa wanapindisha maandiko ili kutetea makossa yao. Paulo alionya kwamba baadhi ya watu watapindisha mafundisho yake ya kuhesabiwa haki kwa imani pekee ili kutetea shahuku zao za kuendelea katika dhambi kwa makusudi (Warumi 6:1-2). Kumekuwa na nyakati ambapo maandiko yametumika kutetea utumwa au serikali kuuwa kundi la watu wa utamaduni fulani. Leo, baadhi ya wahubiri

wamepindidha kweli ya Mungu kuwa Injili ya mafanikio ambayo ni kiyume na kweli ya maandiko.

Petro anawaonya wale wanaopindisha maandiko kwenda katika uharibifu wao wenyewe (2 Petro 3:16). Vilevile, Yakobo alizungumza sana juu wa wajibu wa wale wanaofundisha (Yakobo 3:1). Sisi tunaofundisha maandiko tunatakiwa kuwa makini kwamba tusipindishe maandiko ili kutetea mawazo au dhana potofu.

**Kutoa Maana ya Kufikirika**

Habari ya mahakimu watatu inaelezea kosa lingine llililozoeleka la watafsiri wa Biblia: dhana kwamba tafsiri ya maandiko inatoka katika fikra za msomaji. Baadhi ya watu wanajiuliza tu, "**Ninahisi** Biblia inamaanisha nini?" Wakati hisia na kujisikia ni kwa muhimu, kweli kuu ya maandiko ni ile ambayo mwandishi aliandika, na sio kile ambacho ninahisi ameandika.

**Kujiamini Kupita Kiasi**

Mtafsiri anaiamini akili yake sana kiasi kwamba anafikiri hawezi kukosea kabisa. Tunajifunza neno ili kufikia hitimisho la maana ya andiko; hata hivyo, tunatakiwa kuwa wanyenyekevu kukiri wakati hitimisho letu sio sahihi. Hakuna mwenye majibu yote.

Unyenyekevu katika tafsiri ni muhimu. Unapojifunza Biblia, utakutana na maeneo ambayo wakristo wacha Mungu wanatofautiana mawazo. Hii haina maana kwamba mara zote kuna upande mmoja ambao umepindisha andiko; unaweza kuwa ni utofauti kati ya pande mbili ambazo zimejikita katika kweli ya Mungu. Tunatakiwa kuendelea kuwa wanyenyekevu kwa kuzingatia tafsiri zetu ili kuweza kuvumuliana na wenye mtazamo tofauti.

**Zamu Yako**

Hapa chini ni baadhi ya matamko ambayo si sahihi ambayo watu wamekuwa wanayasema, wakifikiri wananukuu maandiko. Ili kuthamini usomaji makini, tafuta kifungu cha andiko ambalo limepindishwa katika kila mfano na nukuu kile ambacho Biblia inasema. Mfano wa kwanza umekamilishwa kwa ajili yako.

| Baadhi ya watu wanasema nini | Biblia Inasema nini |
|---|---|
| "Fedha ni shina la mabaya yoye." | "Shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha" (1 Timotheo 6:10). |
| "Kazi ni laana." | |
| "Mungu hawezi kukupa zaidi ya kile unachoweza kukibeba." | |

**Somo la 4 Dondoo Muhimu**

(1) Hatua ya tafsiri inauliza, “Andiko linamaanisha nini?”

(2) Baadhi ya changamoto zinazofanya tafsiri kuwa ngumu ni:

- Tofauti ya Lugha
- Tofauti ya Utamaduni
- Jiografia Isiyojulikana
- Aina ya Fasihi Isiyofahamika

(3) Baadhi ya makossa ambayo yanapelekea tafsiri isiyosahihi ni:

- Kusoma andiko kimakosa
- Kupindisha andiko
- Kutoa maana ya kufikirika
- Kujiamini kupita kiasi

# Somo la 5
# Tafsiri: Muktadha

## Malengo ya Somo

(1) Kuelewa thamani ya mazingira ya nyuma ya kihistoria-kiutamaduni kwa ajili ya kutafsiri Maandiko.

(2) Tumia maswali ili kugundua mazingira ya nyuma ya kihistoria-kiutamaduni ya kifungu cha andiko.

(3) Tambua ni kwa namna gani mstari mahususi unakaa vizuri katika muktadha unaozunguka mstari.

(4) Epuka makossa yaliyozoeleka katika kujifunza muktadha.

## Utangulizi

► Taja neno katika lugha yako ambalo lina maana zaidi ya moja. Mtu anapotumia neno hilo, ni kwa namna gani utafahamu maana anayomaanisha?

Moja kati ya Nyanja muhimu ya tafsiri ya Biblia ni muktadha wa kifungu ambacho unakisoma. Katika somo hili tutajifunza muktadha wa kihistoria-kiutamaduni na mazingira ya muktadha wa kifungu cha nadiko.[19]

## Muktadha wa kihistoria-kiutamaduni

► Soma 2 Timotheo 4:6-22.

Paulo anamwandikia Timotheo, "Jitahidi kuja kabla ya wakati wa baridi" (2 Timotheo 4:21). Sikiliza ombi la Paulo katika mwanga wa historia ifuatayo:

- Paulo yupo gerezani kule Rumi. Muda mfupi tu atauawa kwa ajili ya imani yake.
- Timotheo anahudumu Efeso, mamia ya kilometa toka Rumi.
- Kusafiri baharini ni hatari hasa wakati wa baridi. Kwa Timotheo kufika Rumi kabla ya baridi, anatakiwa aanze safari mara tu baada ya kupokea barua.

Muktadha wa kihistoria unaongeza katika sisi kutambua hisia nyuma ya ombi la Paulo. Paulo anasema zaidi ya, "Tafadhali nitembelee ukipata nafasi." Anamuomba mwanae wa kiroho, "Ninataka kukuona tena kabla ya sijafa. Endapo ukingojea hadi wakati wa baridi, usafiri hautawezekana. Tafadhali uje kabla haujachelewa." Barua ina ujumbe ule ule hata kama

---


[19] Nyenzo nyingi katika somo hili zinatoka katika sura ya 6-7 ya J. Scott Duvall na J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012).

haufahamu kabisa muktadha wa kihistoria, lakini Muktadha wa kihistoria unaonesha ukumbwa wa ombi la Paulo.

Muktadha wa kihistoria na kiutamaduni ni muhimu kwa sababu Mungu hakutoa Biblia katika lugha moja ambayo kila mtu duniani anaelewa. Matamko mawili kuhusiana na maandiko ni muhimu:

1. Kanuni za maandiko ni kweli kwa kila mtu wa kila mahali nyakati zote.
2. Kanuni a maandiko zilitolewa kwa watu mahususi katika mahali mahususi kwa wakati mahususi.

**Kutafsiri Maandiko**[20]




| | | |
|---|---|---|
| **1** | Mji wao | Ujumbe wa kwanza wa maandiko |
| **2** | Mto | Tofauti za kihistoria-kiutamaduni ambazo zinatenga ulimwengu wetu na ulimwengu wa kale |
| **3** | Daraja | Kanuni zinazofundishwa katika andiko |
| **4** | Ramani | Mahusiano na Agano Jipya (kwa ajili ya vifungu vya Agano la Kale) |
| **5** | Mji wetu | Matumizi ya kanuni katika ulimwengu wetu |

[20] Picha: "Interpreting the Bible" imechorwa na Anna Boggs, inapatikana katika https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52377290578, licensed under CC BY 2.0. Concept from J. Scott Duvall and J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012)

Kwa kadiri tunavyoelewa vizuri muktadha wa kihistoria na kiutamaduni wa maandiko, ndivyo tutaelewa vizuri kanuni za msingi za Biblia.

Tunapojifunza muktadha wa kihistoria-kiutamaduni, tunaisoma biblia katika "mji wao" ili uelewa ujumbe kwa wapokeaji wa kwanza. Kisha tutaangalia "mto" – Tofauti za kihistoria-kiutamaduni ambazo zinatenga ulimwengu wetu na ulimwengu wa kale. Jinsi tunavyoelewa vizuri ulimwengu wa Biblia, ndivyo tutakavyosikia vizuri zaidi neno la Mungu akiongea katika ulimwengu wetu leo.

Kusoma maandiko katika muktadha wake wa asili ni muhimu kwa sababu ndio msingi muhimu wa kanuni za kutafsiri Biblia: **Tafsiri yeyote sahihi ya andiko la Biblia ni lazima liwe sawasawa na ujumbe wa asili wa andiko.** Sitakiwi kutafsiri maana ambayo itakinzana na ujumbe wa asili wa andiko.

Muktadha wa kihistoria-kiutamaduni ni nini? Muktadha wa kihistoria-kiutamaduni ni kitu chochote nje ya andiko ambacho kinatusaidia sisi kuelewa andiko lenyewe. Hii inajumuisha majibu ya maswali kama vile:

- Maisha ya Waisraeli kule jangwani yalikuwaje (Muktadha kwa ajili ya Kutoka—Kumbukumbu la Torati)?
- Utamaduni wa Palestina ulikuwaje wakati wa karne ya kwanza (Muktadha kwa ajili ya Injili)?
- Waalimu wa uongo walikuwa ni nani ambao wanamsababishia Paulo kuchanganyikiwa katika Wagalatia na Wafilipi?

Baadhi ya maswali ya kuuliza unapojifunza muktadha wa kihistoria-kiutamaduni yanajumuisha:

**(1) Tunafahamu nini kuhusiana na mwandishi wa Biblia?**

Kwa sababu Mungu alizungumza kupitia waandishi wa kibinadamu, ufahamu wa waandishi utatusaidia kuelewa vema neno la Mungu.

Unaposoma nyaraka za Paulo, kumbuka maisha yake kabla ya kubadilishwa. Anapoelezea "alivyoutumainia mwili," (Wafilipi 3:4-6) fahamu kwamba mafarisayo waliheshimika sana kutokana na umakini wao wa kutii sheria. Tunapokumbuka unafiki wao na walivyokataa kumkubali Yesu, tukumbuke pia upendo wao kwa kila taarifa katika sheria ya Mungu.

Kwa upande mwingine, Paulo anapojielezea mwenyewe kwamba "wa kwanza" wa wenye dhambi, (1 Timotheo 1:15) kumbuka kwamba Paulo alilitesa kanisa na aliwatoa wakristo ili wauawe. Huyu ni yule mtu ambaye ameishi na kumbukumbu ya maisha yake ya awali kabla ya kukutana na Kristo akiwa njiani kuelekea Dameski.

Tunaposoma Kutoka, tunatakiwa kujifunza kuhusu heshima na upendeleo aliokuwa nao Musa katika ikulu ya Farao. Tunapofikiri kuhusiana na maisha ya anasa katika ikulu, kile ambacho Waebrania 11:25 anasema kuhusu Musa sasa kinakuwa na maana sana "…akaona

ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo." Tunapoona fursa za kielimu na kiutamaduni alizozifurahia kijana Musa, tunaona kwamba Mungu anamuaandaa mtumishi wake huyu kuongoza taifa kubwa.

**(2) Tunafahamu nini kuhusiana na wapokeaji wa Biblia?**

Pamoja na kujifunza kuhusu mwandishi wa Biblia, tunapaswa pia kujifunza kwa kadiri tunavyoweza kuhusu wapokeaji wa kwanza.

Nyingi kati ya nyenzo katika Mambo ya Nyakati ya 1 na 2 zimerudiwa kutoka Samweli na Wafalme. Kwa nini? Mambo ya Nyakati iliandikwa baada ya Waisraeli kurudi kutoka uhamishoni. Wafalme inaonesha ni kwa nini Mungu aliruhusu Israeli kupata hukumu; Mambo ya Nyakati inaonesha kwamba Mungu bado anawajali watu wake.

Yeremia anahubiri nyakati zinazozunguka uharibifu wa Yerusalemu. Tunaposoma ujumbe wake wa hukumu, tunapaswa kukumbuka kwamba hukumu iliyotamkwa iko karibu kutokea. Hata hivyo, katika Yeremia tunasoma pia ahadi ya Mungu, "Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho" (Yeremia 29:11). Ahadi hii inakuja wakati watu wako karibu kuchukuliwa kwenda utumwani katika nchi ya ugeni. Mpango wa Mungu kwa watu wake unajumuisha hukumu ambayo itawaleta katika toba.

Waraka wa 1 Yohana ulielekezwa kwa Wakristo wanaopitia mafundisho potofu: kwamba ni roho tu ndiyo nzuri; mwili na kila kitu kinachoonekana ni viovu. Waalimu wa uongo walisema kwamba Yesu hakuwa mwanadamu kamili; alionekana tu kuwa kama mwanadamu. Yohana anawakumbusha wasomaji wake kwamba Yesu alikuwa na mwili wa nyama unaoonekana. "Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tulililoliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa" (1 Yohana 1:1).

Waalimu wa uongo walisema pia wokovu unapatikana kupitia maarifa ya siri ambayo yanafunuliwa kwa watu wachache tu. Yohana anaonesha kwamba ni lazima tutii ili tuwe na maarifa ya kweli ya Mungu; "Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake" (1 Yohana 2:3). Maarifa yanayoleta uzima wa milele yanahusisha upendo "Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mautini kuingia uzimani, kwa maana twawapenda ndugu" (1 Yohana 3:14).

**(3) Tunafahamu nini kuhusiana na mazingira ya kihistoria ya kitabu?**

Hebu fikiria muhubiri anatangaza, "Leo nitahubiri namna ambayo mkristo anaweza kupata mke. Waamuzi 21:20-21 inatuambia kwamba tunatakiwa kwenda katika kijiji jirani na kungoja katika vichaka. Mmoja wapo wa wanawake vijana wanapokuja kutoka kijijini, mkamate na umbebe hadi nyumbani kwako. Hiki ndicho kielelezo cha kibiblia cha kuchagua mke." Ni lazima utilie shaka matumizi ya mhubiri juu ya matumizi ya maandiko!

Kitu gani hakiko sawa katika matumizi ya muhubiri? Waamuzi Inasema kwamba wanaume wa kabila la Benjamini walipata wake zao kwa namna hii wakati fulani. Hata inasema pia

walifanya hivi kwa sababu ambayo ilikuwa nzuri – kulitunza kabila moja la Israeli. Hata hivyo, muhubiri anapuuza muktadha wa kihistoria. Habari hii inakuja mwishoni mwa kitabu cha Waamuzi, kitabu kinachoonesha anguko la Israeli kutoka katika mpango wa Mungu hadi kwenye machafuko. Badala ya kuonesha mpango wa Mungu kwa ndoa, habari inaonesha kile ambacho kilitokea pale watu wa Mungu walipoasi.

Wakati mwignine tunafahamu kiasi kidogo kuhusiana na mwandishi na wapokeaji wake, lakini tunafahamu kuhusiana na mazingira ya kihistoria. Hatufahamu kuhusiana na mwandishi wa kitabu cha Ruthu, lakini tunafahamu matukio yaliyotokea katika siku ambazo waamuzi walitawala (Ruthu 1:1). Huu ulikuwa ni wakati wa machafuko ya kijamii katika Israeli (Waamuzi 21:25). Ikikinzanana ukosefu wa uaminifu kwa Mungu uliooneshwa na Israeli, kitabu cha Ruthu inaleta umakini katika uaminifu wa Ruth, mjane wa kimoabu.

Habari inatueleza namna Boazi alivyomuoa Ruth kwa hiari ili kuwainulia uzao watoto wa Naomi waliokufa. Kama mkombozi wa ukoo, Boazi alitoa sadaka urithi wake mwenyewe ili kumtunza Naomi. Katika kufanya hivyo, Boazi akapata nafasi katika ukoo wa Daudi (Mathayo 1:6, 16).

Muktadha wa kihistoria ni muhimu unapotafsiri kitabu cha Yona:

- Ninawi ilikuwa mji mkuu wa Ashuru adui mkubwa na hatari wa Israeli.
- Karibu na wakati ambapo Yona alikuwa anahubiri Ninawi, Amosi na Hosea walikuwa wanaonya kwamba hukumu ya Mungu ingekuja juu ya Israeli kupitia mikono ya waashuru.

Kwa mtazamo wa kibinadamu, Yona kukataa kuhubiri Ashuru kunaeleweka. Kitabu cha Yona inaonesha mtazamo wa Mungu, ambaye anawapenda watu wote bila kupendelea.

### (4) Tunafahamu nini Kuhusiana na Mazingira ya kiutamaduni ya Kitabu?

Muktadha wa kihistoria-kiutamaduni wa andiko pia unaagazia mila za kitamaduni za ulimwengu wa Biblia. Tunapata uelewa mpya wa mifano ya Yesu tunaposoma katika mwanga wa mazingira ya mila za Palestina katika karne ya kwanza:

- Mfano wa Msamaria mwema (Luka 10:30-35) ulikuwa ni mshangao kwa wapokeaji wa Kiyahudi. Wasikilizaji wa Yesu wasingeshangaa kuhusiana na viongozi wa dini kushindwa kumsaidia msafiri aliyekuwa amejeruhiwa. Hata hivyo, walitegemea ambaye angemsaidia angekuwa rabi au farisayo. Kinyume chake, Yesu anamuonesha Msamaria aliyedharauliwa kama kielelezo cha upendo.

- Katika mfano wa mwana mpotevu (Luka 15:11-32), tunapaswa tukumbuke kwamba wababa wa kiyahudi walikuwa wana heshima sana. Wasikilizaji walitegemea kwamba baba angekataa kumrejeza mtoto wake aliyerudi, au pengine angeruhusu awe mtumishi. Kinyume chake, baba aliachilia mbali habari za heshima yake katika furaha ya kurudi mwanae aliyepota. Kitendo hiki kinashangaza sana kiasi kwamba baadhi ya watu wa utamaduni wa mashariki wanauita mfano huu "Mfano wa baba

anayekimbia." Katika namna ile ile, Baba yetu wa mbinguni hatusubiri hadi sisi tujirekebishe ndipo tupokee msamaha; kinyume chake, anamtafuta mwenye dhambi aliyeasi. Hii ni picha ya upendo usio na kipimo wa Baba yetu.

Nyaraka za Paulo zinatakiwa kusomwa katika mwanga wa hali ya utamaduni ya karne ya kwanza. Waefeso 5:21–6:9 ilikuwa ya kushtusha kwa wasomaji wa Paulo. Agizo la Paulo la wanawake kutii waume zao lilikuwa ni la kawaida; Agizo lake kwamba waume wafuate kielelzo cha Yesu cha upendo wa kujitoa kilikuwa ni kigeni kwa wasikilizaji wa Kirumi. Watoto walitegemewa kuwatii wazazi wao, lakini hakuna hata mmoja katika ulimwengu wa Kirumi ambaye angemwambia baba asiwachokoze watoto wake.

Paulo anapowaambia Wafilipi kuishi kana kwamba wenyeji wao uko mbinguni, (Wafilipi 3:20) alikuwa anauandikia mji ambao ulikuwa na haki na upendeleo maalumu wa kiraia kwa raia wa dola ya Rumi. Kwa sababu mji ulianzishwa kama eneo la kupumzikia wanajeshi waliostaafu, wenyeji wa Filipi walijali sana uraia wao. Paulo anawakumbusha kwamba wao wenyeji wao uko mbinguni, na si katika miji ya duniani. Kwa kufahamu muktadha wa kihistoria-kiutamaduni kunatupa sisi uelewa mzuri wa Wafilipi.

### Kugundua Muktadha wa Kihistoria-Kiutamaduni

Kama tulivyoona, kujifunza kwetu muktadha wa kihistoria-kiutamaduni wa kifungu unaanza kwa kuuliza maswali. Ni kwa namna gani tutagundua majibu ya maswali yetu? Nyongeza ya kozi inatoa baadhi ya vyanzo ambavyo vinaweza kutupatia majibu ya maswali yetu. Tunashauri pia kutumia kozi za utangulizi wa Agano la Kale na Agano Jipya ambazo zinatolewa na Shepherds Global Classroom. Kozi hizi zitakupa historia ya nyuma ya kila kitabu katika Biblia.

## Muktadha wa Kibiblia

Kitu kingine cha kukiangalia kwa makini kwa ajili ya kutafsiri Biblia ni muktadha unaozunguka. Ni muhimu kuuliza, "Ni kwa namna gani mstari, kifungu, sura, na kitabu kinakaa vema katika Biblia nzima?"

Hebu fikiri umepata kipande cha karatasi chenye ujumbe mfupi wa sentensi moja iliyonyofoka kutoka katika barua nzima. Karatasi inasoma, "Ndio, 7 ni sawa." Sentensi hii inamaanisha nini?

- Pengine mwandishi alikuwa na miadi na mtu mwingine. Anathibitisha kwamba saa 7:00 mchana ni sawa kwa kikao.
- Pengine mke wa mwandishi ametuma ujumbe akiuliza, "ni watu wangapi ninatakiwa kuwaalika kwa ajili ya chakula cha jioni ijumaa jioni?" Anajibu, "saba (watu) ni sawa."
- Pengine mwandishi ametoa ofa ya kuuza kitabu kwa $8.00. mtu mmoja anamuuliza, "Je, utapunguza bei hadi $7.00?" Mwandishi anajibu, "Sawa, $7 ni sawa."

Tutaelewa maana ya sentensi husika kama tu tutafahamu muktadha. Tunasoma sentensi katika muktadha wa kifungu chote. Tunasoma sentensi katika muktadha wa barua yote. Kwa upana zaidi, tunaweza kusoma barua katika muktadha wa mfululizo wa barua kati ya watu hawa wawili.

Maandiko yanafanya kazi kwa namna hiyo hiyo. Mstari husika ni lazima usomwe katika muktadha wa mistari inayozunguka, sura, na kitabu. Muktadha unakipanua kifungu kutoka katika muktadha wa karibu hadi kwenye Biblia nzima.


Ili kuelewa mstari husika, ni lazima tuangalie muktadha unaozunguka. Zaburi 1:3 inatupa ahadi nzuri kwa mtu ambaye hupendezwa na sheria za Bwana. Atakuwa kama mti unaopata maji vizuri na kuzaa matunda. "kila alitendalo litafanikiwa." Baadhi ya watu wamechukulia hii kama ahadi ya baraka za mali na mafanikio kwa kila mwamini.

Hata hivyo, unaposoma Zaburi yote ya 1, umakini si katika mafanikio ya mali bali mafanikio ya rohoni kwa wale ambao wanatembea katika sheria za Bwana. Zaburi inahitimisha na ahadi; Mungu "anaijua njia ya wenye haki, Bali njia ya wasio haki itapotea" (Zaburi 1:6). Ukinzani ni kati ya njia inayofahamika (ikiangaliwa na kuthibitishwa) na Mungu na njia ambayo inaelekea upotevuni.

Kwa kufuata Zaburi zingine zote na Biblia nzima, ujumbe umethibitishwa. Mafanikio ya mwamini hayapatikani katika umiliki wa mali, bali katika uthibitisho wa Mungu. Haya ndiyo mafanikio ya kweli.

Kusoma kifungu katika muktadha, fuata hatua hizi tatu:

1. Tambua namna kitabu kilivyogawanywa katika vifungu. Muktadha wa karibu wa mstari unaosoma ni upi?
2. Fupisha mawazo makuu ya kifungu katika sentensi moja au mbili. Hii itakusaidia kuuelewa ujumbe wa sehemu yote.
3. Soma kitabu chote na uliza, "Ni kwa namna gani kifungu ninachojifunza kinakaa vema katika ujumbe wa kitabu?"




*Biblia nzima > kitabu chote > kifungu au sura > mstari*

*Biblia > Nyaraka za Paulo > Warumi > Warumi 12-15 > Warumi 12:1-2*

Warumi 12:1-2 inatutaka sisi kujitoa kwa Mungu.

> Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

Hii inaanzisha sehemu (Warumi 12-15) ambayo inaonesha ni kwa namna gani kujitoa huku kutaonekana katika maisha ya kila siku ya mkristo. Kutembea kutoka muktadha wa karibu, Warumi 12-15 inafuata sura 11 za mafundisho yenye maelekezo ambayo yanaonesha namna tulivyopatanishwa na Mungu.

Zaidi ya muktadha wa Warumi, kila waraka wa Paulo unaonesha kujali kwake kuhusiana na utendaji wa kivitendo wa imani yetu ya Kikristo. Mwisho, Warumi 12:1-2 inaingia katika ujumbe wa Biblia yote wa kumtii Mungu na kujitoa kwa Mungu. Kwa mfano, Lugha ya Warumi 12:1-2 inaonesha lugha ya dhabihu katika Mambo ya Walawi. Jinsi tutakavyoelewa muktadha mpana vema wa Biblia, ndiyo maneno ya Paulo yanavyokuwa na nguvu.

### Zamu Yako

► Soma kila mistari ifuatayo na kisha soma muktadha wake wa karibu. Jadili ni kwa namna gani muktadha unaathiri uelewa wako wa mstari.

1. Soma Mathayo 18:20. Hii inamaanisha nini?
2. Sasa soma Mathayo 18:15-20. Je, hii inaathiriri maana ya 18:20?

1. Soma Warumi 8:28. Hii inaahidi nini?
2. Sasa soma Warumi 8:28-30. Ni ahadi gani njema katika 8:28?

1. Soma Ufunuo 3:20. Nani anaalikwa?
2. Sasa soma Ufunuo 3:14-21. Mwaliko unamlenga nani?

## Makosa Yaliyozoeleka Katika Kujifunza Muktadha

Kwa kuhitimisha somo hili, tutaangalia baadhi ya makosa yaliyozoeleka ambayo watafsiri wanafanya wanapojifunza muktadha wa maandiko.

### Kutumia Taarifa Zisizo Sahihi

Mwanafunzi alitoa mawasilisho yake katika Mathayo 19:23-24. Alisema wakati wa Yesu, kwamba lango moja la kuingia Yerusalemu liliitwa "tundu ya sindano." Lango hili lilikuwa finyu sana kiasi kwamba mzigo wa ngamia ilibidi uondolewe ili kwamba mnyama asukumwe kwa kulazimishwa kupita kupitia lango.

Yapo matatizo mawili katika mawasilisho ya mwanafunzi:

1. Hakuna ushahidi wa kibilia unaoonesha lango hili wakati wa Yesu. "Tundu ya sindano" ilimaanisha vile vile inavyomaanisha leo, tundu la sindano ya kushonea.

2. Kwa sababu taarifa ya historia yake haikuwa sahihi, mwanafunzi alifikia hitimisho lisilosahihi kuhusiana na andiko. Mawasilisho yake yalionesha kwamba tuondoe kila kitu kinachozidi katika maisha yetu ili tuweze kupenya katika ufalme wa Mbinguni.

Hata hivyo, Yesu hakua anafundisha kwamba ni vigumu kwa tajiri na mwenye mamlaka kuingia ufalme wa Mungu; alikuwa anafundisha kwamba haiwezekani! Wanafunzi walishtushwa na hili hadi wakauliza, "Ni nani basi awezaye kuokoka?"

Yesu hakujibu, "Ni vigumu ila ukijaribu kwa bidi unaweza kupenya." Alijibu kwa kutumia habari njema ya injili: "Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana." Katika kujifunza muktadha, usiache taarifa zisizo sahihi zikukoseshe.

### Kuweka Muktadha kuwa Kipaumbele kuliko Ujumbe

Hatari ya pili ni kuruhusu kujifunza muktadha kuwa muhimu kuliko ujumbe wa andiko. Paulo aliwakumbusha wakristo wa Korintho kwamba taarifa zisizo sahihi zinaweza kusababisha kiburi, lakini upendo huwanufaisha wengine (1 Wakorintho 8:1).[21] Ni rahisi kufurahishwa na taarifa za muktadha kiasi ambacho tunasahau ujumbe wa andiko tunalojifunza.

Mtu anaweza akajifunza kila kitu kuhusiana na utamaduni wa Wasamaria na kusahau kusudi la mfano wa msamaria mwema: "Enenda... ukafanye vivyo hivyo" (Luka 10:37). Katika jambo hili, ufahamu wetu hautakuwa na matumizi. Jifunze ili kupata ujumbe wa andiko; usizikwe katika kujifunza kwa ajili yako mwenyewe. Jifunze ili kufundisha na kuhubiri kwa ufanisi, si kwa ajili ya kujivuna kwa ajili ya ufahamu wako mkubwa!

### Somo la 5 Dondoo Muhimu

(1) Tafsiri sahihi inahitaji kujifunza muktadha wa kila kifungu mahususi cha Biblia.

(2) Muktadha wa kihistoria-kiutamaduni unazingatia mazingira ya kitamaduni ya Biblia. Uliza:

- Tunafahamu nini kuhusiana na mwandishi wa Biblia?
- Tunafahamu nini kuhusiana na wapokeaji wa Biblia?
- Tunafahamu nini kuhusiana na mazingira ya kihistoria ya kitabu?
- Tunafahamu nini kuhusiana na mazingira ya kiutamaduni ya kitabu?

(3) Muktadha wa Biblia unaagazia ni kwa namna gani mstari unakaa vizuri katika andiko lote.

[21] Paulo hayuko kinyume cha maarifa; aliandika waraka ili kutoa maelekezo mazuri kwa kanisa changa. Hata hivyo, "maarifa" yenye kiburi cha Wakorintho yanachopelekea uharibifu, na sio kujenga.

**Somo la 5 Zoezi**

Katika Somo la 1, ulichagua kifungu cha maandiko ambayo utayasoma wakati wote wa kozi hii. Jifunze muktadha wa kihistoria-kiutamaduni na muktadha wa Biblia wa andiko ulilolichagua. Andaa ukurasa wa nakili ambapo utajibu maswali mengi kwa kadiri inavyowezekana kutoka katika majadiliano ya somo hili kuhusianana Muktadha.

Uliza:

- Mwandishi ni nani?
- Aliandika lini?
- Historia yake ya nyuma ni ipi?
- Wapokeaji wake ni nani?
- Walikuwa na matatizo gani?
- Ni mazingira gani yanayozunguka kifungu?
- Ni matukio gani ya kihistoria ambayo yalitokea wakati wa kitabu hiki?
- Ni vitu gani katika utamaduni ambavyo yanasaidia kuelezea kitabu?

Soma sura zinazozunguka kifungu ili kutambua muktadha wa Biblia wa kifungu.

# Somo la 6
# Tafsiri: Aina za Fasihi

## Malengo ya Somo

(1) Kutambua sifa za aina mbalimbali za fasihi zinazopatikana katika maandiko.

(2) Kuelewa ni kwa namna gani aina ya fasihi inaathiri tafsiri ya andiko.

(3) Tambua endapo simulizi mahususi ya kihistoria katika maandiko inapaswa kutafsiriwa kama kielelezo cha kufuata.

(4) Tambua kanuni ambazo zinafanya kazi kwa watu wote wa nyakati zote katika kifungu chochote cha maandiko.

(5) Tambua matumizi ya vifungu vya Agano la Kale kwa ajili ya mwamini leo.

## Utangulizi

*Angalizo kwa kiongozi wa darasa: Tunakushauri kufundisha somo hili katika vipindi viwili kwa sababu ya kiasi cha nyenzo kinachotakiwa kufunduishwa. Wanafunzi watakuwa na zoezi baada ya kipindi cha pili.*

Kufahamu aina za Fasihi kunatusaidia sisi kutafsiri maandiko.

Biblia inapotuambia kwamba Daudi alichunga kondoo (1 Samweli 16:11), tunafahamu kwamba inaongea kuhusiana na kondoo wa kawaida, kwa sababu alikuwa mchungaji. Wakati kitabu cha Ufunuo kinasema Yohana aliona joka kubwa (Ufunuo 12:3) au kitu kama simba au dubu, tunafahamu kwa hakika, wanyama hao waliwakilisha vitu vingine kwa sababu kitabu cha Ufunuo kina alama nyingi.

Wakati 1 Wafalme 5:6 inatuambia kwamba Sulemani alileta miti ili kutumia kwa ajili ya ujenzi wa hekalu huko Yerusalemu, tunafahamu kwamba alileta miti halisi. Wakati Zaburi 1:3 inasema mwenye haki ni kama mti ulipandwa kando ya mto, tunafahamu kwamba alikuwa anafanya ulinganifu. Wakati Isaya 55:12 inasema kwamba miti itapiga makofi, inamaanisha kutakuwa na furaha hata asili pia inaonekana kufurahia.

Kuelewa aina ya fasihi ni muhimu katika kutafsiri Biblia. Kitabu cha ushairi (Zaburi) kitawasilisha tofauti na waraka (Warumi). Kuelewa tofauti kutatusaidia sisi kutafsiri kila kitabu kama mwandishi alivyokusudia. Hapa ni utangulizi wa aina kubwa za fasihi katika maandiko.

**Aina ya Fasihi: Historia**

Sehemu kubwa ya Biblia ni historia: Pentatuki, vitabu vya historia, Injili, na Matendo ya Mitume, na sehemu zingine fupi fupi ni historia ya kweli na ya uhakika ya watu halisi na matukio halisi.

(Biblia pia ina vielelezo vya kufikirika vilivyotolewa na manabii na mifano aliyotoa Yesu. Tutajadili tafsiri ya hivi katika sehemu inayofuata kwa sababu ni tofauti na tafsiri ya simulizi za kihistoria.)

**Maswali ya Kuuliza Unaposoma Historia**

Unatakiwa kuuliza maswali wakati unasoma simulizi ya historia ya Biblia:

**(1) Habari ni nini?**

Unaposoma simulizi, tunaangalia Muundo wa habari. Kwa mfano, Injili ya Luka inafuatilia huduma ya Yesu kule Galilaya; kisha inaangazia safari ya Yesu kwenda Yerusalemu na kujikita katika mafundisho yake kuhusiana na uanafunzi; Luka anahitimisha kwa kujikita katika kifo na ufufuo huko Yerusalemu. Katika Matendo ya Mitume, Luka anaonesha kukua kwa huduma ya kanisa. Tena, anafuata Muundo wa kijiografia. Injili inahubiriwa Yerusalemu; kisha inachukuliwa hadi Yudea yote na Samaria; na mwisho, Injili inaenda mwisho wa dunia kupitia huduma ya Paul kule Rumi.

**(2) Watu katika habari ni nani?**

Tunaposoma kuhusiana na watu wa kihistoria katika Biblia, tunajifunza kuhusiana na nguvu tunazoweza kuzitengeneza na udhaifu tunaotakiwa kuuepuka. Tunauliza maswali kama, "Nini kilimfanya Nehemia kuwa kiongozi mwenye ufanisi?" na "Nini kilikuwa ni tofauti kati ya kushindwa kwa Sauli na kufanikiwa kwa Daudi?" Tunalinganisha njia ya uinjilisti ya Petro na Paulo. Katika historia ya Biblia, tunapata picha ya watu.

**(3) Je, simulizi hii ya kihistoria inatoa mfano gani wa kufuata?**

Tunaposoma historia, tunapaswa kuuliza endapo matendo yanayooneshwa ni mifano kwa sisi kufuata. Simulizi ya kihistoria inaweza kutoa kielelezo cha kile ambacho Mungu anatarajia kutoka kwa watu wake. Kwa upande mwingine, inaweza kutoa historia muhimu ambayo haitoi kielelezo cha kufuata.

Unakumbuka mfano uliotolewa kuhusiana na muhubiri aliyetumia Waamuzi 21 kuhubiri juu ya namna ya kupata mke? Katika mfano ule, muhubiri alishindwa kuuliza, "Je, Waamuzi anaagiza Agizo hili au ni namna tu kuelezea kitendo?" Waamuzi 21 inaelezea matendo ya Waisrael; haiagizi kufuata tabia.

Unaposoma historia, tunatakiwa kuuliza, "Je, huu ni mfano wa kufuata?" au "Je, haya ni maelezeo ya habari?" Katika hali nyingi, jibu ni rahisi; hakuna anayeweza kufikiri kwamba Waamuzi 21 inatuagiza sisi kuteka mke! Hata hivyo, hali nyingi haziko wazi. Kitabu cha Matendo ya Mitume mahususi kabisa ni kigumu. Je, kanisa litegee Mungu kufanya Miujiza

ambayo ilifanyika katika siku za kanisa la kwanza? Je waamini walijazwa na Roho Mtakatifu watanena kwa lugha mpya?

Ni kwa namna gani sasa tutaweza kuamua endapo kifungu kinatupa sisi kielelezo cha kufuata? Kama hatutajibu swali hili kwa usahihi, hatutasoma kwa usahihi vitabu vya kihistoria kama vile Waamuzi na Matendo ya Mitume. Kama hatutajibu swali hili kwa usahihi, tutasisitiza au kupuuza taarifa za kibiblia kwa kutegemea upendeleo wetu. Kumbuka kanuni hii: **kama kifungu cha historia kinatupa sisi kielelezo cha kufuata, tunategemea kupata maelekezo ya wazi au mifano iliyorudiwa katika vifungu vingine.**

Kwa mfano, Matendo ya Mitume inaonesha kwamba wakristo wa kwanza walikuwa na shahuku kuhusiana na uinjilisti. Tunafahamu kwamba huu ni mfano kwetu sisi kuufuata kwa sababu Mathayo 28:19-20 inatuagiza sisi kufanya wanafunzi. Matendo ya Mitume inaonesha kazi za Roho Mtakatifu katika kanisa. Tunafahamu kwamba hii inatakiwa kuwa sehemu ya kawaida ya maisha ya kanisa kwa sababu Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu atatia nguvu huduma ya wafuasi wake (Matendo ya Mitume 1:8). Kama tutashindwa kuhubiri au kuonesha nguvu ya Roho Mtakatifu katika huduma zetu, hatuishi sawasawa na kielelezo cha Matendo ya Mitume. Habari hizi ni kielelezo kwa kanisa.

Matendo ya Mitume pia inatueleza kwamba wakristo walikuwa na vitu vyote shirika na waliabudu katika nyumba za binafsi. Je, haya ni maagizo kutoka katika maandiko? Hapana. Utaratibu wa kuwa na vitu vyote shirika ulikuwa wa hiari, si lazima, kama Petro alivyomwambia Anania (Matendo ya Mitume 5:3-4). Vivyo hivyo, maandiko hayatuagizi sisi kuabudu katika nyumba binafsi.[22]

Kwa sababu matendo haya hayajaagizwa katika maandiko, tunaweza kuhitimisha kwamba ni sehemu ya historia ya kanisa lakini si lazima kwamba ni kielelezo kwa sisi kufuata. Matendo ya Mitume inaelezea kipindi fulani katika historia; haiagizi matendo haya kwa nyakati zote.

### (4) Je, ni kanuni gani zinazofundishwa katika simulizi ya kihistoria?

Kutokana na Paulo, historia ya Biblia inatolewa kwa ajili ya maelekezo (1 Wakorintho 10:11). Inaonesha namna Mungu anavyofanya kazi katika historia na kile kinachompendeza au kisichompendeza Mungu. Kama wasomaji, tunatakiwa kutafuta kanuni kutoka katika simulizi za kihistoria.

Mara chache sana habari inasema, "Waisraeli walimlalamikia Mungu na wanaadhibiwa. Hautakiwi kumlalamikia Mungu." Badala yake, tunaambiwa kwamba Waisraeli walimlalamikia Mungu na tunaona madhara ya dhambi yao, na tunapaswa kuelewa kanuni inayofundishwa. Badala ya maagizo ya moja kwa moja, historia inatupa kielelezo chanya ili kufuata na kielelezo hasi ili kuepuka. Katika kitabu cha Yoshua, tunaona utii kwa maagizo

[22] Baadhi ya wakristo duniani leo wanaona kwamba kuabudu nyumbani ni salama zaidi kuliko kukusanyika katika sehemu za umma. Hii ni kulingana na mazingira, na si Agizo kuu.

ya Mungu ulileta ushindi; katika kitabu cha Waamuzi, tunaona kwamba uasi kunaleta machafuko.

### Kitabu cha Matendo ya Mitume

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinatoa habari ya kihistoria ya kile kilichotokea baada ya maisha ya Yesu hapa duniani. Kwa wasomaji wa Agano Jipya, Matendo ya Mitume Inatoa muktadha kwa nyaraka zilizoandikwa kwa makanisa.

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinaonesha kwamba kanisa, likiwezeshwa na Roho Mtakatifu, lisingeweza kuzuiwa katika utume wake wa kueneza Injili. Kanisa lilipitia mambo ya kimafundisho, migawanyiko ya ndani, changamoto katika uongozi, unafiki, upinzani wa kipepo, mateso kutoka kwa jamii, na majanga katika safari. Hata hivyo, kanisa lilitembea kifua mbele kwa furaha likishinda. Kwa sababu Roho Mtakatifu alilitia nguvu kanisa, watu binafsi na jamii zilibadilishwa na Injili.

Lengo la Luka kuandika Matendo ya Mitume lilikuwa ni kulipa kanisa ujasiri wa kuendelea kuutimiza utume wake wa kuufikia ulimwengu kwa Injili. Kusudi lake linaonekana katika kitabu chote katika dondoo zifuatazo. Dondoo nyingine za nyongeza zinaweza kuongezwa.

- Yesu aliwaambia wanafunzi wake kupeleka Injili hadi mwisho wa dunia (Matendo ya Mitume 1:8).
- Roho aliwatia nguvu wanafunzi kuhubiri Injili siku ya Pentekoste, na watu 3,000 waliamini (Matendo ya Mitume 2:41).
- Watu walikuwa wakiongezeka katika kanisa kila siku (Matendo ya Mitume 2:47).
- Kiongozi wa kidini Gamalieli alisema kwamba kazi ya Mungu haiwezi kuzuiwa (Matendo ya Mitume 5:39).
- Waamini walioteswa waliondoka Yerusalemu na kueneza Injili (Matendo ya Mitume 8:1, 4).
- Kiongozi wa mateso alibadilishwa na akawa muinjilisti mkubwa (Matendo ya Mitume 9:13-22).
- Paulo na wengine walifanya safari za kimisheni katika ulimwengu uliojulikana wa wakati ule (Matendo ya Mitume 13-21).
- Paulo aliwahubiria watawala (Matendo ya Mitume 24-26).
- Paulo alihubiri Rumi, mji mkuu wa dola (Matendo ya Mitume 28).

#### *Matumizi ya Kitabu cha Matendo ya Mitume*

Wakati mwingine msomaji anaweza kufikiri kwamba kitabu cha Matendo ya Mitume kinatueleza sisi **ni kwa namna gani** tufanye kazi ya kimisheni, kubatiza, kupanda kanisa, na uzoefu wa Roho Mtakatifu. Matendo ya Mitume inanakili namna ambavyo kanisa la

kwanza lilifanya hayo mambo yote; hata hivyo, mwandishi hakukusudia kitabu cha Matendo ya Mitume kiwe kitabu cha maelekezo kwa huduma.

Hatupaswi kufikiri kwamba tunapaswa kufanya kwa namna ile ile ambayo kanisa la kwanza walifanya katika kitabu cha Matendo ya Mitume, lakini tunaweza kujifunza mengi kutokana na vile tumeona kanisa lilivyokabiliana na changamoto.

Matendo ya Mitume inatuonesha sisi kwamba kanisa linatakiwa kuendelea kufika mbali na injili, mara zote likue na kupambana na matatizo yote kwa nguvu na hekima ya Roho Mtakatifu, likitengeneza Muundo kutokana na uhitaaji ili kutatua matatizo kwa vitendo.

## Aina ya Fasihi: Sheria za Agano la Kale

### Thamani ya Sheria za Agano la Kale

Baadhi ya Wakristo wanafikiri kwamba Agano la Kale linamatumizi machache kwa waamini wa leo ispokuwa tu zile sehemu ambazo zinaelezea kanuni za Kikristo. Wanafikiri kwamba Sheria za Agano la Kale hazina matumizi kwa waamini wa leo.

Mtume Paulo aliandika mara nyingi kuhusu mabadiliko ya matumizi ya sheria za Agano la Kale kwa mwamini. Alisema kwamba kifo cha Kristo kiliondoa hukumu ya sheria na kwamba hatupaswi kuwahukumu waamini ambao hawafuati taratibu za sheria ya Agano la Kale (Wakolosai 2:14-17). Alisema kwamba mitume hawaishi tena chini ya matakwa ya kisheria za Kiyahudi (Wagalatia 2:14-16). Alikataa mchungaji mmataifa kutahiriwa (Wagalatia 2:3). Alisema kwamba kila mmoja anatakiwa kufuata dhamiri yake kuhusiana na chakula cha kiyahudi na siku na kwamba waamini hawapaswi kuhukumiana kuhusiana na matakwa haya (Warumi 14). Alisema kwamba mwamini aliifia sheria na kwamba tunamtumikia Mungu katika namna ambayo inatimiza makusudi ya sheria lakini si matakwa ya sheria kimahususi (Warumi 7:4, 6). Muhimu zaidi, alisema kwamba hakuna atakayehesabiwa haki kwa matendo ya sheria (Warumi 3:20).

Biblia pia iantoa matamko kuhusiana na sheria za Agano la Kale likionesha kwamba bado zina umuhimu kwa mwamini. Kwa sababu sheria za Agano la Kale zilikuwa ni maelelezeo ya asili ya Mungu, mtu anayempenda Mungu atapenda na sheria zake (Ona Zaburi 1:2, Zaburi 119:7, 16, 70). Paulo alisema kwamba sheria ni takatifu, yenye haki, na nzuri (Warumi 7:12). Alisema pia, "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki" (2 Timotheo 3:16). Wakati anatamka tamko hili, neno *maandiko* kimsingi lilirejelea Agano la Kale. Paulo alimwambia Timotheo kwamba maandiko yanamfanya yeye mwenye hekima kwa ajili ya wokovu (2 Timotheo 3:15). Matamko haya yanatuambia kwamba kama waamini hatupaswi kuiacha sehemu yeyote ya Agano la Kale. Hata kama hatuokolewi kwa kufuata sheria za Mungu, tunataka kuelewa kusudi lake kwetu ili kwamba tuweze kumpendeza Yeye (2 Wakorintho 5:9-10).

**Mgawanyo wa Sheria za Agano la Kale**

Ili kutusaidia kuelewa kwa namna gani waamini wanatakiwa kuzitumia Sheria za Agano la Kale leo, tumechunguza na kuona aina baadhi ya makundi ya sheria.

**Sheria za Kiibada** zilikuwa ni kuhusu dhabihu, taratibu za kidini, vyakula, na siku maalumu. Paulo anasema kwamba sheria hizi zilitimilizwa ndani ya Kristo (Wakolosai 2:16-17). Kitabu cha Waebrania kinatoa matumizi ya kina ya maana ya ibaada za Agano la Kale. Kwa mfano, karibu vitu vyote katika hekalu husafishwa kwa damu, ikiwakilisha damu ya Yesu ambayo itasafisha Waamini (Waebrania 9:14, 21-24).

**Sheria za Kiraia** zilitolewa kwa Taifa la Israeli. Sheria za kiraia hazijaanzishwa na mtu mmoja mmoja, bali zilianzishwa na mamlaka zilizochaguliwa. Kwa mfano, watu waliofanya uchawi waliuawa (Kutoka 22:18), lakini kesi na adhabu zilifanywa na mamlaka iliyowekwa, na si na raia mmoja mmoja. Kumbukumbu la Torati 17:2-12 inelezea mchakato wa serikali ya mji kusikiliza mashahidi na kutoa hukumu ya haki; mahakama ya juu ilikuwepo kwa ajili ya kezi zilizokuwa ngumu zaidi.

Sheria za nchi zinaweza kuwa tofauti leo, na waamini mmoja mmoja hapaswi kuchukua wajibu binafsi kwa kutimiliza sheria za kiraia za Israeli ya kale. Hata hivyo, sheria hizo zinatufundisha sisi kuhusiana na haki ya Mungu na haki ambayo anaitarajia kutoka kwa watu wake. Kwa mfano, sharia ilitolewa katika Kutoka 22:18 inatuambia kwamba si sahihi kwa mtu kufanya uchawi. Sheria zingine za kiraia zinatueleza kwamba Mungu anataka taifa kuwalinda masikini na kupinga mambo yasiyo ya haki kwa watu wote (Kumbukumbu la Torati 24:14-15, 17-22).

Mtafsiri wa Biblia anajaribu kwanza kuelewa kanuni ya sheria mahususi za kiraia za Agano la Kale, kisha anazingatia namna ambavyo mwamini anatakiwa kutendea kazi kanuni hiyo. Tunatakiwa kuuliza, "Mungu alikuwa anajali nini? Kusudi la Mungu lilikuwa nini? Sheria hii inafunua nini kuhusiana na maadili ya Mungu?" Kisha tunaangalia matumizi ya wakati huu ya ambayo yatampendeza Mungu.

**Sheria za Kimaadili** zilitaja matakwa ya kudumu ya Mungu kwa ajili ya kuishi vema. Sheria za kimaadili zinazungumzia uaminifu, mambo ya kijinsi, kuabudu sanamu, na mambo mengine (Kutoka 20:4-5, 13-16). Sheria nyingi za kimaadili zimerudiwa tena katika Agano Jipya. Sheria za kimaadili ni msingi wa sheria za kiraia za nchi nyingi leo, ingawaje sheria za nchi hazifuati sheria za Mungu kwa usahihi. Sheria za Mungu kwa ajili ya watu wake zinaenda mbali zaidi ya kile ambacho jamii inahitaji.

Mgawanyo wetu wa makundi ya sheria si kamilifu. Vifungu katika Agano la Kale wakati mwingine inajumuisha makundi yote matatu ya sheria na sheria ambazo ni ngumu kuziweka katika makundi. Hata kama sio kamilifu, mfumo wa mgawanyo huu unatusaidia sisi kuelewa sheria za Agano la Kale ambazo zinatenda kazi kwa waamini wa Agano Jipya.

**Kutafsiri Sheria za Agano la Kale**[23]

Unapojifunza sheria za Agano la Kale, zingatia muktadha mpana wa sheria unayojifunza. Kuwa makini na mazingira yanayozunguka simulizi. Ni kwa jinsi gani sheria inakaa vema katika muktadha?

Kisha uliza:

**(1) Andiko hili lilimaanisha nini kwa wapokeaji wa kwanza?**

Ili kuelewa namna Israeli walitafsiri sheria, uliza maswali kama vile:

- Je, kuna muunganiko kati ya sheria na mazingira yanayozunguka mistari?
- Je, sheria ni mwitikio wa hali mahususi inayohusiana na historia ya Israeli?
- Je, sheria inahusiana na mfumo wa haki wa Agano la Kale?

**(2) Ni tofauti gani iliyopo baina ya wapokeaji wa Biblia na ulimwengu wetu?**

Zipo tofauti nyingi kati ya ulimwengu wetu na wa Agano la Kale kuliko kati ya ulimwengu wetu na ule wa Agano Jipya. Kwa mfano:

- Hatutembelei tena hekalu moja; Roho Mtakatifu anakaa ndani ya kila mwamini.
- Hatumwendei Mungu kwa dhabihu, Yesu Kristo alikufa mara moja kwa zote (Waebrania 10:10).
- Neno la Mungu si sheria kwa nchi zetu. Tunaishi chini ya serilaki za kidunia.

**(3) Ni kanuni gani zinazofundishwa katika andiko hili?**

Tendo mahususi linalotakiwa na sheria za Agano la Kale linaweza lisihitajike leo. Tunatakiwa kutafuta kanuni ya kudumu inayofundishwa na sheria. Hili ni Daraja ambalo linaleta andiko kutoka mazingira ya kale katika ulimwengu wa leo. Kanuni hii itakuwa na mahusiano kati ya wapokeaji wa Agano la Kale na wapokeaji wa leo.

Taja kanuni katika sentensi 1-2. Ili kuhakiki endapo kanuni ni ya kibibli, uliza maswali haya:

- Je, kanuni inaoneshwa kwa uwazi na sheria?
- Je, kanuni hii inaweza kutumiwa na watu wote katika nyakati zote na mahali pote?
- Je, kanuni hii inakubaliana na maandiko mengine?

**(4) Je, Agano jipya linachukua kanuni hizi kwa namna yeyote?**

Kila mojawapo la maswali matatu yaliyopita yatumika katika tafsiri yeyote ya kifungu chochote cha maandiko. Swali hili la mwisho linatakiwa kuongezwa kwenye mchakato wa tafsiri wakati tunapojifunza maandiko ya Agano la Kale. Kama umepata kanuni ya kudumu

---

[23] Sehemu hii imetolewa kutoka J. Scott Duvall na J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012).

ya kifungu cha Agano la Kale, kanuni hiyo itabakia na matokeo yale yale leo. Hata hivyo, Agano Jipya linaonesha kwamba matumizi yanatofautiana na nyakati za Agano la Kale.

Kwa mfano, Kutoka 20:14 inaagiza, "Usizini." Katika mafundisho ya Yesu ya mlimani, Yesu anapanua hii ili kugusa mawazo, na si tu kitendo (Mathayo 5:28). Mafundisho ya Yesu hayaondoi kanuni ya Kutoka 20:14; yanapanua matumizi yake.

## Aina ya Fasihi: Ushairi

Biblia ina ushairi mwingi. Ayubu, Zaburi, Mithali, na Wimbo ulio Bora karibu yote ni ushairi, na Mhubiri inajumuisha baadhi ya ushairi. Kuna ushairi pia katika manabii. Ushairi ni aina ya uandishi ambayo inaonesha hisia kali. Haikuundwa ili kuwasilisha taarifa za kina za kihistoria au kutengeneza majadiliano ya kimantiki. Katika ushairi, tunausikiliza moyo wa mshairi; mahususi kabisa tunakuwa makini na hisia zinazooneshwa katika ushairi.

Mara nyingi ushairi unatumia tamathali za semi, na ni maelezeo ambayo hayakusudiwi kuchukuliwa kama lugha ya kawaida.

Hapa ni mfano wa tamko la kiushairi kutoka katika Zaburi: "Kwa upote wa uta wako [Mungu]ukiwaelekezea mishale" (Zaburi 21:12). Tunagundua kwamba kwa kawaida Mungu hana uta ambao atautumia kupiga mishale ya kawaida. Mwandishi anasema kwamba Mungu anaweza kumshinda yeyote ambaye anachagua kuwa adui yake. Mwandishi anawaeleza waamini kuwa na ujasiri na ushindi wa Mungu.

Mara nyingi ushairi unafanya kusudi la kufikirika ukiwasilisha kweli ambao umetajwa wazi sehemu nyingine katika Biblia. Usitengeneze kanuni ya imani au kutendea kazi kutoka katika kifungu cha ushairi kama haijafundishwa kwa uwazi katika vifungu vingine.

Mashairi ya Kiebrania wakati mwingine yanatumia muundo wa sauti lakini hawatumii vina na mizani kama mashairi ya Kiswahili yanavyotumia. Kuelewa sifa za mashairi ya Kiebrania kutakusaidia wewe kuelewa vema na kutambua uzusi wake.

### Sifa za Mashairi ya Kiebrania

#### *Usambamba*

Mara nyingi mashairi ya Kiebrania yana msingi katika usambamba. Sentensi mbili zilizo sambamba zinatumika pamoja; sentensi ya pili inaongeza maana zaidi kwa ile ya kwanza lakini si kila wakati inaongeza taarifa mpya.

Kuna aina tatu za usambamba:

- Mstari unaosema kitu kile kile kwa namna mbili tofauti (Zaburi 25:4, Zaburi 103:10, Mithali 12:28).
- Mstari unaoonesha utofauti baina ya vitu viwili (Zaburi 37:21, Mithali 10:1, 7).

- Mstari unaotoa tamko kisha unaongeza taarifa zaidi katika sentensi inayofuata (Zaburi 14:2, Zaburi 23:1, Mithali 4:23).

Tunapotafsiri usambamba, tunauliza mstari wa pili unaongeza nini katika mstari wa kwanza. Je, unajenga mtari wa kwanza, je, unatoa ukinzani kwa mstari wa kwanza, au je unongeza taarifa mpya?

### *Tamathali za Semi*

Wakati vitabu vyote vya Biblia vinajumuisha tamathali za semi, hizi ni maaluhusi sana katika mashairi. Tamathali za semi zinazopatikana katika mashairi ya Kiebrania zinajumuisha:

1. Ulinganifu wa vitu viwili ambavyo vinafanana kwa namna fulani: "BWANA ndiye mchungaji wangu" (Zaburi 23:1).
2. Kutumia mubaraga ili kusisitiza jambo. Daudi anaelezea uchungu wake namna hii: "Kila usiku nakieleza kitanda changu...kwa machozi yangu" (Zaburi 6:6).
3. Kukizungumzia kitu kana kwamba ni mwanadamu: "Hekima hupaza sauti yake katika njia kuu, Hutoa sauti yake katika viwanja" (Mithali 1:20).
4. Kumuelezea Mungu kwa kutumia sifa za mwanadamu: "Macho (ya Mungu)... yanaangalia; Kope zake zinawajaribu wanadamu" (Zaburi 11:4).

Unapotafsiri tamathali za semi, uliza taswira inayoonesha ambayo tusingeielewa endapo katika maelezo ya kawaida. Kwa mfano, "BWANA ndiye mchungaji wangu" ni zaidi ya "Mungu ananijali mimi." Inazungumzia kujali, lakini pia inazungumzia upendo, uongozi wake, ulinzi wake kutoka kwa adui zetu, na nidhamu wakati tunatanga mbali na kujali kwake.

## Kitabu cha Zaburi

### *Aina za Zaburi*

Zipo aina kadhaa za Zaburi. Zaburi za sifa zinamheshimu Mungu kwa sifa, baraka, na kuingilia kati kwakwe (Zaburi 23, 29). Zaburi kuhusiana na sharia za Mungu zinamsifu Mungu kwa hekima na haki yake (Zaburi 119). Zaburi za huzuni zinaonesha hisia kwa Mungu, zikimuuliza msaada wake, na mzaburi kujitoa kwa mapenzi ya Mungu (Zaburi 3, 13, 22). Zaburi kuhusiana na mfalme zinaelezea baraka ambazo zinakuja kwa taifa kupitia mfalme anayemcha Mungu, na Zaburi hizo pia zinaelekeza kwenye ufalme ujao wa kimasihi (Zaburi 21, 72). Zaburi za hasira zinamuita Mungu kuamua kwa haki watu waovu na kuwatetea watumishi wake (Zaburi 69:21-28, Zaburi 59). Aina nyingine ya Zaburi zinaweza kuorodheshwa.

### *Matumizi ya kitabu cha Zaburi*

Agano Jipya linatueleza sisi zaidi kuhusiana na Zaburi. Zaburi zinaelezea ibaada yetu kwa Mungu (Waefeso 5:19). Pia ni zinatummika kwa mafundisho na kutia moyo (Wakolosai 3:16).

Si kila mtazamo unaooneshwa na Zaburi ni mfano wa mtazamo tunaotakiwa kuwa nao. Hata hivyo, tunajifunza kutoka kwa Zaburi kwamba kila mtazamo unatakiwa kujitiisha kwa Mungu. Katika maombi, unaweza kumuelezea Mungu hisia zozote ulizonazo. Zaburi zinatuonesha kwamba Mungu anaweza kufanya upya imani ya mwamini ambaye anasumbuka na kuvunjwa moyo, hofu, na hasira.

## Aina ya Fasihi: Mashairi yenye Hekima

Ayubu, Mithali, Mhubiri, na sehemu za Zaburi na Yakobo zinawasilisha kundi linalojulikana kama Mshairi yenye hekima. Katika kitabu cha Mithali na Mhubiri, maelekezo yanaelekezwa kwa wasomaji Vijana ambao wanajifunza kanuni za maisha.

### Kitabu cha Ayubu

Vifungu virefu katika Ayubu vinatoa maneno ya wazungumzaji mbalimbali wa kibinadamu, wakiwemo Ayubu mwenyewe. Wazungumzaji wanaonesha mawazo tofauti tofauti. Mtafsiri wa Biblia hatakiwi kuchukulia maelezo kutoka katika mazungumzo ya wanadamu na kuyafundisha kama kanuni za kibiblia. Kitabu cha Ayubu kinachanganua kwa undani maelezo hayo na maneno na mtazamo wa Mungu. Katika Ayubu 38-42 Mungu anajibu mazungumzo, na Ayubu 1-2 pia inaonesha mtazamo wa Mungu.

### Aina ya Fasihi: Mithali

Mithali ni Uchunguzi wa maisha ambao unatajwa kwa ufupi na kwa wazi. Zinataja kile ambacho mara nyingi kunatokea, lakini hazimaanishi kwamba hakutakuwa na mambo yasiyo ya kawaida/mambo ya kipekee.

Kwa juu juu, mithali ni rahisi kutafsiri. Hata hivyo, aina hii ya fasihi inaleta changamoto mahususi. Mithali inataja kanuni ya jumla kuhusiana na maisha, lakini kanuni hizi hazifanyi kazi katika kila mazingira. Kwa mfano, Mithali 21:17 inasema,

> Mtu apendaye anasa atakuwa maskini; Apendaye mvinyo na mafuta hatakuwa tajiri.

Kama kanuni ya msingi, wale wanaopenda anasa kuliko kufanya kazi watakuwa masikini. Hii kanuni ya jumla ni kweli, lakini ina mambo mengi ya kipekee yasiyo ya kawaida. Baadhi ya matajiri wamerithi utajiri wao pasipo kufanya kazi. Wanatumia siku zao kunywa na kucheza, lakini ni matajiri. Watu wengine wanafanya kazi kwa bidii na wanabaki masikini. Mithali inafundisha kanuni ya jumla, lakini si kanuni kuu.

Kuna Mithali nyingi kwenye Biblia, si tu katika kitabu cha Mithali. Hapa ni mfano wa Mithali iliyosemwa na Yesu: "…wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga" (Mathayo 26:52). Wapo watu wakorofi ambao hawakufa kwa ghasia. Tena, Mithali ni kweli kwa

sababu ni uchunguzi wa jumla, lakini yanaweza kuwepo mambo yasiyo ya kawaida au ya kipekee.

Tunapaswa kuuliza maswali haya tunapotafsiri mithali:

**(1) Ni kanuni gani za jumla zinazofundishwa katika andiko hili?**

Kanuni inayopatikana katika Mithali 21:17 ni thamani ya kufanya kazi kwa bidi na nidhamu. Mithali nyingi zinafupisha kanuni ambayo inaweza kutengenezwa katika kifungu kimoja cha maneno.

**(2) Je, ni hali gani za zisizo za kawaida zinazoweza kutokea katika kanuni hii?**

Kuhusiana na Mithali 21:17, tunaona mambo yasiyo ya kawaida katika maisha ya kila siku; inaonesha tu kwamba mtu mwenye busara anatakiwa kutambua kwamba kuna mambo yasiyo ya kawaida kwa kila kanuni ya jumla.

**(3) Ni watu gani katika Biblia ni kielelezo cha kanuni hii?**

Unapotafsiri mithali, ni msaada mkubwa sana kumtafuta muhusika katika Biblia ambaye anatoa kielelezo cha kanuni ya mithali. Kwa mfano, Mithali inasema, "Kijapo kiburi ndipo ijapo aibu; Bali hekima hukaa na wanyenyekevu" (Mithali 11:2). Kiburi cha Sauli na unyenyekevu wa Daudi wa kukiri dhambi unaonesha namna mithali hii inafanya kazi katika maisha halisi.

**Kitabu cha Mithali**

Sehemu kubwa ya kitabu cha Mithali kiliandikwa na Sulemani. Kusudi lililotamkwa la kitabu ni kumsaidia mtu ambaye hajakua kupata hekima na kumsaidia mwenye hekima kuwa na hekima zaidi (Mithali 1:4-5).

Kitabu cha Mithali kinazungumza kuhusiana na aina tatu za watu. **Mjinga** amekua na kuwa mtu mzima lakini bado hajapata uzoefu na uelewa wa maisha. Mtu wa kawaida anatakiwa kupata hekima na kuepuka makossa ambayo yatamuharibu.

**Mwenye hekima** ni yule anaye elewa namna ya kuishi sawasawa na kanuni za Mungu. Ni lazima watu wamuhofu Mungu kama wanataka kuwa wenye hekima (Mithali 9:10). Wenye hekima huendelea kujifunza.

**Mpumbavu** amekataa hekiama (kanuni za Mungu) na amekataa kusikiliza. Anaonesha tabia mbaya na anateseka kwa kufanya maamuzi mabovu. Siyo kwamba mpumbavu hana akili, bali hayaelewi maisha kwa sababu amekataa maongozi ya Mungu.

Baadhi ya dhana kuu katika kitabu cha Mithali ni (1) hatari ya uvivu na thamani ya kazi (2) majanga yanayotokea kutokana na uasherati na uzinsi, na (3) maadili katika aina mbalimbali za mahusiano.

**Kitabu cha Mhubiri**

Kitabu cha Mhubiri kiliandikwa na Sulemani (Mhubiri 1:1).

Ujumbe wa Mhubiri: **kama** tu maisha haya yapo, hakuna haki au kusudi katika maisha au mfanikio yeyote makubwa.

Mhubiri anaelezea kwa nini maisha ya duniani hayawezi kuwapa watu utoshelevu au kusudi. Katika maisha haya:

- Haki imepuuzwa.
- Kila mtu anakufa na anasahaulika.
- Waovu hufanikiwa.
- Hekima ina nguvu lakini imedharauliwa.
- Hekima na maarifa yanaongeza huzuni.

Mhubiri anatuonesha kwamba maisha ya mtu anayeishi maisha akiwa na mtazamo wa umilele atakuwa:

- Mwenye furaha lakini akiwa makini na mambo ya maisha.
- Kumbuka kwamba kifo kinakuja.
- Atafurahia mambo mema lakini akikumbuka kuwa anawajibika kwa Mungu.
- Hataruhusu lengo lolote la kidunia kuwa la muhimu zaidi.

Sulemani alifikia hitimisho hili: Kwa sababu kuna hukumu, mtumikie Mungu na ushike amri zake tangu ujana.

**Aina ya Fasihi: Unabii wa Agano la Kale**

Vitabu vya manabii wa Agano la Kale ni mkusanyiko ulioandikwa wa jumbe zilizo hubiriwa. Manabii 16 wana jumbe zilizorekodiwa katika maandiko. Ni Yeremia tu ndiye ana vitabu viwili. Baadhi ya manabii waliandika vitabu ambavyo haviko katika maandiko (1 Mambo ya Nyakati 29:29). Tunaelezwa kwamba wapo mamia ya manabii ambao hawakuandika chochote.

Manabii 16 walioandika walihudumu kati ya miaka ya 760-460 K.K. (Israeli ilianguka mwaka 722. Yuda ilianguka mwaka 587.) Katika kipindi hiki, kuinuka na kuangujka kwa dola mbali mbali za ulimwengu kulikuwa na mchango kwa Israeli kisiasa, kiuchumi, na kidini. Kuna wakati, wengi wa watu wa mataifa ya Yuda na Israeli walivunja agano lao na Mungu na kutumiakia miungu.

Manabii walikuwa watetezi wa agano la Mungu. Waliwakumbusha watu matakwa ya Mungu. Miaka kadhaa kabla, Mungu aliahidi Israeli kwamba Israeli wangepokea baraka au laana kwa kutegemea utii wao kwake (Mambo ya Walawi 26, Kumbukumbu la Torati 28-32). Manabii walitabiri kutimilika kwa ahadi hizo. Baraka zilizoahidiwa katika utii ni pamoja na uhai, afya, mafanikio, utele katika kilimo, uhuru, na usalama. Laana kwa kutotii ni pamoja

na mauti, magonjwa, ukame, njaa, kuvunjika kwa familia na miji, kushindwa vitani, uhamisho toka nchini kwao, kupoteza uhuru, umasikini, na aibu.

**Unabii ulikuwa ni mawasiliano ya ujumbe toka kwa Mungu**. Unabii ulikuwa ni mahubiri, yakishughulikia jambo lililoppo na yalihitaji mwitikio wa haraka. Ujumbe wa manabii mara nyingi ulijumuisha na utabiri. Hata hivyo, nabii alikuwa mhubiri. Ujumbe wake ulikuwa wa kinabii ama alikuwa anatabiri au la.

Katika namna nyingi, hatujui ni kwa namna gani au lini utabiri uliokuwa ndani ya unabii ulitimilika. Ufahamu huo hauhitajiki sana kwa sisi kujifunza kutoka katika vifungu hivyo. Mara nyingi, utimilifu haukutokea ndani ya maisha ya nabii na wasikilizaji wake, lakini ujumbe huo ulihubiriwa kwa ajili matumizi na mwitikio wa haraka. Nabii alionesha ufalme wa Mungu unaokuja kama sababu ya watu kutubu na kumtii Mungu katika wakati uliopo (Habakuki 2:14).

Njia za manabii kuwasiliana na kuelezea mara nyingi zilikuwa si za kawaida na zenye lugha ya picha. Jumbe zao zilikuwa za kitamathali na mara nyingine zilijumuisha maonesho ya kawaida ya kimwili. **Hata hivyo, hawakuhubiri kwamba watu wafanye jambo fulani jipya au lisilo la kawaida, bali kwamba wanatakiwa kutii sheria za Mungu zilizofunuliwa.**

Mahubiri ya manabii, ambayo yalikuwa ni ili kuwaleta watu tena katika matakwa ya agano (mahusiano yao na Mungu), yanaweza kuhubiriwa leo na kuwaleta watu katika matakwa ya mahusiano yetu na Mungu.

Utabiri (hata wa yale matukio ambayo yatatokea mbeleni kabisa) yalikusudiwa kuwa na matokeo ya karibu. Watu waliitwa ili kutubu na kumtii Mungu. Kusudi hili linafanana na kusudi la mahubiri ya leo.

Baadhi ya utabiri ulikuwa na masharti. Wasikilizaji wangeepuka hukumu iliyotabiriwa kwa kutubu (Yeremia 18:7-11, Yeremia 26:13-19). Wasikilizaji wa Yona katika Ninawi waliepuka uharibifu hata kama ujumbe wa Yona haukutoa rehema (Yona 3:4-5, 9-10).

Utimilifu wa kusudi la Mungu hauna masharti; kwa mfano, katika Isaya 43:5-6 ahadi ya Mungu kwamba atawarejesha mateka tena kurudi Israeli kwa nguvu zake, lakini kifungu hakitoi masharti ambayo ni lazima kutimizwa na Israeli. bado, nafasi ya mtu katika matukuio haya yapo katika masharti ya uchaguzi wa mtu husika.

Vitabu vya unabii vina vifungu vya simulizi za kihistoria, lakini mara nyingi zikiwa katika muundo wa ushairi. Sio ngumu kutofautisha simulizi ya kihistoria ambayo ni lazima itafsiriwe kama lugha ya kawaida tofauti na vifungu vya ushairi ambavyo vinajumuisha alama.

**Maneno Muhimu na Dhana katika Manabii**

**Ibada ya sanamu**: Uvunjaji mkuu wa agano.

**Uzinzi**: Dhambi ambayo mara nyingi iliambatana na ibada ya sanamu na ilitumika kitamathali kurejelea ibada ya sanamu.

**Mataifa**: Inarejelea ulimwengu ambao haukuwepo katika agano la mahusiano na Mungu. Dhana mbili ndogo:

1. Mara nyingi mataifa walikuwa na chuki na Israeli.
2. Mungu alikusudia Israeli wamtukuze yeye kati ya mataifa.

**Hekalu**: Kituo kikuu cha uwepo wa Mungu. Dhana mbili ndogo:

1. Ibada ya kinafiki haikumuheshimu Mungu.
2. Maadui kuvamia kwa hekalu ilionesha kushindwa vibaya kwa Israeli na kupoteza uwepo wa Mungu.

**Nchi/Urithi**: Sehemu maalumu ambayo Mungu aliwaweka Waisraeli ili wabarikiwe.

**Utumwa:** Kutolewa katika sehemu aliyowapa Mungu, na kutumikishwa na mataifa mengine. Utumwa ulimaanisha kwamba Israeli wamepoteza Baraka za Mungu.

**Mvua (na maneno yanayohusiana)**: Alama ya baraka endelevu za Mungu katika nchi ambazo aliwapa Waisraeli. Kukosekana kwa mvua kulizungumzia kutokukubalika na Mungu.

**Mavuno (na maneno yanayohusiana)**: Baraka za Mungu zinahusiana na dhana ya mvua na nchi.

**Siku ya Bwana**: Hukumu ya ghafla ya Mungu ya mbeleni ambayo itawaharibu waovu. Israeli walifikiri kwamba hukumu ni kwa ajili ya mataifa na waliogopa sana kusikia kwamba watahukumiwa pia.

**Farasi**: Waliwakilisha nguvu ya kijeshi.

**Kukombolewa kutoka Misri**: Tukio la kihistoria ambalo liliwafanya Israeli kama taifa kumfanya Mungu mfalme wao. Kuabudu sanamu kulikuwa ni kukosa heshima kwa agano lililofanyika baada ya ukombozi.

**Kutafsiri Fasihi ya Unabii**

Fasihi ya unabii ni moja kati ya fasihi ngumu kutafsiri. Ili kutafsiri unabii kwa ufanisi, uliza maswali haya:

### (1) Nabii alisema nini kwa ulimwengu wake?

Tofauti kabisa na mawazo ya watu wengi, fasihi ya unabii si kuhusu utabiri wa mbeleni pekee. Nabii alizungumza kwanza na ulimwengu wake.

Kwa mfano, Amosi aliandikwa kwa taifa la Israeli, ambalo lilikuwa linamuasi Mungu. Watu walikuwa wanafanikiwa na walifikiri wanaweza kupuuza sheria ya Mungu pasipo matokeo. Amosi alitangaza ujumbe wa hukumu: Israeli watahukumiwa kwa sababu wameacha haki na hukumu ya haki (Amosi 5:7).

**(2) Watu wake waliitikiaje ujumbe wake?**

Mwitikio wa Israeli kwa ujumbe wa Amosi unaonekana katika mwitikio wa Amazia, kuhani mkuu huko Betheli. Alimtaka Amosi kurudi Yuda na asihubiri tena katika ufalme wa kaskazini (Amosi 7:10-13).

**(3) Ni kanuni gani kutoka katika ujumbe wa nabii inayozungumza katika ulimwengu wetu leo?**

Kama ambavyo haki na hukumu ya haki ni viwango vya Mungu katika Israeli ya kale, Mungu anataka haki na hukumu ya haki kutoka kwa watu wake leo. Hatuwezi kumuabudu Mungu katika nyumba ya Mungu huku tukipuuza wito wake wa maisha ya haki (Amosi 5:22-24).

Maswali haya yataleta kweli ya unabii kutoka kwenye ulimwengu wa nabii hadi kwenye ulimwengu wetu. Kwa kuangalia ulimwengu wa nabii, tunahakikisha kwamba tafsiri yetu ina mizizi katika ujumbe wa asili.

## Aina ya Fasihi: Fasihi ya Kiapokaliptiki

Maandiko ya kiapokaliptiki inajumuisha Danieli, Zekaria, Yoeli, Ufunuo, na vifungu kadhaa kutoka katika vitabu vingine vya Biblia.

Mwandishi wa kitabu cha apokaliptiki alipokea ujumbe katika maono au ndoto. Imejaa alama nyingi. Mara nyingi hutumia wanyama, au hata wanyama wa kutisha wa ajabu kama alama.

Badala ya kuelezea matukio katika mpangilio wa muda, maandishi yanaweza kuwa yanarudia rudia matukio/mazingira yale yale, maelezo ya tofauti yakitolewa katika kila maelezo.

Kanuni ya kawaida ya kutafsiri maandiko ni kuichukulia kawaida hadi pale inapoonekana kwamba mwandishi alikusudia kutumia lugha ya tamathali. Kwa habari ya fasihi ya kiapokaliptiki, mtafsiri anatakiwa kutambua kwamba mwandishi alikusudia taarifa zake nyingi kuwa za tamathali. Mifano ya maelezo ya tamathali zinaweza kuwa wale wanyama na mnyama wa kutisha katika maono ya Danieli.

- Mifano ya alama za wanyama: Danieli 7:3-7, Ufunuo 12:3, Ufunuo 16:13, na Zekaria 6:1-3.

Maandiko ya kiapokaliptiki mara nyingi yanatoa changamoto ya kuitunza imani licha ya maovu na ukosefu wa haki katika ulimwengu wa sasa. Inaelezea mapambano makuu yakiwa na vita kali.

Maandiko ya Kiapokaliptiki katika Biblia yanaonesha ushindi mkuu wa Mungu, ambaye uhukumu maovu na kuzawadia mema. Kiini kikuu ni Mungu Mwenyezi ambaye anakuja kuwasaidia watu wake.

Ujumbe wa msingi wa maandiko ya kiapokaliptiki yanaweza kueleweka hata kama alama zote hazieleweki na hata kama mtafsiri hawezi kuweka mstari wa muda wa matukio ya kinabii.

- Mifano ya vifungu vinavyoelezea vita kuu: Yoeli 2:9-11, Ufunuo 19:11-21, na Ufunuo 20:7-9.
- Mifano ya vifungu vinavyofundisha ushindi wa mwisho na ufalme wa milele wa Mungu: Danieli 7:14, 27 na Zekaria 14:9.

Pamoja na vitabu vya kiapokaliptiki, sehemu nyingine za maandiko zinaweza kuwa za kiapokaliptiki kwa sababu zinazungumza kuhusu Mungu kuingilia kati kwa haraka wakati anahukumu nguvu ya uovu na kuwaokoa wenye haki. Si Maandiko haya yote yana tabia nyingine za maandiko ya kiapokaliptiki, kama vile alama za maono, wanyama. (Mifano ni Ezekieli 37-39, Isaya 24-27, Mathayo 24, Marko 13, Luka 21, 2 Wathesalonike 2, and 2 Petro 3.)

**Matumizi ya Jumla ya Maandiko ya Kiapokaliptiki**

Suluhisho kuu la uliwmengu huu si maendeleo ya kitamaduni au kijamii. Sio mageuzi ya kisiasa au mapinduzi. Suluhisho ni Mungu kuingilia kati. Kwa sasa anatupa imani, nguvu, na huruma kwa watu wake. Mbeleni atakuja kwa ghafla na kuubadilisha ulimwengu kikamilifu.

Waamini wanatakiwa kuwa wavumilivu katika imani. Uelewa uliokamilika wa sasa wa mpango wa Mungu au matukio katika ulimwengu si muhimu sana. Kuwa na imani haimaanishi kwamba watu wanaweza kubashiri matokeo fulani ya karibuni. Badala yake, watu wenye imani halisi wanamtii Mungu katika hali zote, kwa sababu wanafahamu kwamba mwishowe utii unathamani.

## Aina ya Fasihi: Mfano

Mfano ni nyenzo ya kufundishia ambayo inalinganisha ukweli wa kiroho na vitu katika asili au hali halisi za maisha. Mfanano kati ya kiroho na kiasili unaoneshwa ili kwamba tuelewe vizuri kweli ya kiroho.

Kutoa mifano ilikuwa ni njia mojawapo aliyoipendelea Yesu kama njia yake ya kufundishia (Mathayo 13:34). Alitoa mifano 30 na anatumia mifanano ya tamathali.

Kupitia mifano, Yesu alifundisha maombi (Farisayo na Mtoza ushuru hekaruni, Luka 18:9-14), upendo kwa majirani zetu (msamaria mwema, Luka 10:29-37), asili ya ufalme wa Mungu (mifano katika Mathayo 13), na huruma za Mungu kwa wenye dhambi (mwana mpotevu, Luka 15:11-32).

Mifano ilimruhusu Yesu kuwakemea wasikilizaji wake bila kukabiliana nao moja kwa moja. Kwa sababu mifano ya Yesu iliyotolewa ilikuwa inavutia sana, ilifungua masikio ya wasikilizaji wa Yesu kwa maneno yake hadi pale ambapo walishtuka na kutambua

“Ananiongelea mimi!” Nathani nabii alifanya vivyo hivyo alipomwambia Daudi mfano wa masikini mwenye kondoo mmoja (2 Samweli 12:1-10). Ni hadi Nathani aliposema, “Wewe ndiwe mtu huyo,” ndipo Daudi alitambua kwamba mfano ulikuwa unamuhusu yeye mwenyewe.

**Kutafsiri Mfano**

Mtafsiri anatakiwa kuwa makini na:

- Ni kwa namna gani mfano ulitolewa?
- Hitimisho la mfano lilikuwa ni nini?
- Ni mwitikio gani au mabadiliko gani ya mtazamo ambayo mfano unatoa?
- Wapokeaji wa kwanza walikuwa na mwitikio gani?

**(1) Ni kwa namna gani mfano ulitolewa?**

Mara nyingi Yesu alitoa mfano akiwa anajibu swali au mtazamo. Kufahamu mazingira ambayo mfano ulitolewa inamsaidia mtafsiri kuuelewa ujumbe.

Kama tafsiri yetu ya mfano haiendani moja kwa moja na mazungumzo au hali ambayo ilipelekea Yesu kuutoa mfano, tutakuwa tumekosa jambo muhimu.

**Mifano ili Kujibu Swali**. Wakati wa mazungumzo, mwanasheria alimuuliza Yesu, “jirani yangu ni nani?” Yesu angeweza kujibu, “Mwenye huhitaji katika njia yako ni jirani yako-na wajibu wako.” Badala yake, Yesu anatoa jibu lile lile kwa namna tofauti, kwa kutoa mfano wa msamaria mwema.

Agustino alikosea kutafsiri mfano kwa sababu alipuuza swali ambalo mfano ulikuwa unalijibu. Hii ndiyo tafsiri ambayo Agustino alitoa: Yesu (msamaria) alimwokoa Adamu (mtu) kutoka kwa Shetani (wanyang’anyi) na akampeleka kanisani (nyumba ya kulala wageni) kwa ajili ya ulinzi. Yesu alimlipa Paulo (mtunza nyumba ya wageni) dinari mbili (ahadi ya maisha ya sasa na yajayo) ya kushinda dhambi (vidonda). Tafsiri ya Agustino haikuwa sahihi kwa sababu haikuwa inahusiana na mazungumzo baina ya Yesu na mwanasheria.

**Mfano ili kujibu mtazamo.** Luka 15:1-3 inasema, “Basi watoza ushuru wote na wenye dhambi walikuwa wakimkaribia wamsikilize. Mafarisayo na waandishi wakanung’unika, wakisema, Mtu huyu huwakaribisha wenye dhambi, tena hula nao. Akawaambia mfano huu, akisema”:

- Mchungaji alikuwa na kondoo aliyepotea. Angalia furaha yake kondoo aliyepotea alipopatikana!

- Mwanamke alipoteza shilingi moja. Angalia furaha yake alipoipata shilingi iliyopotea.

- Baba aliyekuwa na mtoto mpotevu. Angalia furaha yake mtoto wake alipopatikana.

Kupitia mifano hii mitatu, Yesu alionesha, "Hautakiwi kupata mshituko kwamba ninakula na wenye dhambi. Angalia furaha kubwa mbinguni mwenye dhambi mmoja kitubu!"

Ni muhimu sana kukumbuka kwamba **somo la msingi la mfano litahusiana moja kwa moja na swali ambalo limepelekea mfano kutolewa.**

**(2) Hitimisho la mfano lilikuwa ni nini? Ni mwitikio gani au mabadiliko gani ya mtazamo ambayo mfano unatoa?**

Mara nyingi mfano unatoa dondoo kuu moja; ingawaje matumizi yanaweza kuwa mengi. Kila muhusika mkuu katika mfano anaweza kuwa anafundisha somo.

Tumekwisha kuangalia somo la msingi la mfano wa mwana mpotevu: Kuna furaha kubwa mbinguni mwenye dhambi mmoja akitubu. Dondoo hii kuu inajibu mazingira ambayo yalipelekea Yesu kutoa mfano: Mafarisayo hawakuwa tayari kuwasamehe wenye dhambi. Wahusika wote watatu, kila mmoja anafundisha somo moja ambalo linahusiana na dondoo kuu ya mfano moja kwa moja.

| Muhusika | Somo |
|---|---|
| **Mwana Mpotevu** | Wenye Dhambi ambao wanamgeukia Mungu katika toba na wanaupata msamaha ulio tayari kwa ajili yao. |
| **Baba Mwenye Upendo** | Badala ya kutokuwa tayari kusamehe, Baba yetu wa mbinguni anafurahia msamaha. |
| **Kaka Mkubwa** | Mtu asiyesamehe hana upendo kama alio nao Baba. |

Yesu alionesha ukinzani kati ya kutosamehe kwa kaka mkubwa na kusamehe kwa baba. Kusudi la Yesu lilikuwa kukemea kutosamehe kwa Mafarisayo. Aliwataka wao kutubu kutokana na mtazamo wao usio sahihi.

Mtu anayehubiri kutoka katika mfano huu anaweza kusisitiza upendo na msamaha wa baba kwa kusudi la kumtia moyo mwenye dhambi kutubu. Au anaweza kuhubiri kwamba waamini wanatakiwa kuwa na mtazamo wa Mungu wa kusamehe wasioamini.

**(3) Wapokeaji wa kwanza walikuwa na mwitikio gani?**

Ili kuelewa ni namna gani mfano ulikuwa na matokeo kwa wapokeaji wa kwanza, ni lazima tuelewe utamaduni wao. Mifano ya Yesu mara nyingi ilienda kinyume na utamaduni uliozoeleka. Hii iliwafanya wao kushangaa.

Kwa mfano, zingatia tena mfano wa mwana mpotevu. Wapokeaji wa Yesu wangeliona kuwa ni kukosa heshima kwa hali ya juu kwa mtoto kuomba urithi mapema. Kisha mtoto akaupoteza urithi. Wasikilizaji walifikiri kwamba wakati anarudi, baba yake angemkataa,

angekataa kumuona, na labda hata angempiga na kumfukuza. Fikiria mshangao walioupata wasikilizaji wakati ambapo baba alikikibia ili kumkaribisha mtoto wake.

Katika mfano wa Msamaria mwema, wasikilizaji hawakushangaa kwamba Kuhani na Mlawi walimpita aliyejeruhiwa pasipo kumsaidia, kwa sababu waliwaona viongozi wa hekalu kuwa wameharibika na wanafiki. Waliwaheshimu Mafarisayo, na walifikiri ambaye angekuwa mtu wa tatu kumsaidia aliyejeruhiwa angekuwa Farisayo. Hebu fikiria kuhusu mshangao wao kwamba mtu wa tatu ni Msamaria, mtu ambaye walifikiri amedharauliwa kwa ajili ya tabaka lake na kukosa hali ya kidini.

Kwa kadiri unavyoelewa vizuri mazingira ya kiutamaduni ya mfano, ndivyo utakavyoelewa vema ujumbe.

**Taarifa za Kina na Alama Katika Mifano**

Baadhi ya wahubiri kwa makosa wanafikiri kwamba kila kipengere katika kila mfano ni lugha ya alama. Kwa mfano, katika mfano wa Msamaria mwema baadhi ya watu wamesema kwamba msafiri aliposhuka kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko, alikuwa akifanya uamuzi mbaya kwa sababu alikuwa akienda katika jiji ambalo Mungu amelilaani. Hii si tafsiri nzuri ya mfano huo, kwa sababu kusudi la mfano huo lilikuwa kueleza jinsi mtu anavyoonyesha upendo kwa jirani. Maelezo mengine ni maelezeo na sio ishara ya chochote.

Katika mfano wa Marko 4:30-32, wahubiri wametafakari juu ya kile ambacho ndege kwenye mti wanawakilisha, lakini ndege wanatajwa tu ili kuelezea namna ambavyo mbegu ndogo ilikua na kuwa kitu kikubwa ambapo ndege wangekuja na kuketi kwenye matawi.

Katika mfano wa mwana mpotevu hakuna sababu ya kujaribu kupata maana ya mfano kwa ajili ya kila taarifa. Kwa mfano, nguruwe sio ishara. Nguruwe wanatajwa kuonyesha hali mbaya ya mwana mpotevu: Mvulana wa Kiyahudi kwa kawaida asingeweza kuwa karibu na nguruwe.

Ni nadra kwa maelezo ya mifano kuwa ya kiishara. Mfano mmoja wa maelezo ya alama katika mfano ni katika mfano wa ngano na magugu (Mathayo 13:38-39). Tunajua kwamba maelezo katika mfano huu yalikuwa ni alama kwa sababu Yesu alisema yalikuwa hivyo.

**Kuhubiri kwa Mifano**

Muhubiri anaweza kutumia mfano ili kuutumia kwa namna inayoeleweka katika utamaduni wake. Hata hivyo, anatakiwa kuchukua muda kuelewa nini ambacho mfano unamaanisha kwa wasikilizaji wa kwanza. Vinginevyo, hatawasilisha ujumbe ule ule kwa wasikilizaji.

Mtafsiri hatakiwi kutumia mfano kama msingi wa kanuni ya imani au matumizi ambayo hayaungwi mkono na maandiko mwengine yaliyo wazi.

## Aina ya Fasihi: Waraka

### Sifa za Nyaraka[24]

Vitabu vingi vya Agano Jipya ni nyaraka kutoka kwa Paulo, Yakobo, Petro, Yohana, na Yuda. Wakati zipo tofauti kati ya nyaraka, baadhi ya sifa ni sawa kwa nyaraka. Nyaraka za Agano Jipya ni:

1. **Zenye Mamlaka.** Nyaraka za Agano Jipya zilikuwa ni mbadala wa uwepo wa mwandishi. Waraka ulionesha mamlaka ya mwandishi; mamlaka hayo mara nyingi yalioneshwa katika mistari ya ufunguzi.[25]

2. **Za Kimazingira.** Nyaraka za Agano Jipya mara nyingi zilielekezwa katika hali mahususi au tatizo mahususi. Kwa mfano, Wagalatia iliandikwa kwa kanisa ambalo linafikiri wokovu unategemea kufuata matakwa ya Wayahudi. Paulo anasisitiza uhuru wetu katika Kristo. Kinyume chake, kanisa la Korintho lilichukua uhuru huo kupita kiasi—kuvumilia uasherati. Katika 1 Wakorintho, Paulo anasisitiza wajibu wetu wa utii.

3. **Zilielekezwa kwa Waamini.** Nyaraka ziliandikwa kwa makanisa ya majimbo (Warumi) au kwa waamini binafsi (Filemoni) au kwa waamini kwa ujumla (Yuda). Si kila wapokeaji wa nyaraka walikuwa wanaishi katika mahusiano mazuri na Mungu. Paulo aliwaita waamini wa kanisa la Korintho kutubia baadhi ya matendo yao; aliwaita Wagalatia kurudi kwenye Injili, na Yakobo anawaambia matajiri wasio wenye haki kutegemea hukumu. Hata hivyo, nyaraka ziliandikwa katika muktadha familia ya imani ya kikristo.

---

[24] Dhana katika sehemu hii zimechukuliwa kutoka katika J. Scott Duvall na J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012).

[25] Kwa mfano, Waefeso 1:1 inataja Mamlaka ya kitume ya Paulo: "Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu."

| Muundo wa Nyaraka za Agano Jipya |
| --- |
| Utangulizi<br>• Jina la mwandishi na nafasi<br>• Wapokeaji<br>• Salamu<br>• Maombi ya Utangulizi<br>Sehemu kuu (Ujumbe wa msingi wa waraka)<br>Hitmisho (inahusisha nyenzo kama)<br>• Mipango wa safari (Tito 3:12)<br>• Pongezi na salamu (Warumi 16)<br>• Maelekezo ya mwisho (Wakolosai 4:16-17)<br>• Baraka (Waefeso 6:23-24)<br>• Doksolojia (Yuda 24-25) |

**Kutafsiri Nyaraka**

Unapopokea barua kutoka kwa rafiki, unaketi chini na kusoma barua yote. Soma nyaraka za Agano Jipya kwa namna hiyo hiyo. Soma waraka wote ili kupata muhtasari ya ujumbe wa mwandishi. Unaposoma, tengeneza orodha ya Uchunguzi. Kwa kadiri unavyochunguza kwa kina, unakuwa umeandaliwa vema ili kutafsiri waraka.

Kuna maswali kadhaa ya kuuliza unaposoma waraka katika Biblia:

**(1) Nani ni wapokeaji wa waraka?**

Kwa kadiri tunavyofahamu zaidi kuhusiana na kanisa au mtu anayepokea waraka, tutaelewa vizuri zaidi waraka huo. Tunaposoma nyaraka za Paulo, itakuwa na msaada sana endapo unatosoma rejea yake katika Matendo ya Mitume kwa kanisa linalopokea. Mara nyingi hii itatoa uelewa mzuri zaido wa waraka. Kwa mfano:

- Kanisa la Filipi lilizaliwa katika mateso (Matendo ya Mitume 16:12-40). Hii inaonesha maelekezo ya Paulo kwamba wanapaswa kufurahi hata katika nyakati ngumu.

- Waefeso (kama nyaraka nyingine za Paulo) iliandikwa kwa waamini. Wakati Paulo anaomba kwamba waamini wa Efeso wapate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu, (Waefeso 3:19) anaomba kwamba watoto wa Mungu wapokee hata zaidi ya utimilifu wa kimungu. Anaomba kwamba wakristo wafanywe “watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake” (Waefeso 1:4).

**(2) Nani ni mwandishi? Anahusianaje na wapokeaji?**

Unapo pokea barua katika barua pepe, unataka kufahamu: “Nani ameandika hii?” Kwa kadiri unavyomfahamu vizuri mwandishi, ndivyo barua itakavyovutia. Kwa namna hiyo hiyo,

kwa kadiri tunavyomfahamu mwandishi wa waraka wa Biblia, ndivyo tutaelewa vizuri ujumbe wake.

Katika nyaraka zake, mtume Yohana amesisitiza upendo. Yohana mwanzo alijulikana kama mmoja wapo wa "wana wa ngurumo" (Marko 3:17). Huko nyuma, yeye na ndugu yake walimuuliza Yesu awape ruhusa ya kuita moto kutoka mbinguni (Luka 9:54). Nyaraka za Yohana, ziliandikwa baade, zinatuonesha sisi kwamba yeye (Yohana) amebadilishwa sana na ujazo wa Roho Mtakatifu siku ya pentekoste.

Petro aliandika waraka wake kuwatia moyo wakristo walikuwa wanateseka. Aliwahakikishia kwamba wanaweza kuwa jasiri hata katika mashambulizi ya Shetani (1 Petro 5:8-9). Mwanzoni mwa maisha ya Petro, alikana kwamba anamjua Yesu kwa sabau ya hofu (Marko 14:66-72). Nyaraka za Petro zinatuonesha sisi badiliko ambalo lilitokea katika maisha yake.

Kufahamu mahusiano baina ya mwandishi na wapokeaji mara nyingi ni msaada sana katika kusoma waraka. Mahusiano mazuri ya Paulo na kanisa la Filipi yanaonekana wakati wote wa waraka wake wa furaha. Kwa upande mwingine, mzozo kati ya Paulo na Waamini wakorofi wa Korintho unapelekea kemeo la nguvu katika Wakorintho1 na 2.

### (3) Ni mazingira gani yalipelekea kuandikwa kwa waraka?

Tunafahamu mazingira yaliyopelekea nyaraka kadhaa za Paulo. Wakorintho 1 na 2 ziliandikwa ili kujibu matatizo na maswali kule Korintho. Filemoni iliandikwa kama maombi kwa niaba ya mtumishi aliyekimbia, Onesmo.

Waraka kwa Wagalatia unaonesha thamani ya ufahamu wa mazingira ya waraka. Mistari michache katika Wagalatia, inaweza kukufanya uulize, "kuna shida gani Galatia?" Paulo anaanza, "Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine" (Wagalatia 1:6). Kwa haraka inakuwa wazi kwamba waamini hawa wapya wameiacha Injili ya kuhesabiwa haki kwa neema kupitia imani. Na badala yake wameamini ujumbe wa kuhesabiwa haki kwa matendo. Maneno yenye nguvu na yenye hisia ya Paulo yaliyosukumwa na upendo wake kwa waamini hawa. Ameyatoa maisha yake yote kuhubiri ujumbe wa kuhesabiwa haki kwa imani pekee. Anashangaa kwamba Wagalatia wanaiacha kweli na kukubali Injili potofu.

### Aina ya Fasihi: Ufafanuzi

Ufafanuzi ni mafundisho yenye mpangilio maalumu. Yanaenda katika mpangilio wa kimantiki kutoka dondoo 1 kwenda 2. Aina hii ya Fasihi ni ya kawaida katika nyaraka za Agano Jipya, hasa hasa katika Nyaraka za Paulo. Katika nyaraka hizi, Paulo anawasilisha kweli katika namna iliyowazi ya mwalimu mzuri.

Ufafanuzi hutumia maneno kama vile *kwa hiyo*, *na*, au *lakini*. Mara nyingi hujumuisha maswali na majibu. Ufafanuzi hutoa mawasilisho ya kimantiki ya kweli.

Katika Wakolosai, Paulo anawasilisha ufafanuzi kuhusu Kristo. Paulo anafundisha kwamba Kristo ni juu ya wanafilosofia wote wa kibinadamu na utamaduni. Paulo anafuata mpangilio huu wa kimantiki:

1. Paulo anatoa ushahidi kuhusu ukuu wa Kristo (Wakolosai 1:15-23)
   - Yeye ni mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.
   - katika yeye vitu vyote viliumbwa.
   - ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa.
   - Upatanisho unapatikana kupitia yeye.
2. Paulo anawakumbusha wasomaji wake kusudi la kuandika. Ujumbe wa Kristo aliyetukuzwa ulikabidhiwa kwa Paulo ili kuuleta kwa mataifa (Wakolosai 1:24–2:5).
3. Paulo anaonya dhidi ya mafundisho ambayo yanakataa ukuu wa Kristo (Wakolosai 2:6-23).
   - Mafundisho kwamba watu wanaokolewa kwa kushika sheria za Mungu.
   - Matendo hatarishi ya kuwasiliana na roho
   - Msisitizo usio sahihi wa nidhamu ya kimwili kwa ajili ya matokeo ya kiroho
4. Kwa hiyo, kwa sababu ya ukuu wa Kristo, hivi ndivyo unavyotakiwa kuishi (Wakolosai 3-4):
   - Utii kwa Kristo utaleta matokeo katika tabia zetu za kimaadili.
     - Hatutakuwa na tabia mbaya tena (Wakolosai 3:1-11).
     - Tutaishi kwa Amani na shukrani (Wakolosai 3:12-17).
   - Utii kwa Kristo utaleta matokeo katika mahusiano yetu na wengine (Wakolosai 3:18-4:6).
5. Salamu za mwisho zinazo wakumbusha wasomaji kujali kwa Paulo kuhusiana na waamini wa Kolosai (Wakolosai 4:7-18).

Waraka wa Paulo ni ufafanuzi wa mafundisho ya ubwana wa Kristo. Unafundisha kuhusu asili ya Kristo na matokeo ya kweli hii katika maisha yetu kama waamini.

**Somo la 6 Dondoo Muhimu**

(1) Tafsiri sahihi inatuhitaji sisi kuelewa aina ya fasihi ya kifungu cha maandiko tunachojifunza.

(2) Baadhi ya aina muhimu sana za fasihi zinazopatikana katika Biblia zinajumuisha:

- Historia: historia ya kweli na ya uhakika ya watu halisi na matukio halisi.

  Unapotafsiri historia, uliza:

  - Habari ni nini?
  - Watu katika habari ni nani?
  - Je, simulizi hii ya kihistoria inatoa mfano wa kufuata?
  - Je, ni kanuni gani zinazofundishwa katika simulizi ya kihistoria?

- Sheria za Agano la Kale

  Agano la Kale ni muhimu kwa ajili ya waamini wa Agano Jipya kwa sababu:

  - Ni maelezo ya asili ya Mungu.
  - Linatufanya sisi wenye hekima kwa ajili ya wokovu.
  - Linatusaidia kufahamu mapenzi ya Mungu.

  Inaweza kuwa ya masaada sana kufikiri kuhusiana na Nyanja tatu za Sheria za Agano la Kale:

  - Sheria za kiibada
  - Sheria za kiraia
  - Sheria za kimaadili

  Unapotafsiri Sheria za Agano la Kale, uliza:

  - Andiko hili lilimaanisha nini kwa wapokeaji wa kwanza?
  - Ni tofauti gani iliyopo baina ya wapokeaji wa Biblia na ulimwengu wetu?
  - Ni kanuni gani zinazofundishwa katika andiko hili?
  - Je, Agano Jipya linachukua kanuni hizi kwa namna yeyote?

- Ushairi

  Sifa za mashairi ya kiebrania:

  - Usambamba
  - Tamathali za semi

- Mashairi yenye hekima: yanafundisha namna maisha yanavyoenda.

- Mithali: uchunguzi wa jumla wa maisha umetajwa kwa ufupi na kwa uwazi.

  Unapotafsiri Mithali, uliza:

  - Ni kanuni gani za jumla zinazofundishwa katika andiko hili?
  - Je, ni hali gani za zisizo za kawaida zinazoweza kutokea katika kanuni hii?
  - Ni watu gani katika Biblia ni kielelezo cha kanuni hii?

- Unabii wa Agano la Kale: mawasiliano ya ujumbe kutoka kwa Mungu.

  Unapotafsiri unabii wa Agano la Kale, uliza:

  - Nabii alisema nini kwa ulimwengu wake?
  - watu wake waliitikiaje ujumbe wake?
  - Ni kanuni gani kutoka katika ujumbe wa nabii inayozungumza katika ulimwengu wetu leo?

- Fasihi ya kiapokaliptiki

  Unapotafsiri fasihi ya kiapokaliptiki, kumbuka:

  - Imejaa alama.
  - Sio lazima ielezee matukio katika mfuatano wa matukio
  - Inaweza kurudia kuelezea matukio yale yale kwa kutoa taarifa tofauti za kina.

  Dhana kuu katika fasihi ya kiapokaliptiki ni:

  - Changamoto ya kutunza imani katika ulimwengu huu wa uovu
  - Mungu Mwenyezi ambaye anasaidia watu wake.

- Mifano: mafundisho yanayolinganisha kweli ya kiroho na mambo katika asili au mazingira ya maisha. Mara nyingi mifano ilitolewa kama mwitikio ili kujibu swali au mtazamo.

  Unapotafsiri mifano, uliza:

  - Ni kwa namna gani mfano ulitolewa?
  - Hitimisho la mfano lilikuwa ni nini?
  - Ni mwitikio gani au mabadiliko gani ya mtazamo ambayo mfano unatoa?
  - Wapokeaji wa kwanza walikuwa na mwitikio gani?

- Waraka

  Nyaraka za Agano Jipya ni:

  - Zenye mamlaka
  - Za kimazingira
  - Zilielekezwa kwa waamini

  Unapotafsiri nyaraka, uliza:

  - Nani ni wapokeaji wa waraka?
  - Nani ni mwandishi? Anahusianaje na wapokeaji?
  - Ni mazingira gani yalipelekea kuandikwa kwa waraka?

- Ufafanuzi: mafundisho yenye mpangilio maalumu

**Somo la 6 Zoezi**

Katika Somo la 1, ulichagua kifungu cha maandiko ambayo utayasoma wakati wote wa kozi hii. Kifungu chako ni aina gani ya fasihi? Tumia taarifa katika somo hili ili zikusaidie kuelewa zaidi kuhusiana na kifungu chako. Jibu maswali ya tafsiri yanayohusiana na aina mahususi ya fasihi.

# Somo la 7
# Tafsiri: Kujifunza Neno

## Malengo ya Somo

(1) Kutambua thamani ya kujifunza neno kwa kina.
(2) Kuepuka makosa yaliyozoeleka katika kujifunza neno.
(3) Kuelewa na kutumia mchakato wa kujifunza neno.
(4) Kutambua lugha ya kitamathali katika Biblia.

## Utangulizi

Biblia imejaa maana, lakini kwa huzuni, baadhi ya watu wanasoma maandiko pasipo uelewa wa ujumbe wake.[26] Biblia inaundwa na vitabu, sura, vifungu vya maneno, mistari, na maneno. Kuelewa maana za maneno kunatusaidia sisi kutafsiri kwa usahihi kifungu tunachojifunza. Somo hili ni kuhusiana na namna ya kujifunza maneno. Tunajifunza neno ili kuelewa maana yake katika muktadha mahususi wa Biblia.

Wakati mwingine watu wanajifunza maneno ya asili ya kiebrania na kiyunani kwa kutumia vyanzo vya kujifunza Biblia. Vyanzo kama hivyo vinavyotumika havipatikani katika ulimwengu wote, kwa sababu hiyo hatutavijadili katika somo hili. Badala yake, tutajifunza namna ya kujifunza maneno katika tafsiri zetu za Biblia.

Tutatumia mchakato wa hatua tatu wa kujifunza neno:

1. Chagua neno la kujifunza.
2. Orodhesha maana zinazowezekana kwa kila neno lililochaguliwa.
3. Tambua kila neno lina maanisha nini katika muktadha wa kila kifungu.

## Makosa ya Yaliyozoeleka katika Kujifunza Neno

Tunapoanza kujifunza neno, kuna baadhi ya makosa ya kuepuka. Makosa haya mara nyingi yanapelekea tafsiri isiyo sahihi.

### Kupuuza maana ya awali ya neno

Wakati mwingine namna neno lilivyotunika inabadilika kila wakati. Endapo tafsiri zetu za Biblia zilifanyika miaka kadhaa iliyopita, tunahitaji kufahamu kwamba maana za baadhi ya maneno katika Biblia zetu zinaweza kuwa tofauti na maana ya neno leo. Endapo hatutaelewa namna neno lilivyotumika hapo kabla, tunaweza kuja na hitimisho lisilo sahihi

---

[26] Nyenzo nyingi katika somo hili zinatoka katika sura ya 9 ya J. Scott Duvall na J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012).

kuhusiana na kifungu tunajifunza. (Hili si suala kubwa sana tunaposoma tafsiri ya Biblia iliyotoka miaka ya hivi karibuni.)

► Zungumza kuhusiana na neno katika lugha yako ambalo lina maana tofauti leo na lilivyokuwa likimaanisha.

**Kufikiri kwamba neno lina maana ile ile katika kila muktadha**

Waandishi wa Biblia walitumia maneno ambayo yana maana zaidi ya moja. Neno moja linaweza kutumika kwa maana moja katika muktadha mmoja, na maana tofauti katika muktadha mwingine. Ni lazima tuangalie muktadha ambao neno hilo limetumika ili kujua ni maana gani iliyo sahihi katika mstari tunaojifunza.

## Mchakato Wa Kujifunza Neno

### Hatua ya Kwanza: Chagua neno la kujifunza kutoka kwenye kifungu

Hatuhitaji kujifunza kwa kina kila neno ndani ya Biblia. Wakati mwingine maana ya neno iko wazi. Kwa mfano, Biblia inaposema, Daudi aliokota mawe matano laini (1 Samweli 17:40), hatuhitaji kujifunza neno *jiwe* ili kutafuta maana yake.

Kuchagua neno la kujifunza, angalia:

- Maneno ambayo ni muhimu kwa ajili ya maana ya kifungu.
- Maneno yaliyorudiwa rudiwa.
- Tamathali za semi.
- Maneno yasiyo wazi au ni magumu.

► Soma Warumi 12:1-2 na zungushia maneno muhimu kwa ajili ya kujifunza. Pembeni mwa kila neno, toa sababu ya kwa nini unalichagua neno hilo:

1 = Neno Muhimu
2 = Neno Lililorudiwa rudiwa
3 = Tamathali ya Semi
4 = Neno lisilo wazi au gumu

> Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

Baadhi ya maneno ambayo unaweza kuyawekea alama ni:

1 = Neno Muhimu: *nawasihi, itoeni,* msiifuatishe*,* mgeuzwe*,* kufanywa upya
2 = Neno lililorudiwa rudiwa: Hakuna katika kifungu hiki
3 = Tamathali ya semi: *dhabihu iliyo hai*
4 = Neno lisilo wazi au gumu: *ibada yenye maana*

**Hatua ya Pili: Orodhesha maana zinazowezekana kwa kila neno lililochaguliwa**

Lugha nyingi zina maneno ambayo hutumiwa kwa namna nyingi, na maana tofauti sana. Kwa kawaida msikilizaji anajua maana ya mzungumzaji kwa sababu ya muktadha. Mara nyingine, ucheshi au kutoelewana sana hutokea wakati msikilizaji ameshindwa kuzingatia muktadha na anakosea kuhusu kile ambacho mzungumzaji anamaanisha.

► Je, unaweza kufikiria juu ya wakati ambapo mtu alifanya makosa kwa sababu hakuelewa nini mwingine alimaanisha kuhusiana na neno fulani?

Katika hatua hii ya pili, tunapaswa kujaribu kufikiria kila njia iwezekanayo ambayo neno hilo linaweza kutumiwa. Ikiwa tafsiri yetu ya Biblia ni ya zamani, tunapaswa pia kufikiria ikiwa neno hilo lilikuwa na maana za ziada hapo awali.[27] Endapo tuna kamusi, inaweza kutusaidia kutengeneza orodha ya maana zote zinazowezekana. Ikiwa tunajifunza na watu wengine, wanaweza pia kutusaidia kufikiria maana ambayo sisi hatukufikiria.

Kama inawezekana, tafuta tafsiri nyingine za Biblia na kuona endapo zimetumia neno lile lile, kama tafsiri nyingine imetumia neno tofauti, linganisha maana ili kuona tofauti ni nini.[28] Je, yanamaanisha kitu kimoja? Kama sivyo, tofauti ni nini? Je, maana ya kifungu itabadilika kwa kutumia neno lingine?

---

[27] Endapo tunatumia tafsiri ya zamani ya Biblia, kuangalia tafsiri mpya ya Biblia kutatupatia mwanga kuhusiana na maana ya inayowezekana ya neno katika muktadha husika.
[28] Rejea Nyongeza kwa orodha ya tovuti ambapo unaweza kusoma Biblia katika lugha na matoleo mbalimbali.

► *Itoeni* lilikuwa mojawapo ya neno ambalo liliwekewa alama kwa ajili ya kujifunza kutoka katika Warumi 12:1-2. Fanyeni kazi pamoja ili kuorodhesha maana zote zinazowezekana za neno *itoeni*.

**Hatua ya Tatu: Tambua neno linamaanisha nini katika Muktadha**

Baada ya kuangalia matumizi mbalimbali ya neno na kutengeneza orordha ya maana zinazowezekana, uko tayari kutambua neno lina maana gani katika kifungu unachojifunza. Muktadha utakuongoza. Kumbuka, mwandishi hakumaanisha kutumia maana maalumu sana ambayo watu wachache wangeweza kufahamu. Mwandishi alitaka wasomaji kuelewa.

Tuliangalia umuhimu wa muktadha katika somo la 5, kwa sababu hiyo hatutajikumbusha tena nyenzo hizo hapa. Kwa kufupisha wajibu wa muktadha: tunaangalia mstari, sura, na kitabu kinachozunguka ili kupata maana bora ya neno.

Yapo maswali ya kuzingatia wakati unaagalia muktadha na kujaribu kugundua maana ya neno.

**(1) Je kuna ukinzani au ulinganifu katika kifungu ambao unakusaidia kutoa maana ya neno?**

► Soma Yohana 3:16: "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Kwa pamoja, orodhesheni maana zote zinazowezekana na neno *asipotee*. (Mnaweza kutumia kamusi yeyote ambayo mnayo.) Sasa, zingatia ukinzani unaotolewa katika mstari. **Kupotea** kunatofautishwa na **kuwa na uzima wa milele**. Katika orodha yako, ni maana gani ya neno *asipotee* iliyokuwa ikimaanishwa na Yesu katika sentensi hii?

**(2) Ni kwa namna gani mwandishi ametumia neno hili katika maeneo mengine?**

Neno *ulimwengu* pia limetumika katika Yohana 3:16. Neno *ulimwengu* linaweza kumaanisha mambo kadhaa:

- Ulimwengu wa kifizikia
- Watu wote
- Mataifa yaliyojulikana kuwa yamestaarabika
- Jamii ya jumla ambayo inamkataa Mungu

Mwandishi alitumia neno *ulimwengu* kurejelea kila kimojawapo kati ya hivi katika sehemu mbalimbali katika Maandiko. Kutambua ni maana gani ya *ulimwengu* anayo katika Yohana 3:16, tunapaswa kuangalia mifano ya matumizi ya Yohana ya neno.

- Yohana 1:10, "Alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua." Mstari huu unazungumza kuhusu Yesu. Ulimwengu haukumtambua Yeye.

- Yohana 7:7, “Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi; bali hunichukia mimi, kwa sababu mimi naushuhudia ya kuwa kazi zake ni mbovu.” Yesu anaongea katika mstari huu. Ulimwengu unamchukia Yeye.

- Yohana 14:17, “ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.” Ulimwengu hauwezi kumpokea Roho wa Kweli.

- 1 Yohana 2:15-17, “Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.” Maadili ya ulimwengu na utafutaji wake ni kinyume kabisa na Mungu.

Mtume Yohana mara nyingi ametumia neno *dunia* kurejelea jamii kwa ujumla ambayo inamkataa Mungu. Hii inaonesha kiwango cha ahadi ya Yesu: Mungu aliwapenda sana wale ambao walitengwa na Yeye kiasi kwamba alimtoa mwana wake ili kwamba wote waokolewe.

**(3) Muktadha unaonesha nini kuhusiana na maana ya neno?**

► Angalia Luka 1:68-79.

Katika Luka 1:71, Zakaria anaomba ili kwamba Israeli *Tuokolewe*. Anarejelea nini? Neno *Tuokolewe* linamaanisha nini katika mstari huu?

Dhana ya *wokovu* ina maana zaidi ya moja katika maandiko. Mahususi kabisa inaweza kumaanisha:

- Kuokolewa na adui au hatari
- Kuokolewa kutoka magonjwa
- Kuokolewa kutoka dhambini

Muktadha wa karibu (Luka 1:68-74) unaonesha kwamba “*Tuokolewe”* linarejelea kuokolewa na adui. Ukombozi (wokovu) utatimiza ahadi ambayo Mungu alimwahidi Abrahamu (Luka 1:73).

Mistari michache baade, Luka anatumia neno *wokovu* katika maana ya ndani (Luka 1:77). Kwa kupitia uongozi wa Roho Mtakatifu, Zakaria atamuona mtoto wake akiitwa kuwa nabii wa aliye juu. Mtoto wa Zakaria atawapa watu wa Bwana ufahamu wa wokovu katika msamaha wa Dhambi zao. Hapa, *wokovu* umeunganishwa na msamaha wa dhambi.

Maana tofauti tofauti za *wokovu* zimetumika katika maombi haya. Tunatambua maana kutoka katika muktadha.

## Shughuli za Kufanyia Mazoezi

*Angalizo kwa kiongozi wa darasa: Tenga muda wa kutosha darasani kwa ajili ya shughuli hizi za mazoezi kwa vitendo. Ikiwa kipindi chako cha darasani kawaida ni saa moja, tumia kipindi kizima cha darasa kwenye mazoezi haya. Muda uliopendekezwa umetolewa kwa kila zoezi. Kufanya mazoezi pamoja wakati wa darasa kutawasaidia wanafunzi kutumia mawazo wanayojifunza. Kupitia mchakato wa kujifunza neno na watu wengine pia kutawasaidia kuona kwamba mara nyingi kuna mitazamo na maelezo ambayo hawatazingatia ikiwa watafanya kazi peke yao.*

*Kwa shughuli za vikundi vidogo vidogo, kuwa na wanafunzi watatu katika kila kundi. Kundi zima litakuja pamoja dakika tano za mwisho na kujadili kile walichojifunza.*

► **Shughuli za vikundi vidogo vidogo (Dakika 20)**. Katika kundi lako, tafuta mistari kadhaa ambapo neno moja limetumika likiwa na maana mbalimbali. Hapa ni mawazo machache yanayoweza kukusaidia kuanza: *nyumba, maono, siku, tunda*. Unapotambua baadhi ya mistari inayotumia neno moja kwa namna tofauti, andika orodha ya namna zote ambazo neno hilo linaweza kutumiwa. Je, kujifunza maneno kunasaidia vipi katika tafsiri sahihi ya kila mstari?

► **Shughuli ya kundi kubwa (dakika 10)**. Sasa rudi katika Warumi 12:1 na orodha yako ya maana zinazowezekana za neno *itoeni*. Tumia maswali yaliyo hapo juu kukusaidia kutambua maana iliyokusudiwa katika mstari huo.

► **Shughuli za vikundi vidogo vidogo (dakika 30)**. Katika kikundi chako, jizoeze kupitia mchakato wa kujifunza neno. Tayari umeweka alama katika maneno katika Warumi 12:1-2 ambayo yanapaswa kujifunza kwa makini. Kwa kila moja ya maneno hayo, orodhesha kila maana inayowezekana na uamue neno hilo lina maana gani katika muktadha huo.

## Suala Maalumu: Lugha ya Kitamathali

Katika Somo la 6, tuliangalia kwa ufupi matumizi ya tamathali za semi. Haijalishi tumejifunza neno kwa umakini kiasi gani, hitimisho letu halitakuwa sahihi endapo hatutaelewa lugha ya mwandishi ya kitamathali. Katika tamathali ya semi, jambo muhimu si maana halisi ya maneno, bali dhana inayowakilishwa.[29]

Sisi sote tunatumia lugha ya kitamathali. Fikiria kwamba rafiki wa Marekani anakuonyesha picha za bustani yake. Unastaajabishwa na bustani hiyo na kumuuliza rafiki yako, "Unakuzaje mimea mizuri hivyo?" Anajibu, "Nina kidole gumba cha kijani." Haimaanishi kuwa kidole gumba mkononi mwake ni kijani kibichi. Anatumia tamathali ya usemi ya Kiingereza cha Marekani inayomaanisha, "Nina uwezo usio wa kawaida wa kukuza mimea."

---

[29] Nyenzo katika sehemu hii zimechukuliwa kutoka sura ya 36 ya Howard G. Hendricks and William D. Hendricks, *Living by the Book* (Chicago: Moody Publishers, 2007).

► Je, ni vishazi gani katika lugha yako ambavyo vinamaanisha kitu tofauti na maana yake halisi?

Wakati mwingine neno hutumiwa kuwakilisha kitu kingine. Hii sio sawa na neno moja kuwa namaana zaidi ya moja. Kwa mfano, katika Biblia watu wengine wanaitwa mbwa (Ufunuo 22:15). Kauli hiyo ni ukosoaji wa watu ambao wana tabia fulani za mbwa ambazo watu hawapaswi kuwa nazo. Neno *mbwa* bado lina maana ya mnyama tunayemwita mbwa, lakini linatumika kwa njia ya kitamathali kurejelea watu. Yesu alimwita Simoni kwa jina la Petro, maana yake *mwamba*, kwa sababu Petro alikuwa na tabia ya mwamba ambayo ni nzuri kwa watu kuwa nayo (Mathayo 16:18). Yesu alikuwa akitumia maana ya kawaida ya neno *mwamba*, akionyesha uhakika kwamba Simoni alikuwa kama mwamba kwa njia fulani.

Yesu alimwita Herode mbweha (Luka 13:32). Hatuhitaji kujifunza maana ya tofauti ya maana ya neno *mbweha* kisha kuangalia katika muktadha kuangalia ni mnyama wa aina gani Yesu alimaanisha. Ni kauli ya kitamathali, kwa hiyo tunataakiwa kuelewa ni nini Yesu alimaanisha aliposema kuhusu Herode kwa kumwita mbweha. Yesu alimaanisha kwamba Herode alikuwa na akili nyingi lakini hakuweza kuaminiwa kwa sababu ya tabia yake mbaya.

► Ni mnyama gani ambaye anatumiwa kitamathali katika utamaduni wako ili kukosoa watu?

Ni kwa namna gani tunajua kwamba sentensi hii ni halisi au ni ya kitamathali? Hapa kuna miongozi miwili ya kuzingatia:

1. **Tumia maana ya Kitamathali wakati kifungu kinakuambia kufanya hivyo.** Mwanzo 37 inahusisha ndoto mbili. Katika Biblia, ndoto mara nyingi iliwasilisha ujumbe wa kitamathali. Kwa sababu ya hii, hatutakiwi kutegemea kwamba ndoto ya Yusufu itamaanisha kihalisia kwamba miganda ya ngano itauinamia mganda mwingine, au jua, mwezi, na nyota kumwinamia Yusufu kiuhalisia. Badala yake, sentensi ambayo ni ndoto inatuambia sisi kutegemea lugha ya kitamathali. Katika hali hii, tafsiri inatolewa katika Mwanzo 37:8, 10.

2. **Tumia maana ya Kitamathali wakati maana halisi haiwezekani au ni upuuzi.** Katika Ufunuo 1:16, Bwana litokea na upanga ukatao kuwili ukitoka kinywani mwake. Katika kitabu kilichojaa lugha ya picha, ni kwa nadra sana kwamba hii itamaanisha picha halisi ya Yesu! Tunapoendelea katika Ufunuo, tunaona kwamba picha ya Yesu akiwa na upanga ukatao kuwili unakaa vizuri katika ujumbe wa ushindi mkuu dhidi ya nguvu za uovu.

Kumbuka kwamba Mungu alitoa Neno lake ili kuwasilisha kweli, si kuficha ukweli. Lugha nyingi za kitamathali katika Biblia zitakuwa dhahiri. Tuliona orodha ya tamathali za usemi katika Somo 6. Hizi hukupa ufahamu mzuri ya jinsi ya kufasiri lugha ya kitamathali. Baada ya kutambua tamathali ya usemi, uliza, "Kwa nini Mungu aliongoza taswira hii mahususi? Ni ukweli gani unaowasilishwa kwa taswira hii?"

Wakati fulani neno linatumiwa kwa njia ya kitamathali na linakuwa alama ya kudumu. Yesu aliposema, “Kondoo wangu waisikia sauti yangu…” (Yohana 10:27), wasikilizaji walijua

alimaanisha watu wanaomfuata, na Biblia inatumia alama hiyo nyakati nyingine (Zaburi 23, kwa mfano). Katika Ufunuo 5, Simba aliye wa kabila ya Yuda anatokea mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Kamusi ya Biblia inaeleza kwamba "Simba aliye wa kabila ya Yuda" ni jina la cheo linalomrejelea Masihi. Unapojua hilo, unauliza, "Kwa nini Yohana anatumia jina hili? Jina hili linatuambia nini kuhusu Yesu?" Kwa kutambua tamathali ya semi iliyotumika hutusaidia kuelewa taswira ya Yohana ya nguvu za Yesu za ukombozi.

Ule ukweli kwamba waandishi wa Biblia wakati mwingine walitumia lugha ya kitamathali haimaanishi kwamba hatupaswi kamwe kufasiri maandiko kihalisia. Badala yake, kwa kujua kwamba lugha ya kitamathali ilitumiwa nyakati fulani, tunatakiwa kujaribu kuelewa andiko katika namna ambayo mwandishi alikusudia. Hatupaswi kutumia mawazo yetu kufanya tamko la kibiblia kumaanisha kitu ambacho mwandishi hakuwa anajaribu kusema.

## Hitimisho

Mwandishi wa Mithali alitoa ahadi hii kwa mtu anayetafuta hekima; "Ukiutafuta kama fedha, Na kuutafutia kama hazina iliyositirika; Ndipo utakapofahamu kumcha BWANA, Na kupata kumjua Mungu" (Mithali 2:4-5). Hakuna chanzo kikuu cha hekima kuliko Neno la Mungu. Kujifunza kwako maandiko kuna malipo ya milele.

**Somo la 7 Dondoo Muhimu**

(1) Kujifunza neno ni kuchunguza maneno muhimu katika kifungu kwa makusudi ya kugundua maana yake ndani ya muktadha. Kujifunza neno kunatusaidia sisi kutafsiri kwa usahihi kifungu tunachojifunza.

(2) Makosa mawili yaliyozoeleka ya kuepuka unapofanya kujifunza neno:

- Kupuuza maana ya awali ya neno
- Kufikiri kwamba neno lina maana ile ile katika kila muktadha

(3) Mchakato wa kujifunza neno:

- Chagua neno la kujifunza.
    - Maneno ambayo ni muhimu kwa ajili ya maana ya kifungu
    - Maneno yaliyorudiwa rudiwa
    - Tamathali za semi
    - Maneno yasiyo wazi au ni magumu
- Orodhesha maana zinazowezekana kwa kila neno lililochaguliwa.
- Tambua kila neno lina maanisha nini katika muktadha wa kila kifungu.

(4) Maswali ambayo yatatusaida kutambua ni nini neno linamaanisha katika muktadha:

- Je kuna ukinzani au ulinganifu katika kifungu ambao unakusaidia kutoa maana ya neno?
- Ni kwa namna gani mwandishi ametumia neno hili katika maeneo mengine?
- Muktadha unaonesha nini kuhusiana na maana ya neno?

(5) Mambo ya kukumbuka unapojifunza lugha ya kitamathali:

- Wazo ambalo linawakilishwa ndiyo muhimu.
- Picha, kifungu cha maneno, au neno la kitamathali linawakilisha kitu kingine.
- Lugha ya kitamathli inataka umakini kwa sifa za kile inayokiwakilisha.
- Tunatakiwa kujaribu kuelewa andiko katika namna ambayo mwandishi alikusudia andiko kueleweka hivyo—ama maana ni halisi au ya kitamathali.

(6) Wakati gani tunatafsiri sentensi ya kimaandiko kitamathali:

- Wakati kifungu kinakuambia kufanya hivyo
- Wakati maana halisi haiwezekani au ni upuuzi

**Somo la 7 Mazoezi**

(1) Katika Somo la 1, ulichagua kifungu cha maandiko ambayo utayasoma wakati wote wa kozi hii. Kutoka katika kifungu, orodhesha maneo ambayo uanfikiri ni muhimu kujifunza. Angalia maneno muhimu, maneno yaliyorudiwa rudiwa, tamathali za semi, au maneno yasiyo wazi au ni magumu. Jifunze kila mojawapo ya maneno haya kwa kufuata mchakato ulioelezewa katika somo hili. Zingatia muktadha. Tambua maana ya kila neno katika muktadha wa kifungu unachojifunza.

(2) Zingatia kila neno ambalo umekuwa unajifunza. Tafura orodha ya maana zinazowezekana ambazo umezitengeneza katika kujifunza kwako. Ni kwa jinsi gani kutoelewa kwa usahihi maana katika kujifunza kwako kutapelekea kuwa na tafsiri isiyo sahihi ya kifungu? Andika sentensi 2-4 za tafakari.

# Somo la 8
# Tafsiri: Kanuni za Jumla

## Malengo ya Somo

(1) Kuelewa kanuni za msingi za Kutafsiri Biblia.

(2) Kutumia kanuni hizi wakati wa kujifunza andiko.

(3) Kuwa makini na namna ambavyo kushindwa kufuata kanuni hizi kutapelekea kwenye makosa katika mafundisho.

## Utangulizi

Kanuni katika somo hili ni msingi kwa ajili ya kujifunza maandiko. Hizi ni kanuni ambazo waalimu wa Biblia wenye busara wamezitengeneza ili kuongoza ujifunzaji wao. Kanuni hizi zinatakiwa kuwa msingi wa njia zako za kujifunza Biblia. Tafadhali chukua muda kuzielewa kanuni hizi na kisha uzitumie katika kujifunza kwako.

## Zingatia Kusudi la Mwandishi

Mwandishi alikusudia kitu kwa wasomaji wake. Maana ile iliyokusudiwa ndiyo maana ya andiko. Tafsiri ni kazi inayojaribu kuuelewa ujumbe uliokususduwa na mwandishi. Hatutakiwi kutumia maandiko kama nyenzo kwa ajili ya ujumbe ambao ni tofauti na maana iliyokusudiwa na mwandishi.

Tamko la kimaandiko linaweza kumaanisha zaidi ya vile mwandishi alivyokusudia. Ibrahimu alipomwambia Isaka kwamba "Mungu atajipatia mwana-kondoo…" (Mwanzo 22:8), anaweza asijue kuwa Mungu atatimiza maneno haya katika namna kubwa zaidi katika ujio wa Yesu. Musa alipoandika maneno hayo ya Ibrahimu, musa anawezakuwa hakuwa anaelewa maana ya tamko hilo. Hata hivyo, kutumia tamko kwa ajili ya ujio wa Yesu si kutumia maana tofauti na iliyokusudiwa na Musa; ni matumizi mapana, yaliyokamilika ya kanuni ambayo Mungu anatoa kile ambacho kinatakiwa kwa ajili ya wokovu.

Kila mwandishi wa Biblia alikusudia kwamba wasomaji wake wa kwanza wautumie ujumbe wake katika matendo. Matumizi yetu ya ujumbe yanaweza kuwa tofauti na matumizi ya wapokeaji wa kwanza, lakini yanafuata kanuni zile zile. Kwa sababu tunatumia kanuni za kibiblia katika mazingira tofauti, matendo yetu yanaweza kuwa tofauti. Kwa mfano, watu wa Israeli waliambiwa waweke kingo katika dari za nyumba zao (Kumbukumbu la Torati 22:8). Dari za nyumba za wakati huo zilikuwa tambarare na zilitumika kama sehemu ya kuishi. Kama hauishi katika nyumba ambayo ina dari tambarare ambapo watu hawaendi, hauhitaji kingo. Hata hivyo, tunatakiwa kutumia kanuni ya kufanya mali zetu kuwa salama kwa ajili ya watu.

Mtafsiri hatakiwi kutengeneza tafsiri ya kufikirika kwa ajili ya taarifa katika kifungu. Hapa ni mfano wa tafsiri ya kufikirika ya Habari ya Yesu ya Masamaria mwema aliyemsaidia mtu aliyejeruhiwa (Luka 10:30-35):

> Msamaria ni mwinjilisti, mtu aliyejeruhiwa ni mwenye dhambi ambaye ametubu, nyumba ya wageni ni kanisa, na dinari mbili ni ubatizo na meza ya Bwana.

Tafsiri hii inapuuza dondoo ambayo Yesu alikusudia kutengeneza kuhusiana na kuwapenda Jirani zetu (Luka 10:27-29, 36-37): tunatakiwa kuonesha upendo kwa wale tunaokutana nao ambao wana uhitaji.

Yapo matatizo matatu katika tafsiri za kufikirika:

1. Zinatokea katika mawazo ya mtafsiri.
2. Haziongozwi na kanuni nzuri za kutafsiri.
3. Haziwezi kutathiminiwa na njia zozote za kawaida na za kimantiki.

## Anza na Andiko, na si Hitimisho Lako

Shujaa aliangalia ramani ili kufika anakokwenda, lakini Shujaa alisema, "Ramani hii si sahihi." Abiria wa Shujaa wakauliza, "Unajuaje kwamba ramani si sahihi?" Shujaa alijibu kwa ujasiri, "Ninafahamu njia ya kupita. Ramani si sahihi." Masaa machache baadae, akiwa amepotea kabisa, Shujaa akakiri kwamba ameshindwa na akaanza kujaribu kuielewa na kuifuata ramani. Kosa lake lilikuwa ni nini? Alianza na hitimisho. Alikuwa na uhakika kwamba ana jibu sahihi, kwa hiyo alikataa kuisikiliza ramani ambayo ilitoa jibu tofauti.

Baadhi ya watu wanasoma Biblia kwa namna hii. Wakati mmoja mhubiri anaposoma mstari wa andiko asilolipenda. Akasema, "Sifahamu huu unamaanisha nini, lakini halimaanishi kile linachosema." Alianza na hitimisho ("Sikubaliani na fundisho hili") na kisha anasoma andiko. Hakupata andiko linaloendana na hitimisho lake, kwa sababu hiyo aliamua tu kulipuuza andiko ("Halimaanishi kile linachosema").

Ili kutafsiri andiko, tunatakiwa kuanza na andiko na kisha kutafuta hitimisho letu. Kila mmoja wetu ana nadharia fulani. Tunaanza na mtazamo fulani. Hii ni sawa. Tatizo ni pale nadharia zetu zinapotusababisha kupuuza fundisho sahihi la maandiko. Tunapaswa kuhakikisha tunaanza na andiko, na si hitimisho zetu. Hatutakiwi kuruhusu nadharia zetu kutusababisha sisi kupuuza andiko.

### Mfano

"Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu" (Mathayo 5:48).

Baadhi ya watu wanasema, "Hakuna aliye mkamilifu!" Kwa hiyo, wanapuuza agizo la Yesu. Wameanza na hitimisho lao ("Hakuna aliye mkamilifu!") na hata hawajaribu kuelewa kile Yesu alichokimaanisha.

Unapojifunza Mathayo 5:48, lazima tuulize, “Yesu alimaanisha nini kwa kusema ‘wakamilifu? Ni kwa namna gani tunatakiwa kuwa kama Baba yetu wa mbinguni?” Mistari michache kabla ya Mathayo 5:48 inatoa majibu: Tunapaswa kuwapenada adui zetu na kuwatendea mema kwa namna ile ile ambayo Baba yetu wa mbinguni “…huwaangazia jua lake waovu na wema …” (Mathayo 5:45).

### Mafundisho ya Maandiko Hayakinzani na Mafundisho ya Maandiko

Tunaposoma kitabu cha mwandishi wa kibinadamu, kinaweza kujipinga kwa namna fulani. Waandishi wawili wa kibinadamu wanaweza kupingana katika hoja fulani. Hata hivyo, Biblia ni neno la Mungu; haliwezi kujipinga.

Mungu habadiliki (Yakobo 1:17). Kwa sababu ya hili, neno lake ni sawasawa na hata kama liliandikwa kwa kipindi cha miaka mamia na waandishi kadhaa wa kibinadamu. Neno la Mungu haliwezi kujipinga lenyewe.

Kanuni hii ni muhimu kutokana na mafundisho ya uvuvio: “Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu…” (2 Timotheo 3:16-17). Kama chanzo kikuu cha maandiko ni Mungu, Biblia haiwezi kujipinga yenyewe. Hii ni muhimu kwa tafsiri nzuri ya Biblia. Pale ambapo vifungu vinaonekana vinajipinga, tunatakiwa kuuliza kama hatukuelewa vizuri andiko mojawapo. Tunapoelewa kwa usahihi kila kifungu, tunaona kwamba kila kifungu ni sahihi.

**Mfano**

“Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria” (Warumi 3:28).

“…mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu” (Wagalatia 2:16).

“Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake” (Yakobo 2:24).

Baadhi ya waandishi wanafikiri kwamba Yakobo na Paulo hawakukubaliana kuhusiana na kazi ya imani na matendo. Paulo anasisitiza kwamba mtu anahesabiwa haki pasipo matendo ya sheria. Yakobo anaandika kwamba mtu anahesabiwa haki kwa matendo, na si kwa imani peke yake.

Pasipo kuangalia muktadha wa mistari hii mtu anaweza kufikiri kuwa Yakobo alimpinga Paulo. Hata hivyo, muktadha wa kila kifungu unaonesha ni nini Paulo na Yakono walikuwa wanasema. Paulo anazungumzia namna ambavyo mtu anaokolewa na kufanywa mwenye haki. Mtu anakuwa mwenye haki kwa imani. Yakobo anazungumzia kuhusiana na namna ambavyo mtu anaonesha kuwa ameokoka. Mtu anaonesha haki yake kwa matendo. Wote wawili Paulo na Yakobo wanakubaliana kwamba mtu anakuwa mwenye haki kwa imani, na kisha anaonesha haki yake kwa matendo.

## Maandiko ni Mtafsiri Bora wa Maandiko

Kanuni hii ina mahusiano makubwa na kanuni iliyopita. Kwa sababu maandiko hayajipingi yenyewe, tunaweza kutumia vifungu vyenye maana zilizo wazi ili kutusaidia kuelewa vifungu ambavyo maana zake haziko wazi sana. Tunatumia mistari ambayo iko wazi ili kuelezea mistari migumu zaidi; hatupindishi mistari rahisi ili kufaa tafsiri zetu za mistari migumu.

Kitabu cha tafsiri kinasema hivi: "Mara nyingi kile ambacho kimefichika katika sehemu moja ya Biblia, kimewekwa wazi katika sehemu nyingine."[30] Kwa kujifunza maandiko yote, tunaruhusu mistari iliyowazi kutoa mwanga kwa mistari ambayo ni migumu zaidi.

### Mfano

"Au je! Wenye kubatizwa kwa ajili ya wafu watafanyaje? Kama wafu hawafufuliwi kamwe, kwa nini kubatizwa kwa ajili yao?" (1 Wakorintho 15:29).

Kwa sabau ya mstari huu, baadhi ya watu wanafikiri kwamba walio hai wanatakiwa kubatizwa kwa ajili ya watu waliokufa kabla kubatizwa. Hata hivyo, hakuna sehemu yeyote ambapo Biblia inatuambia hivyo. Paulo alitaja utamaduni huu ambao wasomaji wake walikuwa wanaufanya, lakini hatujui utamaduni huu ulikuwaje.

Maandiko ni mtafsiri bora wa maandiko. Kanuni hii inatuongoza sisi kutafsiri 1 Wakorintho 15:29. Tunaposoma Mathayo 28:19, Matendo ya Mitume 2:41, Matendo ya Mitume 8:12, na Matendo ya Mitume 19:5, tunaona kwamba ubatizo ulikuwa kwa ajili ya waamini wanaoishi. Kwa kuwa 1 Wakorintho 15:29 haiagizi kwa wazi ubatizo kwa ajili ya wafu na kwa sababu mistari mingine inaonesha kwa wazi matendo ya kanisa la kwanza, hakuna sababu ya kuamini kwamba 1 Wakorintho 15 inaagiza ubatizo kwa ajili ya wafu.

## Maandiko Yaliandikwa ili Kueleweka

Maana ya neno la Mungu inaweza kupatikana katika maandiko yenyewe, kwa kutumia njia za kawaida za kutafsiri. Neno la Mungu halikuandikwa kwa kutumia herufi za siri.

Tangu mwanzo wa kanisa, kweli zote za injili zimepokelewa na kufunuliwa kwa uwazi kwa kila mtu, si tu kwa washirika maalumu wa kanisa. Yesu alisema kwamba hakuwa na mafundisho yeyote ya siri kwa ajili ya wafuasi wake (Yohana 18:20). Mtume Paulo alimwambia Timotheo kufundisha wengine kweli ambayo Paulo aliifundisha hadharani (2 Timotheo 2:2). Paulo alieleza kwamba kama watu hawawezi kuona kweli, si kwa sababu imefichwa kwa makusudi, bali ni kwa sababu Shetani amewapofusha (2 Wakorintho 4:1-6). Utume wa kanisa wakati wote umekuwa ni kushirikisha kwa wazi kweli ya Injili.

---

[30] Walter Kaiser na Moises Silva, *An Introduction to Biblical Hermeneutics* (Grand Rapids: Zondervan, 1994), 132.

> “Mara nyingi Tafsiri za Kipekee si sahihi.”
> - Gordon Fee, *How to Read the Bible*

Ni kweli kwamba maandiko mengi ni lazima yasomwe kwa umakini ili kupata maana yake, lakini kweli yake haijafichwa. Kweli kuu ya maandiko haijazikwa katika mistari iliyojificha isiyoeleweka. Mzaburi anasema, “Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu” (Zaburi 119:105). Kusudi la neno la Mungu ni kutuongoza sisi, na si kuficha ukweli.

Hakuna funguo maalumu ili kufungu ujumbe wa neno la Mungu. Usiamini vitabu ambavyo vinadai kufungua mfumo maalumu uliofichwa wa Biblia. Mungu aliongea ili kwamba sisi tuelewe neno lake.

**Mfano**

Kwa miaka michahe, mtu mmoja angedai, “Mungu amenifunulia mimi kwamba Yesu angerudi mwaka unaofuata.” Kitabu maarufu mwaka 1987 kilitabiri ujio wa Yesu mwaka 1988. Mwandishi alidai kwamba amegundua kweli hii baada ya kusoma sherehe za kale za Kiyahudi. Mwandishi yule yule aliandika kitabu mwaka unaofuata akitabiri unyakuo mwaka 1989. Hatutakiwi kumwamini mtu ambaye msingi wa mafundisho yake muhimu ni njia za siri au zilizofichika za kutafsiri Biblia. Yesu alisema, “Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake” (Mathayo 24:36).

### Maagizo ya Biblia yanaonesha Ahadi za Biblia

Kanuni hii inafundisha kwamba kama Mungu alitoa agizo, anatengeneza utii kuwezekana.

Fikiria baba ambaye anasema, “Mwanangu, ili kunipendeza unatakiwa kukimbia maili mbili ndani ya dakika mbili.” Kwa mara kadhaa, mtoto atajitahidi kwa uwezo wake wote, lakini kila wakati atashindwa kufikia matarajio ya baba yake. Mwishowe, mtoto anakata tamaa na ataacha kujaribu. Je, huyu ni baba mzuri?

Baadhi ya watu wanafikiri kwamba Mungu ni baba asiye na mantiki. Mungu anaposema, “Iweni watakatifu,”[31] wanasema, “Mungu anafahamu kwamba hatuwezi kuyatii maagizo yake.”

John Calvin alisema kwamba hatuwezi “…kupima nguvu ya wanadamu kwa [maagizo] ya Mungu.”[32] Calvin aliamini kwamba Mungu anatupa maagizo ambayo hatuwezi kutatii kwa uwezo wa kibinadamu, lakini kwamba Mungu hutoa nguvu ya kutii kwa wale wanaookoka. John Wesley alifundisha kwamba kila agizo la Mungu ni ahadi kwamba nguvu za Mungu zitatimizwa ndani ya mwamini.

---

[31] Mungu ameagiza hili mara kadhaa, sio tu mara moja. (Ona Mambo ya Walawi 11:44, 45, Mambo ya Walawi 20:7, na 1 Petro 1:16.)

[32] John Calvin’s mafafanuzi juu ya 1 Wathesalonike 5:23 kutoka *The Epistles of Paul to the Romans and Thessalonians.*

Mtu hawezi kutimiliza maagizo ya Mungu katika nguvu za kawaida za mwanadamu. Lakini tunaweza kutimiliza maagizo ya Mungu kwa nguvu zake. Baba wa mbinguni mwenye upendo anawawezesha Watoto wake kutii agizo lake. Baba mwenye upendo hawezi kufachachafya Watoto wake kwa maagizo yasiyowezekana. Kila agizo la maandiko linasindikizwa na neema ya kutii agizo.

Yesu aliagiza, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote" (Mathayo 22:37). Hili ni vyote viwili agizo na ahadi. Agizo la Mungu la kupenda kwa moyo wote linaonesha ahadi yake ya kutupa sisi moyo usiogawanyika kama tutamwamini Yeye.

**Mfano**

"Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu" (Mathayo 5:48).

Kutoka katika muktadha, tunaelewa kwamba Yesu alikuwa anarejela upendo, na si ukamilifu katika kila njia. Na pia tunaelewa kwamba hili si jambo ambalo tunatakiwa kulikamailisha sisi wenyewe kwa nguvu zetu. Mungu anayetuagiza sisi kuwa wakamilifu ni Mungu anayetimiza agizo. Mzaburi anashuhudia, "[Ni] Mungu ndiye anifungaye mshipi wa nguvu, Naye anaifanya kamilifu njia yangu" (Zaburi 18:32).

Agizo la Yesu ni lazima lieleweke. Ni lazima lisomwe katika mwanga wa muktadha wa karibu wa mafundisho ya Yesu, na katika mwanga wa mafundisho kuhusu watu kuwa wakamilifu (kutogawanyika) moyo na kuwa watakatifu (kutengwa). Mara baada ya kuelewa hili, agizo la Yesu linakuwa ahadi yenye neema, na si kipimo kisichowezekana kwa ajili ya juhudi ya wanadamu.


## Lenzi Tatu juu ya Biblia

Kama wakristo wa kiinjili, tunaamini Biblia ni mamlaka ya mwisho kwa ajili ya mafundisho na mwenendo. Biblia ina maarifa yote yanayohitajika kwa ajili ya wokovu.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba tunatafsiri kile ambacho tumekisoma kupitia njia tofauti tofauti. Kwa wainjili wengi, zipo lenzi ambazo kupitia hizo tunasoma Biblia. Lenzi hizi haziwi mbadala wa mamlaka ya Biblia kwa namna yeyote. Ni namna tu ambayo tunasoma na kuelewa maandiko.

Ili kupata uelewa kamili ya maandiko, tunapaswa kutumia lenzi zote tatu. Endapo tutapuuza lenzi moja, tunaweza kutafsiri maandiko isivyo sahihi. Kusoma Biblia kwa kutumia lenzi hizi kunatusaidia sisi kuelewa vema ujumbe wa neno la Mungu.

Picha hii inaweza kukusaidia kuona mahusiano ya lenzi hizi juu ya Biblia. Tunaangalia Biblia kupitia lenzi.[33]




**Lenzi ya 1: Utamaduni**

> "Utamaduni na tunda la mafundisho ya Roho Mtakatifu tangu enzi… Si ya uhakika, lakini pia [ni muhimu], na tutakuwa dhaifu endapo hatutaizingatia."
> - J.I. Packer,
> "Kukuza Umoja Wa Maandiko Leo"

Lenzi ya kwanza kupitia hiyo tunayaangalia maandiko ni utamaduni. Lenzi ya utamaduni inauliza, "Ni kwa namna gani wakristo katika historia walilielewa andiko hili?" Utamaduni unajaribu uelewa wetu wa andiko kwa kulinganisha na katika mwanga wa uelewa wa wakristo wengine katika kipindi chote cha historia.

Utamaduni unajumuisha matamko ya kanisa la kwanza, mafundisho makuu ambayo yamewaunganisha wakristo huko nyuma, na mafundisho wa vivazi vya mwanzoni. Utamaduni unaonesha namna ambavyo Biblia imetafsiriwa katika kipindi chote cha historia ya kanisa.

Tamaduni za kanisa hazikubaliani kwa kila kitu, utamaduni ambao unategemewa sana ni ule uliofundishwa na kanisa kila mahali na kila nyakati. Utamaduni wa dhehebu unaweza kuzingatiwa, lakini si kwa kiwango cha mamlaka kama utamaduni wa kanisa la ulimwengu mzima.

Mungu anazungumza kupitia utamaduni ili kutusaidia sisi kuelewa neno lake. Kama tafsiri yako inatoa maana ya andiko ambayo hakuna mwingine yeyoye aliyewahi kuiona, lazima ufikirie kwamba umekosea!

---

[33] Kielelezo hiki kimechukuliwa kutoka katoka weblog ya Danny Coleman: https://dannycoleman.blogspot.com/2013/02/quadrilateral-lenses.html. Picha ya Biblia na Wolfgang Eckert kutoka Pixabay, imechukuliwa kutoka https://pixabay.com/illustrations/a-book-bible-literature-pages-6402285/.

**Lenzi ya 2: Mantiki**

Mantiki ni lenzi ya pili ambayo tunatumia. Lenzi hii inauliza, "Uelewa wa kimantinki wa andiko hili ni nini?" Lenzi ya mantiki inatutaka sisi kutumia akili zetu kuelewa kile tunachokisoma katika maandiko. Inatambua kwamba maandiko yanaweza kueleweka kwa kutumia akili zetu. Tunatumia mantiki kuelewa maandiko; hata hivyo; hatupaswi kuukataa ukweli wa Biblia kwa sababu tu hatuwezi kutumia mantiki kuuthibitisha kwamba ni kweli. Watu wengi wanakataa rekodi za Biblia za miujiza kwa sababu wanafikiri kwamba miujiza ni kinyume cha uelewa wa kimantiki. Hata hivyo, miujiza si kinyume cha mantiki kwa sababu kimantiki tunaelewa kwamba Mungu anazo nguvu za kufanya miujiza.

Baadhi ya wakristo wanapinga matumizi ya mantiki; wanasema kwamba akili zetu katika anguko haziwezi kutumika kuelewa Neno la Mungu. Ni kweli kwamba wanadamu wana mipaka katika uwezo wao wa akili. Hata hivyo, Paulo mara kwa mara ameomba kutmia mantiki anapoleta hoja zake. Katika Warumi, kwa mfano, Paulo anauliza mfululizo wa maswali ambayo yanawaongoza wasomaji wake katika uelewa wa kweli kuu kuhusiana na wokovu. Wakati mantiki na akili zetu si mamlaka ya mwisho, hatuwezi kupuuza maana za kimantiki za maandiko.

**Lenzi ya 3: Uzoefu**

Uzoefu ni lenzi ya mwisho. Lenzi hii inauliza, "Je, uelewa wangu unashabihiana na uzoefu wa wakristo wengine?" Uzoefu binafsi haupaswi kuaminiwa zaidi ya kweli kuu. Hata hivyo, uzoefu ni wa thamani sana endapo utasawazishwa na utamaduni na mantiki.

Kila lenzi hizi ni muhimu. Kana tunatumia utamaduni pekee, tutaangukia katika makosa ya kanisa la Rumi ambalo linayachukua mafundisho ya kanisa kama yako sawasawa na maandiko kimamlaka. Kama tutatumia tu mantiki, tutaangalia akili kama mamlaka ya mwisho. Endapo tutatumia uzoefu pekee, tafsiri zetu zitakuwa na mipaka na zitategemea hisia za mtu binafsi, mtazamo, na mawazo ya watu. Lenzi hizi ni njia za sisi kuelewa maandiko, lakini hazitakiwi kutumika katika namna ambayo inakinzana na mamlaka ya maandiko.

**Mfano**

"Kwa hiyo nampigia Baba magoti… mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu" (Waefeso 3:14, 19).

Paulo anaomba kwamba Waefeso wakue sana katika mahusiano yao ya ndani na Mungu. Anaomba kwamba wapate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu. Tunapata nini tunaposoma maombi haya kupitia lenzi hizi tatu?

**Utamaduni**. Wakristo wa vizazi vyote wamefundisha kwamba Mungu ameahidi kuwatakasa kabisa waamini. Wakristo hawajaweza kukubaliana na undani wa kina wa taarifa uhusiana na namna ambavyo Mungu analikamilisha kusudi hili ndani ya waamini, lakini katika nyakati

zote za historia ya kanisa, wakristo wa historia mbalimbali wamekubaliana kwamba Mungu anawaita Watoto wake katika mahusiano ya ndani sana na yeye.

Katika karne ya pili, Irenaeus aliandika kwamba Kusudi la Mungu kwetu ni "kwamba tufanywe katika sura na mfano wa Mungu."[34] Irenaeus aliamini kwamba kila mwamini anaweza kujazwa na ukamilifu wa Mungu. Katika karne ya nne, waandihi wa mashariki kama vile Gregory wa Nyssa alifundisha kwamba wakristo wanatakiwa zaidi na zaidi kujazwa na ukamilifu wa Mungu. Katika karne ya 17, mkatoloki wa Kifaransa Francois Fenelon aliandika kwamba, kupitia nguvu ya neema ya Mungu, tunaweza kuishi "kama Yesu alivyoishi, kufikiri kama alivyofikiri...."[35] Kupitia neema ya Mungu, tunaweza kufanywa katika mfao wake.

**Mantiki**. Tunapozingatia maombi ya Paulo, akili zetu zinauliza, "Je, tafsiri yangu ya maombi haya ni sawasawa na maandiko mengine?" Je, ni mantiki kutafsiri maombi haya kama ahadi ya Maisha ya ndani sana kwa wakristo? Kwa kuangalia maandiko mengine, tunaona kwamba Warumi 12:1, 1 Wathesalonike 5:23, na maandiko mengine yanashauri Maisha ya ndani sana ambayo yapo kwa ajili ya waamini. Uhalisia wa kujazwa na utimilifu wote wa Mungu ni wa kimantiki.

**Uzoefu**. Uzoefu wa wakristo wengi wakubwa katika kipindi chote cha historia kinaonesha njaa ya kuwa na Maisha ya ndani sana. Kila mkristo aliyejikita anashahuku zaidi na Mungu. Shuhuda za wakristo wakubwa zinaoesha kwamba njaa hii ilitimizwa kwa neema ya Mungu.

### Maswali ya Kuuliza wakati Unafikiri Kuhusiana na Vifungu vyenye Mjadala

Kuna vifungu vya maandiko ambavyo vimetafsiriwa tofauti tofauti katikati ya makanisa na wakati mwingine katikati ya marafiki. Unapoangalia kimojawapo kati ya vifungu hivyo, badala ya kutetea tu mawazo yako, fikiria maswali yafuatayo:

- Je, ninaanza na hitimisho? Je, tayari nimeshaamua kile ninachofikiri kwamba andiko linasema kabla sijasoma?
- Je, tafsiri yangu inakinzana na vifungu vingine vya maandiko?
- Je, vifungu vingine vinatoa maana ya wazi ya kifungu hiki?
- Je, tafsiri yangu inajikita katika ujumbe uliofichwa, au ninajaribu kutafsiri kifungu katika namna wazi kwa kadiri inavyowezekana?
- Je, kifungu hiki kinatoa agizo? Kama ndivyo, kuna ahadi gani ambayo inaoneshwa katika agizo hili?

---

[34] Kama yalivyonukuliwa na William M. Greathouse, *From the Apostles to Wesley* (Kansas City: Beacon Hill Press, 1979), 38

[35] *From the Apostles to Wesley*, 85

- Tamaduni gani ya kanisa la kikristo katika kipindi chote inasema nini kuhusiana na kifungu?
- Uelewa wa wazi na wa kimantiki wa andiko hili ni nini?
- Uzoefu wa wakristo wengine unasema nini kuhusiana na kifungu hiki?

Maswali haya hayakuhakikishii wewe kwamba utaweza kupatana katika tafsiri ya kifungu. Hata hivyo, yanaweza kukusaidia kutafuta maeneo mnayokubaliana. Kama sivyo, maswali yanaweza kukusaidia kutambua sababu ambazo zinawafanya wakristo halisi ambao wamejikita katika mamlaka ya neno la Mungu kutokukubaliana juu ya tafsiri ya baadhi ya vifungu vya maandiko.

## Somo la 8 Dondoo Muhimu

(1) Uelewa wa kanuni za msingi za tafsiri ya Biblia utakusaidia kukuzuia kuja katika hitimisho lisilo sahihi katika kujifunza.

(2) Anza na andiko, na si hitimisho lako. Usiruhusu nadharia zako kukusababisha wewe kupuuza andiko.

(3) Mafundisho ya Maandiko hayakinzani na Mafundisho ya Maandiko. Kama vifungu viwili vinaonekana kukinzana, fikiri kwamba pengine haukuelewa vizuri mojawapo ya kifungu.

(4) Maandiko ni mtafsiri bora wa maandiko. Ruhusu vifungu vilivyo wazi kuelezea vifungu vigumu.

(5) Maandiko yaliandikwa ili kueleweka. Tafuta maana ya kawaida ya andiko.

(6) Maagizo ya Biblia yanaonesha ahadi za Biblia. Mungu anayetupatia maagizo anatuwezesha sisi kutii.

(7) Biblia ina maarifa yote yanayohitajika kwa ajili ya wokovu.

(8) Tunaangalia maandiko kupitia lenzi tatu ambazo zinatusaidia sisi kuelewa neno la Mungu:

- Utamaduni: uelewa wa wakristo wengine katika kipindi chote cha historia
- Mantiki: uelewa wa kimantiki wa andiko
- Uzoefu: uzoefu wa kiroho wa wakristo

# Somo la 9
# Matumizi

## Malengo ya Somo

(1) Kuwa makini na mibadala hasi ya matumizi ya kibiblia.

(2) Fuata mchakato wa kuhamisha kutoka tafsiri kwenda kwenye matumizi ya andiko.

(3) Fahamu maswali muhimu ya kuuliza ili kupata matumizi ya andiko.

(4) Fanyia mazoezi hatua hizi kwenye vifungu vya maandiko vilivyochaguliwa.

## Utangulizi

► Jadili uhusiano kati ya **tafsiri** na **matumizi** katika ujifunzaji wako wa Biblia wa sasa. Unapohubiri au unapofundisha kipi ni rahisi: kutafsiri andiko au kutumia katika ulimwengu wa leo? Unapojifunza andiko au unaposikiliza mahubiri, Je, unaweza kupata matumizi katika maisha yako?

Amani alisema, "Mchungaji, tunaweza kukutana? Nina swali kubwa kuhusu Biblia" Baadae katika juma lile, mchungaji alikutana na Amani na waliangalia vifungu mbalimbali ambavyo vilizungumzia suala ambalo alilipitia Amani. Baada ya dakika chache, Amani alifunika Biblia yake na kusema, "Ngoja niwe muwazi. Tayari ninajua Biblia inasema nini lakini sitaki kufanya hivi. Ni ngumu sana kwangu."

Tatizo la Amani halikuwa tafsiri, tatizo lilikuwa matumizi. Haitoshi kuangalia tu nini andiko linasema na kutafsiri maana yake ni lazima tulitumie katika maisha yetu. Mara nyingi sana, kujfunza Biblia huishia kwenye hatua ya tafsiri.

> "Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo."
>
> - Yakobo 1:23-24

Tunaanza kwa kuchunguza andiko linasema nini; tunaendelea kwa kutafsiri linasema nini; lazima tuishie kwa kulitumia kwenye maisha yetu. Tunaweza kufupisha mchakato huu kwa maswali matatu:

- Andiko linasema nini? (Uchunguzi)
- Andiko linamaanisha nini? (Tafsiri)
- Ni kwa namna gani andiko linafanya kazi katika maisha yangu? (Matumizi)

## Mbadala wa Matumizi

Mzaburi aliandika kuwa, mtu ambaye anapendezwa na sheria ya Bwana na kuitafakari sheria yake, atakuwa "kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda

yake kwa majira yake" (Zaburi 1:2-3). Shetani anajaribu kutuweka nje na neno la Bwana. Anafahamu kuwa tutadhoofika na kufa kiroho kama hatutajilisha neno la Mungu.[36]

Endapo hatatutoa nje na neno la Mungu, Shetani atajaribu kutufanya tusitumie ukweli huo katika maisha yetu. Kwa kadiri ambavyo hatutumii neno la Mungu, hatutazaa matunda. Endapo shetani hataweza kutufanya tusisome Biblia, atatujaribu ili kukubali mbadala wa matumizi.

**Tafsiri inakuwa mbadala wa Matumizi**

Inawezekana kujifunza maandiko kwa makini na kupata maana pasipo kuweka katika matendo. Daudi aliposikia hadithi ya Nathani kuhusu tajiri aliyeiba kondoo wa masikini, alijibu kwa tafsiri sahihi. "…Aishivyo BWANA, mtu huyo aliyetenda jambo hili, hakika yake astahili kufa; naye atamrudishia yule mwana-kondoo mara nne, kwa sababu ametenda neno hili, na kwa sababu hakuwa na huruma" (2 Samweli 12:5-6).

Tafsiri ya Daudi ilikuwa sahihi. Alijibu kwa jina la Bwana akisisitiza haki, alihitaji fidia. Hakuna anayeweza kuipinga tafsiri ya Daudi, lakini Daudi alishindwa kuutumia mfano katika maisha yake. Nabii ndiye alifanya matumizi, "Wewe ndiwe mtu huyo" (2 Samweli 12:7).

Hii ni hatari ya kipekee kwa wahubiri na waalimu. Tunaweza kufundisha maandiko kwa wengine wakati tukipuuza kutotii kwetu wenyewe. Yakobo alionya kuhusu tafsiri pasipo utii. "Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi" (Yakobo 4:17). Baada ya kuwa tumetafsiri maandiko sawasawa, hatupaswi kushindwa kuyaweka katika vitendo. Hatupaswi kufanya tafsiri kuwa mbadala wa matumizi.

**Utii Kwa Sehemu unakuwa mbadala wa Utii Kamilifu**

Inawezekana kujifunza kifungu cha maandiko, kutambua maana yake, na kutafuta matumizi ya baadhi ya maeneo pasipo kuruhusu kutubadilisha kikamilifu. Tunaweza kutafuta baadhi ya maeneno ambayo tutatii andiko, lakini tunaweza kupuuza maeneo ya ndani na muhimu kabisa ya kutotii katika maisha yetu.

Pengine tumekuwa kukijifunza Waefeso 4:29, "Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia." Katika hatua ya matumizi, tunapima mahusiano yetu ya umuhimu. Tunauliza:

- "Je, mahubiri yangu yanalijenga kusanyiko langu?" "Ndio; Mimi ni mchungaji mwaminifu."
- "Je, ninatumia maneno ya kujenga kwa watoto wangu?" "Ndio; Mimi ni mzazi mwenye upendo."

---

[36] Nyenzo katika somo hili zimechukuliwa kutoka Howard G. Hendricks na William D. Hendricks, *Living by the Book* (Chicago: Moody Publishers, 2007).

- "Je, ninamjenga mwenzi wangu?" "Hapana; mara nyingi nina mtazamo hasi katika majibu yangu."

Mawasiliano yako na mwenzi wako ni mahali ambapo Roho wa Mungu anataka kukubadilisha. Shetani anakujaribu ili uweke mbadala wa utii katika maeneo mengine yanayobadilisha maisha, kuhusiana na matumizi ya andiko hili katika uhusiano wako na mwenzi wako. Anakujaribu kukubali utii kwa sehemu badala ya kujitoa kwa utii kamilifu.

**Tunafanya Visingizio kuwa Mbadala wa Toba**

Mwana sheria alimuuliza Yesu, "Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" (Luka 10:25). Mwanasheria alikuwa tayari anafahamu jibu: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako" (Luka 10:27).

Mwanasheria aliyaelewa maandiko "Naye akitaka kujidai haki, alimwuliza Yesu, Na jirani yangu ni nani?" (Luka 10:29). Tatizo lake halikuwa tafsiri; tatizo lake lilikuwa matumizi. Mwanasheria alihalalisha ukosefu wake wa upendo.

Pengine Roho wa Mungu anasema na wewe, "Maneno yako hayamjengi mwenzi wako; hayo ni mawasiliano mabovu yanayoharibu." Umesoma neno, umetafsiri neno, sasa ni muda wa kutumia neno. Badala yake, unaweza kufikiri, "mwenzi wangu kila mara ana mtazamo hasi. Kama nina mtazamo hasi, ni kwa sababu mwenzi wangu ana mtazamo hasi. Siyo kosa langu!" Je, umefanya nini? Umeihalalisha tabia yako badala ya kutubu kwa sababu ya wewe kushindwa kulitii neno la Mungu.

**Tunafanya Hisia kuwa Mbadala wa Kubadilishwa**

Yakobo aliandika kuhusu mtu anayesikia neno lakini halifanyii kazi (Yakobo 1:23-24). Wakati mwingine mtu anasikia neno na anaguswa kabisa, lakini anaruhusu mwitikio wa hisia kuwa mbadala wa badiliko la kweli. Kila mchungaji anajua kukatishwa tamaa katika kuhubiri ujumbe juu ya mada fulani, hasa watu wanaposema "Mahubiri yale yalinigusa sana," na kisha kuona mabadiliko yasiyodumu

Huenda unasikia Waefeso 4:29 ikifundishwa kwenye semina ya ndoa. Wakati wa muda wa kuweka ahadi mwishoni mwa semina, unamwambia mwenza wako, "Samahani. Ninataka kuzungumza maneno chanya. Nitafanya vizuri!" Lakini punde, unarudi tena katika tabia za zamani za maneno makali, hasi, na mazungumzo yanayoumiza.

Nini kimetokea? Kulikuwa na mwitikio wa kihisia, na siyo mabadiliko ya kweli. Hii ni hatari, baada ya kushindwa kunakojirudia rudia, tunaamini kwamba mabadiliko hayawezekani. Mwitikio wa kihisia juu ya kweli lazima unaambatana na mabadiliko ya kweli na utii, ambavyo vinawezekana tu tunapojinyenyekeza kwa kazi ya Roho Mtakatifu.

## Hatua za Kutumia Maandiko

Baada ya kumwelezea mtu anayejitazama katika kioo na akasahau jinsi alivyo. Yakobo amwelezea mtu ambaye analitumia andiko katika maisha yake. "Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake" (Yakobo 1:25). Haitoshi kulisikia neno la Mungu, tunatakiwa kulitendea kazi Neno. Kipi ni kinahitajika ili kutendea kazi andiko?

Ili kulitendea kazi kikamilifu Neno la Mungu, unahitaji kufanya mambo matatu.

### Hatua ya 1: Fahamu maana ya Andiko

Ndiyo maana somo kuhusus uchunguzi na tafsiri ni muhimu sana. Iwapo hatufahamu andiko, matumizi yetu hayatakuwa sahihi. Tunaanza hatua ya matumizi kwa kuuliza, "Ni kwa namna gani Wakristo wa karne ya kwanza waliweza kutumia andiko hili katika ulimwengu wao?"

Kwa mfano, Paulo aliandika, "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:13). Baadhi ya waalimu wamelichukulia ndiko hili kama ahadi kwamba tunaweza kupata chochote tunachokihitaji kwa sababu, "Kristo ananitia nguvu." Mwanariadha anatangaza, "Nitashinda mchezo wa leo kwa sababu 'Ninayaweza mambo yote katika Kristo.'" Waponyaji wa kiimani wanawahakikishia wasikilizaji wao, "Kama una imani ya kutosha, utaponywa, kwa sababu 'Unayaweza mambo yote katika Kristo.'" Wahubiri wa mafanikio yasiyo ya kweli wanatangaza, "Mungu anataka kukufanya wewe kuwa tajiri. Unachotakiwa kufanya ni kushirikiana na Mungu. 'Unayaweza mambo yote katika Kristo.'"

Tunapouliza, "Ni kwa namna gani Wakristo wa Filipi walilitumia andiko hili?" Tunagundua kuwa hii haikuwa ahadi ya mafanikio ya kidunia, bali ni ahadi ya kuvumilia kiroho. Paulo alikuwa gerezani kule Rumi; wapokeaji wake walikuwa wanapitia mateso. Hakumaanisha kwamba alikuwa na mafanikio ya kidunia, bali kwamba alikuwa na uwezo wa kuvumilia katika hali zote kwa imani na utii. Paulo alijifunza kuridhika katika hali zote katika Kristo, angeweza kufanya chochote ambacho Mungu alimtaka kufanya. Hii haikumaanisha maisha ya anasa; ilimaanisha kwamba hakupoteza roho ya kuridhika akiwa anapitia magumu.

### Hatua ya 2: Elewa ni kwa namna gani Andiko linatumika katika maisha

Paulo alimuonya Timotheo kwamba ni lazima yeye mwenyewe afahamu kwanza ili aweze kuwahudumia wengine kwa ufanisi. "Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia" (1 Timotheo 4:16). Kwa kadiri Timotheo anavyoweka umakini kwake na kwa mafundisho ayayoyahubiri, ndivyo atakavyo watumikia kwa ufanisi wasikilizaji wake.

Baada ya kufahamu andiko na namna lilivyotumika kwa wasomaji wa kwanza, ni lazima nijifahamu mwenyewe na kuona namna linavyotumika katika ulimwengu wangu. Pengine ninajiangalia mwenyewe na kuona kwamba mara zote sitarajii Mungu kunibariki na

kunisaidia. Wafilipi 4:13 inaniambia kukabialiana na changamoto kwa ujasiri kwa sababu "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."

Sasa matumizi yanakuwa wazi na mahususi. Kama mstari pembeni mwa mstari huu, ninaweza kuandika hivi, "Ukiwa unafanya kazi katika mazingira ambayo yanapinga maadili ya kikristo, nitaiamini neema ya Mungu ili kunitia nguvu kuwa mwaminifu. Ninayaweza mambo yote katika Kristo." Hii imechukua mstari toka karme ya 1 hadi karne ya 21.

Matumizi sahihi ya andiko yanafanya kazi katika ulimwengu halisi. Neno la Mungu linahusiana na maeneo yote ya maisha. Ninapotendea kazi andiko, siulizi, "Ni matumizi gani ya kidini ambayo yapo katika andiko hili?" Badala yake, Ninauliza, "Ni kwa namna gani nitaliishi andiko hili katika maeneo yote ya maisha?"

John Wesley aliandika, "Injili ya Kristo haijui dini yeyote bali jamii; hakuna utakatifu bali utakatifu wa kijamii."[37] Tunaiishi Injili si kama watawa waliotengwa kutoka kwa wengine, bali kama waamini katika mahusiano na wengine. Tunakua katika utakatifu siyo kwa kujitenga na wengine bali ndani ya muktadha wa jumuiya ya kanisa.

Hapo awali, tuliangalia katika Waefeso 4:29. Ninapozingatia matumizi ya mstari huu, ninatakiwa kuutumia katika mahusiano na wakristo wenzangu: "Je, maneno yangu yanamjenga mwamini mwenzangu au yanavunja vunja?" Ninatakiwa kuhusianisha mstari na familia yangu: "Je, mazungumzo yangu yanajenga familia yangu, au yanaondoa nguvu ya ujasiri ya mwenza wangu na watoto?" Ninatakiwa kuhusianisha mstari na kazi yangu: "Je, mimi na mwajiriwa ambaye niazungumza maneno chanya, au ninasambaza mawazo hasi?" Waefeso 4:29 inahusiana na kila eneo la maisha.

Hii ndiyo sababu Paulo aliandika kwamba watumwa ambao wanaishi vema katika mahusiano na bwana zao wanayapamba mafundisho ya Mungu mwokozi wetu katika mambo yote (Tito 2:10). Matumizi sahihi ya kina ya maandiko yatafanya Injili kuwa ya kuvutia kwa watu wanaotuzunguka sisi.

**Hatua ya 3: Tii Maandiko**

Kusudi la juu zaidi la kujifunza Biblia kila siku ni Matumizi. Katika 2 Timotheo 2:3-6, Paulo anaelezea Wakristo kama askali, wanariadha, na wakulima. Picha hizi zinaelezea mtu ambaye anaendelea bila kuchoka ili kufikia lengo. Askali hapumziki wakati wa vita; wanariadha hapumziki katikati ya urefu wa riadha; mkulima hapumziki kulima hadi pale atakapomaliza kazi. Maisha ya Ukristo yanahitaji uvumilivu. "Tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu" (Waebrania 12:1).

Unapojifunza maandiko, uliza, "Je, kuna eneo la maisha yangu ambapo ninahitaji kuutendea kazi ukweli huu?" Mwombe Mungu akusaidie kutumia kweli katika maisha yako kwa

[37] Dibaji na John na Charles Wesley's 1739 toleo ya *Hymns and Sacred Poems.*

utaratibu mzuri uliopangwa. Unapofanya hivi, Mungu atakufunulia kweli zaidi. Na hata utakuwa na shahuku kubwa ya chakula cha kiroho.

Endapo Mungu anazungumza na wewe kupitia Waefeso 4:29 ili kukuonesha kuhusiana na mazungumzo yako, unapaswa kujitoa ili kufanyia mazoezi mazungumzo yanayojenga. Hii inaweza kuwa rahisi endapo unamwomba Mungu akupe fursa kila siku ya kunena neema katika maisha ya mtu fulani. Inaweza kumaanisha kumwomba rafiki unayemwamini akuonye anapokusikia ukitumia mawasiliano yanayoharibu. Hii inaweza kuwa njia ya kutendea kazi Neno la Mungu kila siku.

Chuoni, palikuwa na kijana mmoja ambaye alikuwa anahangaika na majaribu katika maeneo fulani. Tahir alipenda muziki, pamoja na mtindo pamoja na maneno ya wimbo ambayo yangeweza kumjaribu katika udhaifu wake. Tahir alitaka ushindi dhidi ya jaribu, lakini hakuweza kuyatumia maandiko kwa uthabiti katika maisha yake.

Septemba, shule ilikuwa na ibada za uamsho. Tahir angeenda madhabahuni. Angerudi bwenini kwake na kutupa muziki wake ambao si sahihi. Kwa majuma kadhaa, angekuwa na ushuhuda mzuri. Baada ya muda mfupi angevunjwa moyo; Novemba, angesema, "Nimerudi nyuma."

Febriari, shule ingekuwa na kongamano la Biblia. Tahir angeenda mbele madhabahuni. Angezitupa tena rekodi zake na angekuwa na ushuhuda mzuri kwa majuma machache. Kisha, Aprili, angenunua tena baadhi ya muziki na mchakato ungeanza tena!

Tahir alihitaji nini? Tafsiri nzuri? Hapana! Alifahamu maeneo ya udhaifu wake; alifahamu nini Biblia Inasema kuhusiana na kuwa na kutunza akili njema; alifahamu madhara ya baadhi ya muziki katika maisha yake ya kiroho. Tatizo la Tahir halikuwa tafsiri; alitakiwa tu kutendea kazi kile alichokifahamu.

Ni maeneo gani ya matumizi unayotakiwa kuyatendea kazi?

## Mswali ya Kuuliza

Itakuwa na msaada zaidi kuuliza maswali haya matano wakati unatafuta njia za kutendea kazi andiko katika maisha yako.

### (1) Je, kuna dhambi ya kuepuka?

Wakristo wengi hukata tamaa wakati wanapoona kwamba eneo fulani katika maisha yao limeshindwa kufuata matakwa ya maandiko. Mungu anaposema na sisi kupitia neno lake kuhusiana na eneo la dhambi katika maisha yetu hatutakiwi kukata tamaa. Badala yake, tunatakiwa kuwa tayari kulitii neno lake.

### (2) Je, kuna ahadi ya kuidai?

Wakati mwingine matumizi ni kuidai tu ahadi ya Mungu. Tunatakiwa kuwa makini na kutafsiri ahadi kwa usahihi. Baadhi ya ahadi zilikuwa ni kwa ajili ya watu fulani au kwa taifa la iasraeli. Tunatakiwa kuwa makini ili tusiichukue ahadi nje na muktadha. Hata hivyo,

tunapokuwa tumetafsiri kwa umakini ahadi katika muktadha wake na kufahamu kwamba ni ahadi kwa waamini wote, tunaweza kuzidai ahadi hizo katika maisha yetu.

**(3) Je, kuna hatua ya kuchukua?**

Uliza, "Nifanye nini kwa sababu ya kifungu hiki cha andiko. Ni kweli gani ambayo kifungu hiki kinafundisha? Je, kinanionya kuhusiana na fundisho langu lisilo sahihi? Je, ninahitaji kubadilisha kufikiri kwangu ili kuwa sawa na maandiko? Ninatakiwa kufanya nini kwa sababu ya andiko hili?"

Mfano mmoja ni maombi. Tunaposoma maombi ya Daudi, Paulo, Nehemia, na Yesu, tunaona kielelezo kwa ajili ya maisha yetu ya maombi. Ni kujifunza vizuri kiasi gani kama kuyachukua maombi ya Paulo au Yesu na kuyafanya yangu! Ninaposoma, ninaweza kuchukua hatua katika kutendea kazi kwa kuchukua maombi ya hayo katika maisha yangu.

**(4) Je, kuna Agizo la kutii?**

Mara nyingi sehemu ya pili ya nyaraka za Paulo zinaundwa na maagizo. Maagizo haya mara nyingi ni rahisi na ya moja kwa moja. Wakati mwingine Wakristo wanatafuta kweli kuu, huku wakipuuza matumizi rahisi ya kile ambacho tayari wanafahamu!

Mtu mmoja aliandika kuhusiana na kutafuta kweli wa ndani zaidi huku ukipuuza ukweli ulio wazi. Alieleza kuhusu mafunzo yake ya kwanza juu ya Kiyunani cha Agano Jipya. Katika Mathayo 16:24, Yesu alisema, "Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate." Kiyunani cha asili hakina maana ya tofauti, inayoshangaza. Maana hii ni sawa kabisa na kile inachomaanisha. Siyo ngumu kuelewa maana. Badala yake, ni vigumu kutii.[38]

Wakati mwingine kinachohitajika ni rahisi sana, "Ndiyo, Bwana. Nitatii."

**(5) Je, kuna mfano wa kufuata?**

Maandiko mengi yanajumuisha wasifu wa watu. Tunapososma wasifu, tunauliza, "Je, kuna mfano wa kufuata?"

Tunaposoma kuhusu Abrahamu katika Mwanzo 18, tunaweza kufuata kielelezo cha Abrahamu kwa kuuombea ulimwengu wetu. Mwalimu alikuwa anafundisha Nigeria. Nigeria imekuwa inasumbuliwa na mgogogro kati ya Waislamu na Wakristo. Mmoja wa wanafunzi akawaomba wanafunzi wenzake, "Kwa nini tunagombana na Waislamu kuliko tunavyowaombea? Je, tunaamini kwamba Mungu anaweza kuwaleta katika wokovu? Kama ni hivyo, tunatakiwa kufuata kielelezo cha Abrahamu na kuwaombea ili wapate wokovu!" haya ni matumizi.

---

[38] Imechukuliwa kutoka Andy Crouch, "Information and Formation" katika *Christianity Today,* Machi 2014. Inapatikana mtandaoni katika https://www.christianitytoday.com/ct/2014/march/information-and-formation.html.

## Weka Katika Matendo

Tumefanya uchunguzi kutoka katika Warumi 12:1-2. Tumejifunza neno juu ya maneno muhimu katika mistari hii. Tumejifunza muktadha wa kihistoria, kiutamaduni, na kibiblia ili kutafsiri kwa usahihi ujumbe wa Paulo.

Sasa tupo tayari kwa ajili ya hatua muhimu sana. Ni kwa namna gani utatendea kazi Warumi 12:1-2 katika maisha yako?

► Rejea tena nakili juu ya Warumi 12:1-2 ambazo ulizitengeneza hapo kabla katika somo lililopita. Kisha orodhesha mambo matatu mahususi utakayoyatenda ili kufanyia kazi andiko katika maisha yako.

► Endapo unajifunza somo hili katika kundi, shirikisha matumizi yako katika kundi. Endapo mtakuwa mnakutana tena hapo mbeleni, tengeneza uwajibikaji. Mfanye mtu awajibike na omba kundi kufuatilia kwa kukuuliza wewe namna unavyofanya matumizi yako.

## Hitimisho

Kozi hii ni kuhusu kutafsiri Biblia ili kwamba tuweze kuwafundisha wengine. Huu ndio wito tulioitiwa kama waalimu wa neno la Mungu. Hata hivyo, kuna hatari katika hili. Kama hatutakuwa makini, tunaweza kujifunza Biblia kwa ajili ya kuhubiri na kufundisha tu. Tunaweza kushindwa kuutumia ukweli wa Biblia katika maisha yetu.

Kujifunza Biblia si kwa kusudi la kujifunza na kufundisha. Neno la Mungu linawea kulinganishwa na chakula kwa ajili ya kutujenga kimwili. Kula chakula kuna matokeo ya kila siku na ya muda mrefu. Hauwezi kushusha kiwango cha cholesterol yako kwa mlo mmoja wenye afya, haujengi afya ya kiroho kwa kujifunza Biblia siku moja. Inachukua mlo wa wenye afya wa mara kwa mara ili kujenga afya ya kimwili, na itachukua mlo wa muda mrefu wa neno la Mungu ili kujenga nguvu za kiroho. Lakini bado, mlo wa siku moja wa neno la Mungu ni muhimu kwa chochote utakachokutana nacho siku hiyo, kama ambavyo chakula cha asubuhi kinavyokusaidia katika kazi ya siku husika.

Kama wachungaji, waalimu, na viongozi wa kanisa, hatupaswi kusahau kwamba maisha yetu ya kiroho ni lazima yajengwe kila siku. Katika juhudi zetu za kuwafundisha wengine, kamwe tusisahau kuilisha mioyo yetu na mkate wa neno la Mungu. Ni hadi pale tu tutakapojijenga wenyewe ndipo tutakuwa na nguvu ambayo tunahitaji ili kuhudumia watu wa Mungu.

Paulo alikuwa anafahamu hatari hii. Aliandika kuhusiana na hofu yake kwamba asije kukataliwa baada ya kuwahubiri wengine (1 Wakorintho 9:27). Ni jambo baya sana sisi kuwafundisha wengine wakati tunaikataa neema ya Mungu katika mioyo yetu. Jifunze ili kufundisha wengine, lakini pia jifunze ili kumsikia Mungu akizungumza na moyo wako.

## Weka katika Matendo

► Luka 14:25–17:10 ni mfululizo wa mifano na maelekezo. Yesu anaposafiri kwenda Yerusalemu kwa mara ya mwisho, alitoa maelekezo ya mwisho kwa wanafunzi wake. Unaposoma maelekezo ya Yesu, tafuta matumizi mahususi kutoka katika mistari hii. Uliza:

- Je, kuna dhambi ya kuepuka?
- Je, kuna ahadi ya kuidai?
- Je, kuna hatua ya kuchukua?
- Je, kuna Agizo la kutii?
- Je, kuna mfano wa kufuata?

## Somo la 9 Dondoo Muhimu

(1) Haitoshi tu kwa sisi kutafsiri kwa usahihi Neno la Mungu; tunapaswa kulitendea kazi katika maisha yetu ya kila siku.

(2) Shetani anatujaribu sisi ili kuwa na mbadala wa matumizi:

- Tafsiri inakuwa mbadala wa Matumizi
- Utii Kwa Sehemu unakuwa mbadala wa Utii Kamilifu
- Tunafanya Visingizio kuwa Mbadala wa Toba
- Tunafanya Hisia kuwa Mbadala wa Kubadilishwa

(3) Ili sisi kufanyia kazi maandiko katika maisha yetu, tunatakiwa kufuata hatua hizi tatu:

- Fahamu maana ya andiko.
- Elewa ni kwa namna gani andiko linatumika katika maisha.
- Tii Maandiko.

(4) Ili kupata njia za kutendea kazi maandiko katika maisha yako, uliza maswali haya:

- Je, kuna dhambi ya kuepuka?
- Je, kuna ahadi ya kuidai?
- Je, kuna hatua ya kuchukua?
- Je, kuna Agizo la kutii?
- Je, kuna mfano wa kufuata?

## Somo la 9 Zoezi

Katika Somo la 1, ulichagua kifungu cha maandiko ambayo utayasoma wakati wote wa kozi hii. Kwa kutumia nakili ambazo umeziandaa katika Uchunguzi na tafsiri, tengeneza orodha ya hatua ya matumizi ya kivitendo kwa ajili ya andiko unalojifunza.

# Somo la 10
# Kufanyia kazi Kujifunza Kifungu

## Malengo ya Somo

(1) Fanyia kazi matumizi ya hatua za tafsiri kwa vifungu vilivyochaguliwa.

(2) Andaa andiko au mawasilisho ya mdomo ya uchunguzi wako wa kina wa kifungu cha andiko.


## Utangulizi

*Angalizo kwa kiongozi wa darasa: Tunza muda darasani kwa ajili ya kufanyia kazi shughuli katika somo hili, hata kama kitahitajika kipindi zaidi ya kimoja cha darasa.*

Katika kozi hii, tumeangalia hatua za kutafsiri Biblia: Uchunguzi, Tafsiri, na Matumizi. Tumejifunza juu ya kuepuka makosa yaliyozoeleka katika kutafsiri Biblia. Tumejifunza kanuni muhimu kwa ajili ya kujifunza maandiko. Tumefanyia mazoezi kila hatua. Katika somo hili, kwanza tutapitia tena mchakato wote. Kisha darasa zima kwa Pamoja litajifunza vifungu toka Agano la Kale na Jipya kwa kutumia mchakato huu. Pia uatafanyia mazoezi stadi kibinafsi. Kisha utakamilisha mradi wa kozi uliouanza katika Somo la 1.

Kwa kuanza, pitia tena picha hapa chini:

**Kutafsiri Biblia**[39]




| | | |
|---|---|---|
| **1** | Mji wao | Ujumbe wa kwanza wa maandiko |
| **2** | Mto | Tofauti za kihistoria-kiutamaduni ambazo zinatenga ulimwengu wetu na ulimwengu wa kale |
| **3** | Daraja | Kanuni zinazofundishwa katika andiko |
| **4** | Ramani | Mahusiano na Agano Jipya (kwa ajili ya vifungu vya Agano la Kale) |
| **5** | Mji wetu | Matumizi ya kanuni katika ulimwengu wetu |

Sehemu inayofuata ya somo hili linarudia tena mchakato wote wa kutafsiri Biblia. Wakati wa kila hatua ya mchakato wa tafsiri, watafsiri wanatakiwa kuuliza maswali ambayo yatawaongoza katika mahitimisho sahihi. Maswali haya yana msingi katika kanuni za kutafsiri.

Maswali yanayotakiwa kuulizwa kwenye kila hatua katika mchakato yameorodheshwa. Mifano inaonesha namna ya kutumia maswali na kwa nini ni ya muhimu kwa ajili ya tafsiri sahihi.

Mkusanyiko wa maswali yanatakiwa kuchukuliwa kama boksi ya vifaa kwa ajili ya tafsiri. Kama ambavyo mjenzi hatahitaji kutumia kila kifaa katika mradi wa jengo fulani, sio kila

[39] Picha: "Interpreting the Bible" Imechorwa na Anna Boggs, inapatikana katika https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52377290578, licensed under CC BY 2.0. Concept from J. Scott Duvall na J. Daniel Hays, *Grasping God's Word* (Grand Rapids: Zondervan, 2012)

swali hapa litatumika kwa kila kifungu. Swali linaweza kuchukuliwa kuwa halihitajiki endapo majibu yake yanaonekana hayawezi kuwa halisi au endapo yanaonekana kutochangia chochote.

## Uchunguzi: Kuelewa Muktadha wa Kihistoria-Kiutamaduni

### Mwandishi

- Mwandishi alikuwa nani?
- Wajibu wake ulikuwa nini?
- Uhusiano wake na wapokeaji ulikuwaje?

1 Timotheo 5:20: "Wale wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote..."

Mtume Paulo mwandishi wa 1 Timotheo, alikuwa mlezi wa Timotheo. Hili lilkuwa ni agizo ambalo Paulo alikuwa anamuelekeza Timotheo, ambaye alikuwa mchungaji kijana.

Kuelewa mambo haya kunatusaidia sisi kutambua kwamba maelekezo ya Paulo hayawezi kutumika kwa kila mkristo.

### Wapokeaji wa Kwanza

- Walikuwa ni nani?
- Walikuwa na tabia gani?

Filemoni alikuwa ni mwamini binafsi aliyeandikiwa.

Waebrania iliandikwa kwa ajili ya Wayahudi waliokuwa wanateswa.

### Mazingira

- Ni wakati gani katika historia ya wokovu andiko hili liliandikwa?

2 Mambo ya Nyakati 7:14: "Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao."

"Watu wangu" linarejelea taifa mahususi ambalo lilikuwa watu wa Mungu. Ahadi "kuiponya nchi yao" si lazima iwe na matumizi ya moja kwa moja kwa katika kanisa.

- Mazingira ya utamaduni yalikuwa nini? Kama inawezekana, tumia kamusi ya Biblia kusoma utamaduni wa asili. Hii itakusaidia kulinganisha/kukinzanisha utamaduni wao na wetu.

2 Wakorintho 13:12: "Salimianeni kwa busu takatifu."

Kusalimiana kwa busu takatifu ulikuwa ni utamaduni wa kawaida baina ya wakristo wa wakati ule.

- Yapi yalikuwa ni matukio yanayotokea kwa sasa?
- Hali ndani ya kanisa ilikuwaje? (Vifungu vya Agano Jipya pekee)

**Uchunguzi: Kuelewa Muktadha wa Uandishi**

Angalia tabia za aina ya fasihi ya kitabu na kifungu.

- N aina gani ya fasihi ya kitabu/kifungu hiki?
- Nini ni tabia za aina hii ya fasihi?

  Zaburi 124:4-5:

  - Aina ya Fasihi: Ushairi
  - Tabia: Usambamba

  Ufunuo 12:3:

  - Aina ya Fasihi: Fasihi ya kiapokaliptiki
  - Tabia: Wanyama ni Alama

**Uchunguzi: Kuelewa Kusudi Kuu la Kitabu**

- Kusudi la uandishi lilikuwa nini? Tafuta kile ambacho mwandishi anasisitiza au ambacho mwandishi ameonesha wasiwasi, kutoa maelezo, au changamoto kwa wasomaji.

  1 Wakorintho 7:1: "Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika…"

  1 Wakorintho iliandikwa ili kujibu barua ambayo kanisa la Korintho lilimwandikia Paulo, likimuuliza maswali.

- Ni nini kinaonekana kuwa tatizo/mahitaji ya wapokeaji?

  1 Wakorintho 1:10: "Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja."

  *Mgawanyiko* imejadiliwa mara kwa mara katika barua.

- Mwandishi alikuwa akiwaambia nini wapokeaji? Maagizo yeyote yanayotolewa baada ya Uchunguzi wa mwandishi ni dalili za wazi za kile ambacho mwandishi alitarajia. Yanaonyesha jinsi tunavyopaswa kutumia kifungu.

**Uchunguzi: Kutambua Mwanzo na Mwisho wa Kifungu**

Mara nyingi, lakini si mara zote, mgawanyo wa sura utaashiria mwisho au mwanzo wa kifungu. Mara kwa mara, sura nzima inaweza kuunda kifungu kimoja. Wakati mwingine, migawanyo ya sura huwekwa kimakosa na haipaswi kutumiwa kama mgawanyiko wa vifungu. Tazama mabadiliko ya mada, ambayo kwa kawaida yana alama zinazoonesha mpito. Ukijaribu kuweka mambo mengi sana katika kifungu, kifungu hakitakuwa na mada

moja kuu. Ikiwa hutajumuisha vya kutosha katika kifungu, kifungu hakitakuwa na mawazo kamili.

- Ni mistari gani inayijumuishwa katika kifungu?

  2 Wakorintho 7:1: "Kwa kuwa tuna ahadi hizo, wapenzi wangu…"

  Sehemu hii ya kifungu inapatikana mwishoni mwa sura ya mwisho, 2 Wakorintho 6:14-18.

  Isaya 52:13-15 iko katika kifungu kile kile kama Isaya 53.

**Uchunguzi: Kuelewa Nanma Kifungu Kinahusiana na Kitabu**

- Je, ni simulizi ambayo inaingia katika wazo kuu kubwa?

  Waamuzi 17:5: "Basi mtu huyo Mika alikuwa na nyumba ya miungu, naye akafanya naivera, na kinyago, akamweka wakfu mmoja miongoni mwa wanawe, akawa kuhani wake."

  Mtu mmoja alikuwa na sanamu yake na kuhani wake. Mstari hu una mistari inayozunguka simulizi ya Waamuzi 17-18 inaelezea wazo la jumla la Waamuzi, "…kila mtu alifanya hayo aliyoyaona kuwa ni mema machoni pake mwenyewe" (Waamuzi 17:6, Waamuzi 21:25).

- Je, kinatoa theolojia kwa ajili ya matumizi ya baadae?
- Je, ni matumizi ya kifungu kilichipita katika kitabu?

  Waefeso 4-6 kimsingi ni matumizi ya vitendo ya theolojia inayofundishwa katika Waefeso 1-3. Katika Waefeso 4:1 neno "Kwa hiyo" linaonyesha daraja kutoka kufundisha theolojia hadi kufundisha matumizi ya vitendo.

  Waefeso 4:1: "Kwa hiyo nawasihi...mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa…"

**Uchunguzi: Angalia Muundo wa Kifungu**

- Je, baadhi ya nyenzo ni maandalizi ya kifungu kikuu?

  Marko 2:2: "…Wakakusanyika watu wengi, isibaki nafasi hata mlangoni…."

  Taarifa hizi zinamuandaa msomaji kusikiliza kuhusiana na mtu aliyeshushwa toka darini.

- Ni maneno gani yanatumika kuunganisha mawazo kimpangilio?

  Kujirudia kwa matumizi ya *ndipo* katika Mathayo 24.

- Je, swali au tatizo limewasilishwa?

  Warumi 6:1: "Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?"

- Ni maneno gani yaliyotumika kuunganisha mawazo kimantiki?

  Kujirudia kwa matumizi ya *Kwa* katika Warumi 6 kuonesha mfuatano wa kimantiki.

- Je, ulinganifu au ukinzani umetumika?

  Warumi 6:19-20: "…Kwa kuwa kama mlivyovitoa viungo vyenu vitumiwe na uchafu na uasi mpate kuasi, vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki mpate kutakaswa…"

  Ukinzani baina ya utumwa wa kale (kwa uchafu na uasi) na utumwa wa sasa (kwa haki).

- Je, kuna marudio au matumizi ya maneno yaleyale?

  Warumi 6 inarudia rudia/maneno yaleyale: kufa, kuifia, aliyekufa, kifo, kusulubishwa, kuzikwa, ubatilike.

  Maneno haya yote ni maneno yanayoonesha hitimisho.

- Je, kuna orodha yeyote?

  1 Timotheo 4:12: "…bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi."

- Ni vielelezo au lugha gani za picha ambazo zimetumia?

  Warumi 6 inatumia kusulubiswa kama tamathali ya semi.

- Je, njia ya kufikia lengo umeelezwa?

  Warumi 8:13: "…kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi."

  "kwa Roho" – njia

  "mkiyafisha matendo ya mwili" – Lengo

  "mtaishi" – Lengo kuu

- Je, kuna sababu za matamko yaliyotolewa au madai?

  Kujirudia kwa matumizi ya *Kwa* yanapelekea katika mafafanuzi ya matamko katika Warumi 6.

- Je, kuna kilele au sehemu kuu? Hili ni swali mahususi kwa ajili ya simulizi

  Katika mfano uliotolewa katika Mathayo 21:33-41, mistari ya 38-39 ni kilele.

- Je, chanzo na matokeo vimeelezewa?

  Wagalatia 5:16: "Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili."

Chanzo: “Enendeni kwa Roho”

Matokeo: “hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.”

- Je, sehemu hii inakaa kama ufupisho wa kile kilichopita au kinachofuata?

  Waamuzi 2:11-23 inafupisha kitabu cha Waamuzi.

  Waefeso 5:1 inafupisha Waefeso 4:25-32.

- Je, sehemu hii inanukuu au inarejea andiko lingine? Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi wametumia nukuu au vielelezo kutoka Agano la Kale.

  Warumi 12:1: “Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.”

  Katika mtari huu, *dhabihu* ni neno la picha ambalo linarejelea kitu katika Agano la Kale.

**Uchunguzi: Chunguza na Jifunze Maneno Muhimu**

- Ni maneno gani muhimu katika kifungu?

  Maneno muhimu kutoka katika 1 Wakorintho 2:14-15:

  - *Mwanadamu wa tabia ya asili*
  - *Mtu wa rohoni*

  Maneno muhimu kutoka katika Warumi 8:

  - *Mwili*
  - *Roho*

- Yanamanisha nini katika muktadha huu? Jifunze kila neno kwa kila moja.

**Uchunguzi: Chunguza Kila Tamko**

- Lina maana gani? Rudia kwa maneno yako kile ambacho tamko linasema.
- Kwa nini limejumuishwa, na kwa nini limewekwa hapa? Fikiria ingekuwaje endapo tamko hilo lisingekuwa hapo.

**Tafsiri: Fupisha Ujumbe**

Kwa kuwa sasa umechunguza kwa makini taarifa za kina na mstari au andiko, fupisha ujumbe wa mwandishi kwa wapokeaji wa kwanza. Ufupisho wa **mstari** unaweza kuwa wa **sentensi moja**. Ufupisho wa **kifungu** unaweza kuwa **sentensi kadhaa** au hata **vifungu kadhaa.**

Lengo la hatua hii ni kutaja kile ambacho mwandishi anakisema kwa wasomaji wake wa kwanza. Huu sio wakati wa kuwa na mawazo na ubunifu wako. Unaweza kuwa mbunifu

wakati unatengeneza njia za kuwasilisha ujumbe katika mahubiri au mafundisho, lakini kwa sasa unajaribu kutafuta maana ya andiko. Maana inatakiwa kutoka katika maandiko na sio katika mawazo yako.

- Ni nini mwandishi anajaribu kukisema kwa wapokeaji waliokusudiwa?

  1 Wakorintho 1:10-13 inaweza kufupishwa namna hii: "Tafadhali pataneni katika mafundisho yenu na ushirika na msigawanyike na kuwa makundi. Nimesikia kutoka katika nyumba ya Kloe kwamba mnabishana. Mnachagua kuwafuta viongozi mbalimbali, lakini ni Kristo tu ndiye alikufa kwa ajili yenu."

Angalia ufupisho wako. Fikiria maswali yafuatayo Pamoja na nyezo ambazo zimepatikana kutoka katika Uchunguzi ulioufanya:

- Je, nimezingatia vya kutosha hali ya mazingira ya awali ya uandishi?
- Ni nini kinaonekana kuwa nia na makusudi ya mwandishi kuandika kifungu hiki?
- Je, tafsiri yangu ya kifungu inalingana na dhana kuu ya kitabu?
- Je, tafsiri yangu inakipa kifungu jukumu lake sahihi katika kitabu?
- Je, msisitizo wa muundo wa kifungu unaendana na muhtasari wangu?
- Je, maana ya kila tamko ndani ya kifungu linaunga mkono muhtasari wangu?
- Je, ninatafsiri ipasavyo matumizi ya mwandishi ya maneno muhimu?

## Tafsiri: Taja Kanuni

Katika kifungu, tafuta kanuni moja inayotumika nyakati zote na watu wote. (Kifungu kinaweza kufundisha kanuni kadhaa, lakini kwa sababu ya kufanyia mazoezi, chagua moja.) Itaje katika sentensi moja.

Moja kati ya kanuni zinazopatikana katika Waefeso 4:25: "Sema kweli katika mawasiliano yote."

Kisha angalia ili kuhakikisha kwamba kanuni yako inaonesha kwa usahihi ujumbe wa asili wa andiko:

- Kanuni hii imefundishwa kwa uwazi katika andiko?
- Kanuni hii inapatana na maandiko mengine?
- Kanuni hii ni kweli kwa nyakati zote kwa watu wote?

Husianisha kanuni na kweli nyingine:

- Ni kweli gani inayohusiana ambayo imefunuliwa kwingineko katika maandiko?
- Ni kwa namna gani kweli hii inaongezeka katika ufahamu wetu?
- Je, tafsiri yangu inaweza kusahihishwa kwa kuzingatia maandiko kwa ujumla wake?
- Je, kweli hii inonekana kupingana na vifungu vingine? Kama ni hivyo, je, vinaweza kupatanishwa?

## Matumizi: Tengeneza Matumizi Kwa ajili ya leo

Kanuni ambazo umezipata zinaweza kutumika kwa namna tofauti tofauti. Fanya matumizi moja mahususi katika ulimwengu wa leo.

- Ni katika mazingira gani mahususi ya wakati wa leo ambapo ukweli huu unaweza kutumika?
- Je, ni lini, wapi, na kwa nani taarifa hizo zinafaa?
- Ni kwa namna gani ukweli unaweza kutumika katika kitendo na wazo?
- Kama nikikichukua kifungu kwa umakini sana, kitaniletea mabadiliko gani katika Maisha yangu?

Muulize Roho Mtakatifu kukuongoza katika kuliishi neno la Mungu anayeishi katika Maisha yako.

## Kufanyia Mazoezi Kutafsiri ya Nyaraka

Tunapotafsiri nyaraka za Agano Jipya, tunaanza kwa kuchunguza kwa kadiri inavyowezekana kuhusina na waraka, tunaendelea kuchunguza waraka ili kupata ujumbe wake, na tunamaliza kwa kutumia kanuni katika ulimwengu wetu. Safari hii ya tafsiri inatuchukua sisi kutoka ulimwengu wa wapokeaji wa kwanza hadi kwenye ulimwengu wa msomaji wa leo.

### Kufanyia Mazoezi Pamoja

► Pamoja kama darasa, fanyia kazi mchakato wa tafsiri kwa ajili ya 1 Yohana 2:15-17. Kama nyongeza ya maswali na mchakato wa tafsiri ulioelezewa hapo juu, kumbuka kujifunza yaliyomo katika nyaraka kama aina ya fasihi (ona Somo la 6).

### Kufanyia Mazoezi Peke Yako

► Kila mwanafunzi achukue mojawapo ya vifungu hivi na kufanyia mazoezi mchakato wa tafsiri. Kisha wanafunzi washirikishe hitimisho zao kwa wanakikundi katika kundi.

- Warumi 13:8-10
- Waefeso 6:18-20
- 2 Timotheo 4:6-8
- Yakobo 3:13-18
- 1 Petro 2:9-10

## Kufanyia Mazoezi ya Kutafsiri Sheria za Agano la Kale

Tunapotafsiri sheria za Agano la Kale, kwanza tunatakiwa kuelewa ilimaanisha nini kwa wapokeaji wa kwanza. Lazima tutazame kwa makini utofauti kati ya mazingira yao na yetu, hasa hasa utofauti wowote ambao unahusiana na ukweli kwamba tunaishi katika Agano Jipya. Katika sheria za Agano la Kale, tunatakiwa kutambua kanuni ambazo zitatendewa

kazi na watu wote wa nyakati zote. Kisha tunaweza kuzitumia kanuni hizi katika maisha yetu.

**Kufanyia Mazoezi Pamoja**

► Pamoja kama darasa, fanyia kazi mchakato wa tafsiri kwa ajili ya Hesabu 15:37-41. Kama nyongeza ya maswali na mchakato wa tafsiri ulioelezewa hapo juu, kumbuka kujifunza yaliyomo katika sheria za Agano la Kale kama aina ya fasihi na tumia maswali katika Somo la 6.

**Kufanyia Mazoezi Peke Yako**

► Kila mwanafunzi achukue mojawapo ya vifungu hivi katika mchakato wa tafsiri. Kisha wanafunzi washirikishe hitimisho zao kwa wanakikundi katika kundi.

- Mambo ya Walawi 19:9-10
- Kutoka 20:4-6
- Kutoka 22:10-13
- Kumbukumbu la Torati 14:1-2

## Somo la 10 Zoezi

Katika Somo la 1, ulichagua mojawapo ya vifungu hivi vya maandiko.

- Kumbukumbu la Torati 6:1-9
- Yoshua 1:1-9
- Mathayo 6:25-34
- Waefeso 3:14-21
- Wakolosai 3:1-16

Sasa kwa kuwa umefanyia kazi kila hatua ya safari ya tafsiri, fanya usomaji yakinifu wa kifungu ulichokichagua. Ukimaliza, andaa somo kutoka mojawapo kati ya mfumo huu:

1. Kama umekuwa ukisoma kozi katika kundi, utatakiwa kushirikisha ujifunzaji wako katika mawasilisho. (1) Onesha uchunguzi wako, (2) Fundisha kanuni kutoka katika andiko, na (3) Onesha namna ya kutumia andiko katika maisha ya mwamini leo.

2. Kama umekuwa unasoma peke yako, andika andiko lenye kurasa 5-6 ambapo utaelezea (1) Uchunguzi wako, (2) Kanuni kutoka katika andiko, na (3) Onesha namna ya kutumia andiko katika Maisha ya mwamini leo.

# Nyongeza
# Nyenzo za Kujifunzia Biblia

## Utangulizi

Vyanzo mbalimbali ni msaada kwa wafasiri wa Biblia. Kwa bahati mbaya, upatikanaji wa vyanzo hivi vya utafiti hutofautiana kulingana na lugha. Hapa tunaelezea kwa ufupi aina mbalimbali za vyanzo, ambavyo vinaweza kupatikana au visipatikane katika lugha yako. Baadhi ya vyanzo hivi ni vitabu vilivyochapishwa, wakati vingine vinaweza kupatikana kidijitali na vilevile katika chapisho.

## Aina za Vyanzo vya Kujifunza Biblia

### Vifaa vya Kutafuta Mistari Ambayo Inajumuisha Neno mahususi

Katika mchakato wa kutafsiri kifungu cha andiko, ainisha maneno muhimu. Sehemu moja ya kujifunza maneno haya ni kulinganisha matumizi yake katika vifungu vingine. Ili kufanya hivi, unahitaji kufahamu kuhusiana na vifungu vingine ambavyo vinatumia maneno yale yale.

Vifaa vifuatavyo vitakusaidia wewe kutafuta mistari mingine ambapo neno fulani linatumiwa katika toleo la Biblia katika lugha yako.

#### *Itifaki ya Biblia*

Itifaki inaorodhesha maneno yanayopatikana katika Biblia. Chini ya kila neno lililoingizwa yameorodheshwa marejeleo ya mistari ambayo neno hilo linaonekana.

Vitabu vikubwa vya itifaki vina kila neno kuu linalopatikana katika Biblia. Itifaki ndogo imewekwa nyuma ndani ya baadhi ya Biblia. Ina maneno machache na hazijumuishi kila aya kwa maneno hayo.

Itifaki inaweza kusaidia katika kujifunza ikiwa unaelewa uwezo na mapungufu yao. Mambo ya kukumbuka unapotumia itifaki ili kujifunza ni pamoja na:

1. Biblia ilitafsiriwa katika lugha yako kutoka Kiebrania na Kiyunani. Katika baadhi ya matukio, maneno mengi ya Kiebrania na Kiyunani yametafsiriwa kwa neno moja katika lugha yako. Ikiwa neno hilo hilo limetumiwa katika Biblia yako katika mistari miwili tofauti, hupaswi kufikiri kwamba lilitafsiriwa kutoka kwa neno lile lile la awali katika maeneo yote mawili.
2. Hata kama neno linalotumiwa katika sehemu mbalimbali katika Biblia yako halitokani na neno lilelile la awali katika Kiebrania au Kiyunani, kila matumizi yake katika Biblia yako ni kielelezo cha matumizi ya kawaida ya neno hilo wakati Biblia yako

ilipotafsiriwa. Kwa hiyo, una mifano ya matumizi mbalimbali ya neno. Hii ni muhimu unapoorodhesha maana zote zinazowezekana za neno hilo.

3. Baadhi ya itifaki huonyesha neno la asili la Kiebrania au kiyunani kando ya kila neno linaloingizwa. Hilo hukusaidia kujua ikiwa neno hilo katika lugha yako limetafsiriwa kutoka katika neno lile lile la Kiebrania au la kiyunani katika mistari mbalimbali iliyoorodheshwa.

4. Itifaki inayoonyesha maneno asilia pia inatoa ufafanuzi, kama kamusi. Hata hivyo, itifaki au kamusi kwa kawaida hutoa maana kadhaa zinazowezekana za neno, kwa hivyo ni lazima bado uangalie muktadha ili kubainisha maana ambayo mwandishi alikusudia.

***Programu za Biblia/Tovuti***

Ikiwa Biblia ya lugha yako inapatikana kwenye mtandao au kama programu, unaweza kutafuta neno, na tovuti au programu itakuonyesha mistari yote ambayo neno hilo linatumiwa.

**Kamusi za Biblia**

Kamusi za Biblia:

1. Zinatoa maelezo ya usuli (historia ya mambo ya nyuma) kuhusu maneno, maeneo na watu.

2. Zinatoa mifano ya mistari ambapo maneno yaliyoingizwa yametumika.

3. Huweza kueleza maana mbalimbali za neno katika sehemu mbalimbali.

Wakati mwingine kamusi za Biblia huchapwana kuwa vitabu. Kamusi za Biblia zinazotafutwa pia wakati mwingine hujumuishwa kwenye tovuti za kujifunza Biblia au katika programu ya Biblia.

**Vijitabu vya Mkononi vya Biblia**

Kijitabu cha mkononi cha mwongozo wa Biblia kinatoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia chenye taarifa za msingi kuhusu mwandishi na historia.

Ikiwa vijitabu cha mkononi cha mwongozo wa Biblia havipatikani katika lugha yako, tunapendekeza utumie utangulizi bila malipo wa kozi za Agano la Kale na Agano Jipya zinazotolewa na Shepherds Global Classroom. Kozi hizi hutoa msingi wa kila moja ya vitabu vya Biblia.

**Atlasi za Biblia**

Atlasi ya Biblia ina ramani za kila sehemu inayotajwa katika Biblia, picha za majiji ambayo yamechimbuliwa, na makala kuhusu ulimwengu wa kale.

Ramani na taarifa sawa zinapatikana kwenye baadhi ya tovuti pia.

### Tafsiri za Biblia

Endapo tafsiri moja au zaidi ya Biblia inapatikana katika lugha yako, kusoma kifungu chako cha kujifunza katika matoleo kadhaa kunaweza kuwa na faida sana. Kwa kutumia tovuti ya Biblia au programu, unaweza kulinganisha kifungu kwa kuonyesha tafsiri nyingi pembezoni.

Matoleo mbalimbali ya Biblia yanatafsiriwa kwa falsafa tofauti za tafsiri. Baadhi ya makundi ya watafsiri hujaribu kuhifadhi sarufi na muundo wa sentensi za maandiko ya awali ya Kiebrania au Kiyunani. Kwa kadiri inavyowezekana, huweka mpangilio wa maneno asilia na kugawanya sentensi kwa njia sawa na asilia.

Makundi mengine ya watafsiri hujaribu kuwasilisha ujumbe katika lugha iliyoboreshwa, wakati mwingine hubadilisha muundo wa sentensi ili kueleza dhana vizuri zaidi.

Ni vyema kuanza kujifunza kifungu katika tafsiri inayofuata kwa ukaribu muundo katika lugha asilia. Kisha unaweza kuangalia katika tafsiri zilizobadilishwa zaidi kwa kulinganisha.

Tovuti tatu za bure ambazo zina matoleo mengi ya Biblia katika lugha nyingi ni:

- http://www.biblegateway.com
- https://www.faithcomesbyhearing.com/audio-bible-resources/bible-is
- https://www.bible.com/

### Mfafanuzi ya Biblia

Vitabu vaya Mafafanuzi ya Biblia hutoa maelezo kwa kila mstari au kifungu katika Biblia. Mafafanuzi yanaweza kuchapishwa au kujumuishwa kwenye tovuti za kujifunza Biblia au katika programu ya kujifunza Biblia. Vitabu vingine vya ufafanuzi vilivyochapishwa vinashughulikia kitabu kimoja tu cha Biblia, na vingine vinashughulikia vitabu vingi, au Biblia nzima. Kwa sababu mafafanuzi yanaonyesha msimamo wa kitheolojia wa waandishi, lazima uwe mwangalifu.

### Usuli wa Biblia (historia ya nyuma ya mambo)

Mafafanuzi na vitabu kuhusu usuli wa Biblia vinatoa muktadha wa kitamaduni na kihistoria wa Biblia. Ufahamu wa tamaduni za ulimwengu wa Biblia utakupa ufahamu bora wa ujumbe wa maandiko.

Kwa mfano, mifano ya Yesu inategemea utamaduci wa siku zake; vitabu vya Musa mara nyingi hujibu mazoea ya tamaduni za kuabudu sanamu za majirani wa Israeli; maandiko ya Paulo yanaelekezwa kwa Wakristo wanaoishi katika ulimwengu wa watu wanaoabudu miungu. Tunapoelewa usuli huu, tunawezeshwa zaidi kutafsiri mafundisho ya maandiko.

**Biblia za Mafunzo**

Biblia nzuri ya mafunzo ni ile ambayo, Biblia, mafafanuzi, Vijitabu vya Mkononi vya Biblia, itifaki ya Biblia, na atlasi zote katika kitabu kimoja. Biblia ya mafunzo ni mwanzo mzuri wa kujifunza kwako. Ni nyenzo iliyochapishwa, lakini kama ilivyotajwa hapo awali, tovuti zingine za masomo ya Biblia au programu vile vile ni muhimu kwa namna nyingi.

# Vyanzo Vinavyopendekezwa

**Somo la 1**

Vyanzo ambavyo vimetumika wakati wote wa kozi hii vimeorodheshwa hapa.

Biblia. *Swahili Union Version*.

Carson, D.A. *Exegetical Fallacies* (2nd edition). Ada: Baker Books, 1996.

Duvall, J. Scott and J. Daniel Hays. *Grasping God's Word: A Hands-On Approach to Reading, Interpreting, and Applying the Bible.* Grand Rapids: Zondervan, 2012.

Fee, Gordon D. and Douglas Stuart. *How to Read the Bible for All Its Worth*. Grand Rapids: Zondervan, 2003.

Hendricks, Howard G. and William D. Hendricks. *Living by the Book.* Chicago: Moody Press, 2007.

Klein, William W., Craig L. Blomberg, and Robert L. Hubbard, Jr. *Introduction to Biblical Translation.* Nashville: Thomas Nelson, 1993.

Virkler, Henry A. and Karelynne Ayayo. *Hermeneutics: Principles and Processes of Biblical Interpretation*. Ada: Baker Books, 2007.

Zuck, Roy B. *Basic Bible Interpretation*. Colorado Springs: David C. Cook, 1991.

**Somo la 2**

Vyanzo hivi vinapatikana katika mtandao bila gharama yeyote

Biblia za Sauti. www.faithcomesbyhearing.com

Kamusi za Biblia. www.biblestudytools.com/dictionaries/

Kalenda za Usomaji wa Biblia. www.bible.com

Tafsiri za Biblia. www.biblegateway.com

Atlasi ya Biblia ya Mtandaoni. www.bibleatlas.org

**Somo la 4**

Mihadhara hii ya mtandaoni juu ya kutafsiri Biblia inaweza kukupa wewe uelewa wa ndani wa kutafsiri Biblia.

Dr. Walter Martin. "Biblical Hermeneutics One by Dr. Walter Martin." Inapatikana katika www.youtube.com/watch?v=mJQGVzlLN-Y

Seven Minute Seminary. "Why Bible Background Matters." Inapatikana katika www.youtube.com/watch?v=-wiIK8A2EFk

Seven Minute Seminary. "The Role of Archaeology in Biblical Studies." Inapatikana katika www.youtube.com/watch?v=Dm3HlLoNOak

# Rekodi ya Mazoezi

Jina la Mwanafunzi ________________________________________

Herufi za awali za majina zitaandikwa kila wakati zoezi linapokamilika. Mazoezi yote yanatakiwa kukamilishwa kikamilifu ili kupokea cheti kutoka Shepherds Global Classroom.

| Somo | Mazoezi | |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |

Maombi ya cheti kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa katika tovuti yetu ya www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitahamishwa kutoka kwa raisi wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi kwa niaba ya wanafunzi wao.